
NGAZI YA
KUFIKIA
MBINGUNI

Masihi anakuja, na **Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili! Soma ili usikose kuwa mbinguni siku moja. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu, na wale wote waliotusaidia katika kutafsiri hiki kitabu-** Washauri, Watafsiri, Wahariri, watu wa Teknolojia, na Watu wenye kutia moyo na maombezi. Tudumu kuombeana

1. Grace Masaka Momadi, Jersey, Marekani
2. Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
3. Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
4. Kwandu Kasiri-Mpagalushu-Bariadi, Tanzania
5. Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania
6. Jabez Masaka-North Carolina, Marekani
7. Daniel Masaka-Kisii, Kenya
8. Denis Masaka-Jersey, Marekani
9. Yunus Tiras Magira-Mara, Tanzania

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

## Dibaji

Vitabu vichache husambazwa kwa mamilioni au vina ushawishi mkubwa katika kuinua ubinadamu kama vile kitabu hiki cha Ngazi ya kufika Mbinguni au ***Steps to the Messiah katika Kiingereza***. Katika matoleo mengi, kitabu hiki kidogo kimechapishwa katika lugha zaidi ya 160, na kuwahuisha (inspire) mamilioni ya wanaume na wanawake kote ulimwenguni, hata wale wanaoishi katika pembe za mbali za dunia. Kuanzia kuonekana kwa toleo la

kwanza, mnamo 1892. Kitabu hiki kimetoa faraja kwa mamilioni, na watu wengi wamegeuza hatua zao kutoka kwenye maanguko.

Vitabu vya Roho ya Unabii, au kalamu yenye matumaini, ni msaada katika nyanja mbali-mbali kama vile afya, familia, ndoa, malezi. Kichwa cha kitabu kinaelezea dhamira yake. Kinamwelekeza msomaji kwa Yesu Kristo, kwamba Ndiye pekee anayeweza kukidhi mahitaji ya moyo. Kinaelekeza miguu ya wenye mashaka na wanaosimama katika njia panda kwa kutojua cha kufanya, kwenye njia ya amani. Kinamwongoza mtafutaji wa haki na ukamilifu wa tabia, hatua kwa hatua, ngazi kwa ngazi, katika njia ya maisha ya Kikristo. Kwenye uzoefu huu, ndipo ambapo mwanadamu anaweza kujua ukamilifu wa baraka unaopatikana katika kujisalimisha kikamilifu kwa moyo-nafsi. Kinamfunulia mwandamu siri ya ushindi kwa urahisi kwa kumweka kwenye neema ya kuokoa na nguvu ya kulinda ya Rafiki mkuu wa wanadamu wote, naam MWENYEZI MUNGU MWENYEWE.

Yakobo, mzee wa imani wa zamani, alipoteswa na hofu kwamba dhambi yake ilikuwa imemtenga na Mungu, alilala chini kupumzika, na kisha "akaota, na tazama ngazi ilikuwa imesimamishwa juu ya nchi, na kilele chake kilifika mbinguni." Kwa hivyo uhusiano kati ya dunia na mbingu ulifunuliwa kwake, na maneno ya faraja na tumaini yalisemwa kwa mzururaji Yakobo, na Yeye aliyesimama juu ya ngazi inayoweka kivuli, ili kwamba maono ya mbinguni yaweze kurudiwa kwa wengi wanaposoma kisa hiki cha njia ya uzima, hakika haya ndiyo matakwa ya dhati ya wachapishaji, na—

Muhtasari wa hiki kitabu umetangulia, na mwongozo wa sura kwa sura wenye maswali ya kujifunzia na kuelewa kitabu hiki, upo nyuma, pamoja na masomo ya Biblia rahisi ya kumsaidia mtu kujua maana ya maisha na jinsi ya kuishi katika dunia yetu hii. Haya ni muhimu kwa vile tunaamimi kwamba Masihi anarudi hivi karibuni, nasi tumepewa nafasi ya kujitayarisha. Kauli mbiu yetu ni uwe tayari, uwe tayari, uwe tayari, Masihi anarudi hivi karibuni!

## YALIYOMO

SURA YA 1—UPENDO WA MUNGU KWA MWANADAMU………………4
SURA YA 2 - HITAJI LA MWENYE DHAMBI LA KRISTO……………….9
SURA YA 3 - TOBA…………….……………………………………………..13
SURA YA 4 - UNGAMO…………….………………………………………..22
SURA YA 5 - KUJIWEKA WAKFU……………………………………25
SURA YA 6 - IMANI NA KUKUBALI…………………………………29
SURA YA 7 – KIPIMO CHA UANAFUNZI………………………………33
SURA YA 8 - KUKUA KATIKA KRISTO………………………………39
SURA YA 9 - KAZI NA UZIMA………………………………………45
SURA YA 10 - MAARIFA YA MUNGU……………………………………50
SURA YA 11 - FURSA YA MAOMBI……………………………………55
SURA YA 12 – NIFANYE NINI KUHUSU MASHAKA…………………65
SURA YA 13 - KUFURAHI KATIKA BWANA……………………………..71

## MUHTASARI WA KITABU CHA NGAZI YA KUFIKIA MBINGUNI UPO MWISHO WA KITABU (STEPS TO the Messiah)

### SURA YA 1—UPENDO WA MUNGU KWA MWANADAMU

Asili na ufunuo kwa pamoja hushuhudia juu ya upendo wa Mungu. Baba yetu aliye mbinguni Ndiye chanzo cha uzima, hekima, na furaha. Vitazame vitu vya ajabu na vya kupendeza vya asili-uumbaji. Fikiria juu ya upatanifu wake wa kustaajabisha kwa ajili ya mahitaji na furaha ambayo sio ya mwanadamu tu, bali ya viumbe vyote vilivyo hai. Mwangaza wa jua na mvua, vinavyoifurahisha na kuiburudisha dunia, vilima na bahari na tambarare, vyote hivi hutuambia juu ya upendo wa Muumba. Ni Mungu Ndiye anayetoa mahitaji ya kila siku ya viumbe Vyake vyote. Kwa Maneno mazuri ya mwandishi wa Zaburi, alisema— {SCsw 9.1}

***Macho ya watu wote yakuelekea Wewe, Nawe huwapa chakula chao kwa wakati wake. Waufumbua mkono Wako, Wakishibisha kila kilicho hai matakwa yake*** **Zaburi 145:15-16.— {SCsw 9.2}**

Mungu alimuumba mwanadamu kuwa mtakatifu, mkamilifu na mwenye furaha; na aliiumba dunia nzuri, vyote hivi vilitoka mkononi mwa Muumba, bila hata alama au doa la uharibifu wala

kivuli cha laana. Ni uvunjaji wa sheria ya Mungu—sheria ya upendo—ndio ulioleta huzuni na mauti. Ingawa hali kama ilivyo, ni hivyo, hata katikati ya mateso yanayotokana na dhambi, upendo wa Mungu bado unadhihirishwa. Imeandikwa katika Kitabu cha **Mwanzo 3:17,** kwamba Mungu aliilaani ardhi, kwa kumsaidia mwanadamu. Michongoma na miiba—yaani, magumu na majaribu yanayofanya maisha yake kuwa ya taabu na mashaka—yaliteuliwa kwa ajili ya mema yake, kama sehemu ya mafunzo yanayohitajika katika mpango wa Mungu kwa ajili ya kumwinua mwanadamu, kutoka katika uharibifu na udhalilishaji ambao dhambi imeleta. Dunia, ingawa imeanguka, sio yote yana huzuni na mateso. Kupitia asili yenyewe kuna ujumbe wa tumaini na faraja. Kuna maua juu ya michongoma, na miiba imefunikwa na maua ya waridi — **{SCsw 9.3}**

"***Mungu ni upendo***" imeandikwa juu ya kila chipukizi linalotokeza kwenye mimea, juu ya kila shina la mti wenye majani mabichi yanayochipuka. Ndege wazuri wanaoimba kwa furaha hewani, maua nyororo yenye rangi maridadi, katika ukamilifu wake, yakitoa harufu nzuri hewani, miti mirefu ya msituni, yenye majani yake mengi ya kijani kibichi—yote haya yanashuhudia kujali na huruma nyororo, za Baba Mungu wetu na matamanio Yake ya kuwafanya watoto Wake wafurahi. **{SCsw 10.1}**

**Neno** la Mungu linafunua tabia Yake. Yeye Mwenyewe ametangaza upendo Wake usio na mipaka, sikitiko na huruma Yake. Wakati Musa alipoomba, ***Nakusihi unionyeshe utukufu Wako***. Bwana akamjibu Akasema, ***Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako, Nami nitalitangaza Jina la Bwana mbele yako; Kutoka 33:18-19.*** Huu ndio utukufu Wake. *“Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli; Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, Mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi” Kutoka 34:6-7. Yeye "sio mwepesi wa*

*hasira, U mwingi wa rehema" kwa maana Yeye hufurahia rehema. Yona 4:2, Mika 7:18.* {SCsw 10.2}

Mungu ameifunga mioyo yetu Kwake kwa ishara zisizohesabika mbinguni na duniani. Kupitia vitu vya asili, na vifungo vya mahusiano ya kina, nyeti, yenye ukaribu kabisa na upendo mwanana, huruma nyororo na ya juu zaidi, ya kidunia, ambayo mioyo ya wanadamu inaweza kujua, naam, Yeye Ametafuta kujifunua Mwenyewe kwetu. Hata hivyo, mambo haya yanawakilisha kwa ukamilifu mdogo tu, upendo Wake. Ingawa ushahidi huu wote umetolewa, adui wa mema alipofusha akili za wanadamu, hata wakamtazama Mungu kwa hofu; walimdhania kuwa ni mkali na asiyesamehe. Shetani aliwaongoza wanadamu kumfikiria Mungu kama nafsi ambayo sifa yake kuu ni kushugulikia haki kwa ukali na adhabu, bila msamaha,—kwamba ni mwamuzi mkali, mgumu sana, anayedai malipo kwa ukali. Adui alimwonyesha Muumba kama kiumbe anayetazama kwa jicho la wivu ili kubaini makosa na mapungufu ya wanadamu, ili aweze kuwakamata watu na kuwapatiliza kwa hukumu. Ilikuwa ni kwaajiili ya kuondoa kivuli hiki cha giza, ndiyo kwamba Yesu alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu ili kuufunulia ulimwengu upendo usio na kikomo wa Mungu, {SCsw 10.3}

Mwana wa Mungu alikuja kutoka mbinguni ili kumdhihirisha Baba. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, Huyu Ndiye aliyemfunua. Yohana 1:18. Wala hakuna amjuaye Mwana, ila Baba; na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia. Mathayo 11:27. Mmoja wa wanafunzi alipotoa ombi hilo Mwana wa Mungu kwamba, "Utuonyeshe Baba" Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona Mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Yohana 14:8-9 {SCsw 11.1}

Katika kuelezea utume Wake hapa duniani, Yesu alisema,

"Kwa maana Bwana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa" Luka 4:18. Hii ndiyo ilikuwa kazi Yake. Alizunguka-zunguka akitenda mema na kuwaponya wote walioteswa na Shetani. Kulikuwa na vijiji vizima ambapo hapakuwa na kilio cha ugonjwa katika nyumba yoyote, kwani alikuwa amepita katikati yao na kuwaponya wagonjwa wao wote. Kazi Yake ilitoa ushahidi wa mpako wa mafuta wa Kiungu. Upendo mwanana, kujali, rehema, na huruma nyororo, vilifunuliwa katika kila tendo la Maisha Yake; moyo Wake ulikwenda kwa huruma nyororo na kujali watoto wa wanadamu. Aliitwaa asili ya mwanadamu, ili aweze kufikia mahitaji ya mwanadamu. Maskini, watu wa tabaka la chini na wanyenyekevu hawakuogopa kumkaribia. Hata watoto wadogo walivutiwa Naye. Walipenda kupanda kwenye magoti Yake na kutazama uso Wake wa tafakari, uliokuwa umejaa wema, ukarimu na upendo. {SCsw 11.2}

Yesu hakuficha neno hata moja la Kweli, lakini alilisema kwa upendo kila wakati. Alitumia busara kubwa na tafakari/uangalifu wa dhati na wema katika mahusiano Yake na watu. Hakuwahi kuwa mkorofi na kutenda kwa jeuri, hakuwahi kusema neno kali bila sababu, hakuwahi kuumiza nafsi nyeti, inayokwazika kirahisi. Hakuhukumu udhaifu wa mwanadamu. Alizungumza Ukweli, lakini kila wakati kwa upendo. Alishutumu unafiki, kutoamini, na uovu; lakini machozi yalikuwa katika sauti Yake alipotoa maonyo Yake makali. Aliulilia Yerusalemu, mji alioupenda, ambao ulikataa kumpokea Yeye, ambaye Ndiye Njia, Kweli, na Uzima. Watu walikuwa wamemkataa Mwokozi, lakini Yeye aliwatazama kwa huruma ya upendo. Maisha Yake yalikuwa ya kujikana nafsi na kuwajali wengine. Kila roho, ilikuwa ya thamani machoni Pake. Ingawa alikuwa na asili ya mwandamu na hadhi ya Mungu ndani Yake, alijishusha kwa upendo mwanana, huruma nyororo,

mahusiano ya vifungo vya karibu na wema mkubwa, kwa kumjali kila muumini wa familia ya Mungu. Katika watu wote Aliona roho zilizoanguka ambazo ilikuwa ni utume Wake kuwaokoa. {SCsw 12.1}

Hiyo ndiyo tabia ya Kristo kama ilivyofunuliwa katika maisha Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu. Ni katika moyo wa Baba, ndipo ambapo vijito vya huruma ya Kiungu, vinadhihirishwa katika Kristo, na hutiririka hadi kwa wanadamu. Yesu, Mwokozi aliye mpole, Mwenye upendo, wema, huruma nyororo na Mwenye kutusikitikia, alikuwa Mungu “aliyedhihirishwa katika mwili.” 1 Timotheo 3:16. {SCsw 12.2}

Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa sisi kwamba Yesu aliishi, akateseka na kufa. Alikuwa "Mtu wa huzuni," ili tuweze kufanywa washiriki wa furaha ya milele. Mungu alimruhusu Mwanawe mpendwa, aliyejaa neema na Kweli, kutoka katika ulimwengu wa utukufu usioelezeka, hadi katika ulimwengu ulioharibiwa na kukumbwa na hali mbaya ya dhambi, ndiyo, limwengu uliotiwa giza na kivuli cha mauti na laana. Alimruhusu kuondoka kifuani mwa upendo Wake, kuacha ibada ya malaika, ili apate aibu, matusi, fedheha, chuki, na kifo. "Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Isaya 53:5. Mtazame akiwa nyikani, huko Gethsemane, msalabani! Mwana wa Mungu asiye na doa alibeba juu Yake mzigo wa dhambi. Yeye ambaye alikuwa mmoja na Mungu, alihisi katika nafsi Yake, utengano mbaya ambao dhambi huleta kati ya Mungu na mwanadamu. Hili lilikamua kilio chenye uchungu kinywani Mwake, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Mathayo 27:46. Ulikuwa ni mzigo wa dhambi, kutambua ukubwa wa ubaya wake, utengano wa roho Yake, kutoka kwa Mungu—ndio vilivyovunja moyo wa Mwana wa Mungu. {SCsw 13.1}

Lakini dhabihu hii kubwa haikutolewa ili kutengeneza ndani ya moyo wa Baba upendo kwa mwanadamu, sio kitu

kilichomfanya Mwenyezi Mungu awe tayari kumwokoa mwanadamu. Hapana, hapana! "Kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee." Yohana 3:16. Baba anatupenda, sio kwa sababu ya upatanisho mkuu, bali alifanya/alitoa upatanisho kwa sababu anatupenda sisi wanadamu. Kristo alikuwa njia ambayo Baba angeweza kumimina upendo Wake usio na kikomo juu ya ulimwengu ulioanguka. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake." 2 Wakorintho 5:19. Mungu aliteseka pamoja na Mwanawe. Katika maumivu makali ya Gethsemane, kifo cha Kalvari, moyo wa Upendo Usio na Kikomo, ulilipa gharama ya ukombozi wetu. {SCsw 13.2}

Yesu alisema, Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai Wangu ili niutwae tena. Yohana 10:17 Yaani, "Baba Yangu amewapenda ninyi sana hivi kwamba ananipenda Mimi zaidi kwa kutoa uhai Wangu ili kuwakomboa. Kwa Mimi kuwa Mbadala na Mdhamini wenu, kwa kuusalimisha uhai Wangu, kwa kuchukua madeni yenu, na makosa yenu, Mimi nimependwa na Baba Yangu; kwani kwa dhabihu Yangu, yote mawili yamewezekana, kwamba Mungu ambaye ni Mwenye haki, bado anaweza kwa wakati huo huo, kumhesabia haki yeye amwaminiye Yesu." (mdhambi anayemwamini, anaweza kuhesabiwa haki, na bado Mungu akawa ametenda haki!) {SCsw 14.1}

Hakuna mwingine isipokuwa tu Mwana wa Mungu ambaye angeweza kutimiza ukombozi wetu; kwa maana ni Yule tu aliyekuwa kifuani mwa Baba, Ndiye angeweza kumtangaza Yeye. Ni Yule tu aliyejua urefu na kina cha upendo wa Mungu Ndiye ambaye angeweza kuudhihirisha. Hakuna chochote kilicho pungufu ya hii dhabihu, isiyo na kikomo iliyotolewa na Kristo kwa niaba ya mwanadamu aliyeanguka, ambacho kingeweza kuuonyesha upendo wa Baba kwa wanadamu waliopotea. {SCsw 14.2}

"Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee." Yeye Hakumtoa tu ili aishi kati ya wanadamu, kubeba dhambi zao, na kufa kama dhabihu kwa ajili yao. Alimtoa kwa kizazi kilichoanguka. Kristo alipaswa kujitambulisha na maslahi na mahitaji ya ubinadamu. Yeye ambaye Alikuwa Mmoja na Mungu, amejifungamanisha na watoto wa wanadamu kwa vifungo ambavyo haviwezi kuvunjwa kamwe. Yesu "haoni haya kutuita sisi ndugu" (Waebrania 2:11); Yeye Ndiye Dhabihu yetu, Mtetezi wetu, Ndugu yetu, akiwa amebeba umbo letu la kianadamu mbele ya kiti cha enzi cha Baba, na katika zama zote akiwa pamoja na jamii ambayo ameikomboa—Mwana wa Adamu. Na haya yote ili mwanadamu ainuliwe kutokana na aibu na uharibifu wa dhambi na maadili/hadhi Iliyoshuka chini, ili aweze kuakisi upendo wa Mungu na kushiriki furaha ya utakatifu. {SCsw 14.3}

Bei iliyolipwa kwa ajili ya ukombozi wetu, dhabihu isiyo na kikomo ya Baba yetu wa mbinguni kwa kumtoa Mwanawe afe kwa ajili yetu, inapaswa kutupa mawazo yaliyoinuliwa kuhusu kile tunachoweza kuwa kupitia Kristo. Mtume Yohana, aliyevuviwa, alipoona kimo, kina, na upana wa upendo wa Baba kwa jamii inayoangamia, alijawa na sifa, kicho, upendo na heshima; na akishindwa kupata lugha inayofaa ya kuonyesha ukuu na wema na huruma za upendo huu, aliusihi ulimwengu kutazama ili ujionee wenyewe- "Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu" 1 Yohana 3:1 Hii inampa mwanadamu thamani iliyoje! Kupitia uasi wa wana wa mwanadamu wanakuwa raia wa Shetani. Kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho ya Kristo, wana wa Adamu wanaweza kuwa wana wa Mungu. Kwa kuchukua asili ya kianadamu, Kristo huwainua wanadamu. Wanadamu walioanguka wamewekwa mahali ambapo, kupitia muunganiko na Kristo, wanaweza kweli kustahili jina la "wana wa Mungu." {SCsw 15.1}

Upendo kama huo hauna uwiano. Kwamba sisi tu watoto wa

Mfalme wa mbinguni! Ahadi ya thamani iliyoje! Mada ya kutafakari kwa kina zaidi! Upendo wa Mungu ulioshehen, usio na mfanano, kwa ulimwengu ambao haukumpenda! Wazo hilo lina nguvu ya kutiisha roho na huiteka nia na akili, viyaendee mapenzi ya Mungu. Kadiri tunavyojifunza zaidi tabia ya Mungu katika nuru ya msalaba, ndivyo tunavyoona zaidi rehema, huruma nyororo ya hali ya juu, wema, na msamaha vikiwa vimechanganyika na usawa na haki, na ndivyo tunavyozidi kutambua ushahidi usio na kifani, wa upendo usio na kikomo, na huruma yenye matamanio, yanayozidi huruma ya mama kwa mtoto wake mpotovu. {SCsw 15.2}

**[Neno lililotumika hapa mara nyingi, ni gumu kulitafsiri Kiswahili!**

**"Tenderest ties" refers to the deepest, most intimate, and sacred emotional bonds that connect human beings, typically characterized by profound love, affection, and mutual care. It represents the strongest form of attachment in relationships, often associated with vulnerability, gentleness, and lasting**

**Tender sympathy refers to a deeply felt compassion, warmth, and gentle concern for someone's suffering or loss, often emphasizing emotional connection and active care over mere pity. It embodies an "affected heart" that is moved to kindness, offering comfort during difficult times through thoughtful support and validation.**

**Pitying tenderness is a complex emotion combining gentle affection or concern with a sense of sorrow for another's distress. It often involves a desire to support the vulnerable or hurting person, often from a standpoint of unequal positions, distinguishing it from mutual empathy**

"Uhusiano mnyenyekevu na laini zaidi" hurejelea vifungo vya kihisia vya ndani zaidi, vya karibu zaidi, na vifungo vitakatifu vinavyowaunganisha wanadamu, ambavyo kwa kawaida hujulikana kwa upendo mkubwa, upendo mwanana, kujali, huruma nyororo, mapenzi, jotojoto, moyo kuumia mno kwaajili ya mateso au hasara ya mtu, moyo uliosukumwa kwa wema, kutoa faraja, mapenzi yenye ulaini wa moyo, hisia za huzuni kwa mwingine, kusaidia, kujali na utunzaji wa pande zote. Huwakilisha aina nzito/kali zaidi ya uhusiano katika mahusiano, mara nyingi huhusishwa na unyonge, upole, kumsaidia asiyejiweza, hamu ya kumsaidia mtu aliye katika mazingira magumu au aliyeumiana mwendelezo wa kudumu.

## SURA YA 2 - HITAJI LA MWENYE DHAMBI LA KRISTO

Hapo awali, mwanadamu alipewa nguvu za kiwango cha juu na akili yenye utimamu, na msawaziko mzuri (balansi). Alikuwa mkamilifu katika utu wake, na katika maelewano/upatanifu na Mungu. Mawazo yake yalikuwa safi, malengo yake matakatifu. Lakini kwa kukosa utii, nguvu zake zilipotoshwa, na ubinafsi ukachukua nafasi ya upendo. Asili yake ilidhoofika sana kutokana na uasi, hivyo kwamba haikuwezekana kwake, kwa nguvu zake mwenyewe, kupinga nguvu za uovu. Akafanywa kuwa mateka wa Shetani, na angebaki hivyo milele endapo Mungu asingeingilia kati kwa namna ya pekee. Ilikuwa ni kusudi la mjaribu kuzuia mpango wa Kiungu katika uumbaji wa mwanadamu, na kuijaza dunia kwa huzuni na uharibifu. Na angeonyesha uovu huu wote kwamba ndiyo matokeo ya kazi ya Mungu katika kumuumba mwanadamu. {SCsw 17.1}

Katika hali yake ya kutokuwa na dhambi, mwanadamu alikuwa na ushirika wa furaha na Yeye "ambaye ndani Yake Yeye

hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika" Wakolosai 2:3. Lakini baada ya dhambi yake, hakuweza tena kupata furaha katika utakatifu, na akatafuta kujificha ili Mungu asimwone-asiwepo mbele za uwepo wa Mungu. Hiyo bado, ndiyo hali ya moyo ambao haujafanywa upya. Haupatani na Mungu, na haushangilii na kuwa na furaha katika kuwa na ushirika Naye. Mwenye dhambi hangeweza kuwa na furaha mbele za Mungu; angeepa kuwa na ushirika wa/na viumbe watakatifu. Hata kama angeruhusiwa kuingia mbinguni, kwake lisingekuwa jambo la kumletea yeye furaha. Roho ya upendo usio na ubinafsi inayotawala hapo mbinguni—kila moyo unaoitikia moyo wa Upendo Usio na Mwisho—usingeamsha chochote chenye kuleta mwitikio ndani ya nafsi yake. Mawazo yake, maslahi yake, nia zake, zingekuwa ngeni kwa zile zinazowahamasisha wakazi wasio na dhambi huko mbinguni. Angekuwa noti isiyolingana katika wimbo wa mbinguni. Mbingu ingekuwa kwake mahali pa mateso; angetamani kufichwa mbele Zake ambaye ni nuru yake, na kitovu cha furaha yake. Sio amri iliyotolewa kiholela, bila ya msingi, kwa upande wa Mungu kwamba hiyo ndiyo inayowatenga waovu kutoka mbinguni; Waovu wamefungiwa nje kwa kutofaa kwao wenyewe, kuwa katika ushirika Wake Mwenyezi Mungu. Utukufu wa Mungu ungekuwa kwao moto ulao. Wangekaribisha uangamivu, ili wafichwe kutoka kwa uso wa Yeye ambaye alikufa ili kuwakomboa. **{SCsw 17.2}**

Haiwezekani kabisa kwetu, sisi wenyewe, kuponyoka kutoka kwenye shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni miovu, na wala hatuwezi kuibadilisha. Ni nani awezaye kuleta kitu kilicho safi kutoka ndani ya kitu kilicho kichafu? Hapana hata mmoja awezaye. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Ayubu 14:4; Warumi 8:7. Elimu, utamaduni, desturi, kuzoesha nia na mapenzi ya mtu, juhudi za kibinadamu, vyote vina "mahali pake sahihi, lakini hapa havina nguvu. Vinaweza kuleta matokeo ya

"usahihi wa nje wa tabia, lakini haviwezi kubadilisha moyo;" haviwezi kutakasa chemchemi za uzima. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya mwanadamu kubadilishwa kutoka "dhambini hadi utakatifu." Nguvu hiyo ni Kristo. Neema Yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha "nguvu za vitivo vya roho visivyo na uhai, na kuvivutia kwa Mungu, hadi utakatifu. **{SCsw 18.1}**

Mwokozi alisema, “Mtu asipozaliwa upya mara ya pili”, pasipo kupokea moyo mpya, matamanio, malengo, nia na mapenzi mapya, mwanadamu “hawezi kuuona ufalme wa Mungu Yohana 3:3 Wazo kwamba ni muhimu tu kuendeleza mema ambayo yapo ndani ya mwanadamu kwa asili, ni udanganyifu, uletao kifo. "Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni. Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.1Wakorintho 2:14, Yohana 3:7. Kuhusu Kristo imeandikwa" Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa ni nuru ya watu"-Jina pekee chini ya mbingu walilopewa wanadamu, litupasalo sisi kuokolewa kwalo.” Yohana 1:4, Matendo ya Mitume 4:12. **{SCsw 18.2}**

Haitoshi kuitambua na kuitazama tu tabia ya Mungu, upendo na fadhili Zake, kuona wema Wake, ukarimu na huruma nyororo ya Baba. Haitoshi kutambua tu hekima na haki ya sheria Yake, kuona kwamba imejengwa juu ya kanuni ya milele ya upendo. Paulo mtume alipoona haya yote, alitangaza kwa kushangilia, mimi “Naikiri ile sheria ya kuwa ni njema.” Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema. Lakini aliongeza, katika uchungu wa nafsi yake-uchungu na kukata tamaa, kwaajili ya majonzi ya moyo, "bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi." Warumi 7:16, 12, 14, Alitamani sana kupata usafi wa moyo, kutakaswa, na haki, ambayo ndani yake mwenyewe, hakuwa

na uwezo wa kuvipata hivi vitu, naye akapaaza sauti kwa kulia, Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Warumi 7:24. Hiki ndicho kilio kilichopanda kutoka kwa mioyo yenye mizigo katika nchi zote na katika vizazi vyote. Kwa wote, kuna jibu moja tu, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Yohana 1:29 **{SCsw 19.1}**

Kuna mifano mingi ambayo Roho wa Mungu ameitumia ili kuufafanua Ukweli huu, na kuufanya uwe wazi kwa wanadamu wanaotamani kuwekwa huru kutokana na mzigo wa hatia. Wakati, baada ya dhambi yake ya kumdanganya Esau, Yakobo alipokimbia kutoka nyumbani kwa baba yake, alilemewa na hisia ya hatia. Akiwa mpweke na mkimbizi asiye na makazi, aliyetengwa na yote yaliyofanya maisha kuwa ya thamani, maana na furaha, wazo moja ambalo liliishinikiza roho yake juu ya yote, lilikuwa hofu kwamba dhambi yake ilikuwa imemtenga na Mungu, kwamba alikuwa ameachwa na Mbingu. Kwa huzuni alilala chini ili apumzike kwenye ardhi tupu, bila ya matandiko, akizungukwa na vilima vya upweke tu, na juu yake, mbingu zenye nyota angavu. Alipokuwa amelala, nuru ya ajabu ilimwangazia wakati akiwa katika maono yake; na tazama, kutoka uwanda aliokuwa amelala, ngazi zenye upana mkubwa na kivuli zilionekana kuongoza juu hadi malango ya mbinguni kabisa, na juu yake malaika wa Mungu walikuwa wakipanda juu na kushuka chini; na wakati huo-huo kutoka katika utukufu wa juu, sauti ya Kiungu ilisikika katika ujumbe wa faraja na tumaini. Hivyo Yakobo alijulishwa kile kilichokidhi hitaji na matamanio ya roho yake—Mwokozi. Kwa furaha na moyo wa shukrani aliona njia iliyofunuliwa ambayo yeye, mwenye dhambi, angeweza kurejeshwa kwenye ushirika na Mungu. Ngazi ya ajabu ya ndoto yake ilimwakilisha Yesu, njia pekee ya mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu. **{SCsw 19.2}**

Huu ndio mfano ule ule ambao Kristo alirejelea katika mazungumzo Yake na Nathanaeli, aliposema "***Mtaziona mbingu***

***zimefunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu".*****Yohana 1:51.** Katika uasi, mwanadamu alijitenga mwenyewe na Mungu; dunia ilikatiliwa mbali na mbingu. Kutokana na korongo kubwa lililokuwepo kati yake na Mungu, hapakuwezekana kuwa na mawasiliano (ushirika) yoyote. Lakini kupitia kwa Kristo, dunia imeunganishwa tena na mbingu. Kwa sifa/stahili Zake Mwenyewe, Kristo amekuwa daraja kwenye lile korongo kubwa ambalo dhambi ilikuwa imelitengneza, ili Malaika wahudumuo waweze kufanya mawasiliano na ushirika na mwanadamu. Kristo anamuunganisha mwanadamu aliyeanguka katika udhaifu na kutokuwa na msaada kwake na Chanzo cha nguvu zisizo na kikomo. **{SCsw 20.1}**

Ndoto za mwanadamu za kupiga hatua, za maendeleo ni batili tu, jitihada zote za kuboresha hali ya binadamu ni kazi bure tu, ikiwa wanapuuza Chanzo pekee cha tumaini na msaada kwa jamii ya wanadamu iliyoanguka. "Kila kutoa kuliko kwema, na kila kipawa kilicho kamili" (Yakobo 1:17) hutoka kwa Mungu. Hakuna ubora wa kweli wa tabia kando ya Yeye. Na njia ya pekee ya kumfikia Mungu ni Kristo. Yeye asema, "Mimi Ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi." Yohana 14:6. **{SCsw 21.1}**

Moyo wa Mungu una hamu/matamanio kwa watoto Wake wa duniani kwa upendo ulio na nguvu kuliko mauti. Kwa kumtoa Mwana Wake, Yeye amemimina kwetu mbingu yote katika kipawa kimoja. Maisha ya Mwokozi na kifo Chake na maombezi Yake, huduma ya malaika, kusihi kwa Roho, ufanyaji kazi wa Baba juu na kupitia yote, maslahi na shauku isiyokoma ya viumbe wa mbinguni—vyote vimehusishwa kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. **{SCsw 21.2}**

Loo, hebu na tutafakari dhabihu hii ya ajabu ambayo imefanywa/imetolewa kwa ajili yetu! Hebu na tujaribu kuthamini na kuwa na shukrani kwa kazi na nishati ambazo Mbingu inatumia

ili kuwarejesha wanadamu waliopotea, warudi tena katika nyumba ya Baba. Sababu zenye nguvu zaidi, na mawakala wenye uwezo zaidi, havingeweza kamwe kuwekwa katika utendaji; thawabu zilizo kuu sana, kwa kutenda yaliyo sahihi na mema, kufurahia mbingu, ushirika na jamii ya malaika, mawasiliano na upendo wa Mungu na Mwana Wake, kuinuliwa na kuongezwa kwa nguvu zetu zote katika zama za milele zote—Je, haya yote siyo vichocheo vikuu na vitia moyo vinavyotusukuma kutoa huduma ya upendo kutoka mioyoni mwetu, kwenda kwa Muumba na Mkombozi wetu? {SCsw 21.3}

Na, kwa upande mwingine, hukumu za Mungu zilizotamkwa dhidi ya dhambi, adhabu isiyoepukika, kushuka chini kwa maadili - tabia mbaya, na maangamizi ya mwisho, vimewasilishwa katika Neno la Mungu ili kutuonya dhidi ya kumtumikia Shetani. {SCsw 21.4}

Je, sisi tusiikubali rehema ya Mungu? Ni nini zaidi ambacho Yeye angeweza kufanya? Hebu tujiweke katika uhusiano ulio sahihi, na Yeye aliyetupenda kwa upendo wa ajabu. Hebu tuzitumie vyema njia na yale yote tuliyoandaliwa kwa ajili yetu, ili tupate kubadilishwa kufanana na mfano Wake, na kurejeshwa katika ushirika na malaika wahudumuo, katika mapatano na mawasiliano pamoja na Baba na Mwana. {SCsw 22.1}

## SURA YA 3 - TOBA

Je, mwanadamu anawezaje kuwa mwenye haki mbele za Mungu? Mwenye dhambi anawezaje kufanywa mwenye haki? Ni kupitia Kristo pekee ndipo tunaweza kuletwa katika upatanisho na Mungu, na utakatifu; lakini Je, tunawezaje kuja kwa Kristo? Wengi wanauliza swali lile lile lililoulizwa na ule umati katika siku ya Pentekoste, waliposadikishwa juu ya dhambi, walipiga kelele na kulia wakisema, “Je, tutendeje?” Neno la kwanza la mtume Petro

katika kujibu lilikuwa, "***Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe"*** **Matendo ya Mitume 3:19** **{SCsw 23.1}**

Toba inajumuisha kuisikitikia dhambi na kugeuka mbali nayo. Hatutaachana na dhambi isipokuwa tumeona ubaya wake; hakutakuwa na badiliko la kweli katika maisha yetu, mpaka tuachane nayo moyoni. **{SCsw 23.2}**

Kuna wengi ambao wanaoshindwa kuelewa asili ya kweli ya toba. Watu wengi huomboleza kwamba wamefanya dhambi na hata kufanya matengenezo ya nje kwa sababu wanaogopa kwamba kufanya kwao makosa, kutawaletea mateso wenyewe. Lakini hii sio toba, katika maana ya Biblia. Wanaomboleza mateso, badala ya dhambi. Esau alikuwa na kilio kama hicho, alipoona amepoteza haki yake ya uzaliwa wa kwanza milele. Balaam, alitishika, alipomwona malaika aliyesimama katika njia yake na upanga uliofutwa, alikiri hatia yake ili asije akapoteza uhai wake; lakini hakukuwa na toba ya dhati kwa dhambi, hakuwa na uongofu uliokusudiwa, wala kuchukia uovu. Yuda Iskariote, baada ya kumsaliti Bwana wake, alisema kwa sauti iliyosikika, "***Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia***". **Mathayo 27:3** **{SCsw 23.3}**

Ungamo hilo lililazimishwa kutoka katika nafsi yake yenye hatia kwa hisia mbaya ya kuhukumiwa na kutazamia hukumu kwa hofu. Matokeo ambayo yangempata, yalimfanya ajae hofu, lakini hapakuwa na huzuni ya kina, yenye kufanya moyo upondeke, katika nafsi yake kwamba alikuwa amemsaliti Mwana wa Mungu asiye na doa na kumkana Mtakatifu wa Israeli. Farao, alipokuwa akiteseka chini ya hukumu za Mungu, alikiri dhambi yake ili kuepuka adhabu zaidi, lakini akarudi kwenye upinzani na uasi wake dhidi ya Mbingu, mara tu mapigo yalipokoma. Hawa wote waliomboleza matokeo ya dhambi, lakini hawakuhuzunika kwa ajili

ya dhambi yenyewe. {SCsw 24.1}

Lakini moyo unapojitoa chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu, dhamiri itahuishwa, na mwenye dhambi hutambua kwa kiasi fulani kina na utakatifu wa sheria takatifu ya Mungu, ambayo ndiyo msingi wa himaya/serikali Yake mbinguni na duniani. "Nuru ya Kweli, inamtia nuru kila mtu akija katika ulimwengu," inaangazia vyumba vya siri vya roho, na mambo yaliyofichwa ya giza yanadhihirika. Yohana 1:9. Usadikisho unagusa akili na moyo. Mwenye dhambi hutambua haki ya Yehova na anahisi hofu ya kuonekana katika hatia na uchafu wake mwenyewe, mbele za Yeye achunguzaye mioyo. Anaona upendo wa Mungu, uzuri wa utakatifu, furaha ya usafi wa moyo na utakaso; anatamani kusafishwa na kurejeshwa kwenye ushirika na Mbingu. {SCsw 24.2}

Ombi la Daudi baada ya kuanguka kwake linaonyesha asili ya huzuni ya kweli, kwa ajili ya dhambi. Toba yake ilikuwa ya dhati na ya kina. Hakukuwa na juhudi za kupunguza hatia yake; hakutamani kuepuka hukumu iliyompa tishio wakati akitoa maombi yake. Daudi aliona ukubwa na uzito wa makosa yake; aliona uchafu wa roho yake; aliichukia dhambi yake. Haikuwa kwa ajili ya msamaha tu kwamba aliomba, bali kwa ajili ya usafi wa moyo. Alitamani furaha ya utakatifu—kurejeshwa katika mapatano na ushirika na Mungu. Haya ndiyo yalikuwa maneno ya roho yake: {SCsw 24.3}

***Heri aliyesamehewa dhambi, Na kusitiriwa makosa yake.***

***Heri Bwana asiyemhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila.*** Zaburi 32:1-2 {SCsw 25.1}

*Ee Mungu, unirehemu, Sawasawa na fadhili Zako.*

*Kiasi cha wingi wa rehema Zako, Uyafute makosa yangu.*

*Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu.*

*Maana nimejua mimi makosa yangu Na dhambi yangu i mbele yangu daima.*

*Nimekutenda dhambi Wewe peke Yako, Na kufanya maovu mbele za macho Yako. Wewe ujulikane kuwa una haki unenapo, Na kuwa safi utoapo hukumu.*

*Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; Mama yangu alinichukua mimba hatiani.*

*Tazama, wapendezwa na kweli iliyo moyoni; Nawe utanijulisha hekima kwa siri,*

*Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji*

*Unifanye kusikia furaha na shangwe, Mifupa uliyoiponda ifurahi.*

*Usitiri uso wako usitazame dhambi zangu; Uzifute hatia zangu zote.*

*Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu*

*Usinitenge na uso Wako, Wala Roho Wako mtakatifu usiniondolee.*

*Unirudishie furaha ya wokovu Wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi.*

*Nitawafundisha wakosaji njia zako, Na wenye dhambi watarejea kwako.*

*Ee MUNGU, Mungu wa wokovu wangu, Uniponye na damu za watu, Na ulimi wangu utaiimba haki Yako.* **Zaburi 51:1-14** **{SCsw 25.2}**

Toba kama hii, haiwezi kufikiwa kwa uwezo wetu wenyewe, bali inapatikana tu kutoka kwa Kristo, ambaye alipaa juu na kuwapa wanadamu vipawa. **{SCsw 25.2}**

Hapa ndipo kuna jambo ambalo wengi wanaweza kukosea, na hivyo wanashindwa kupokea msaada ambao Kristo anatamani

kuwapa. Wanafikiri kwamba hawawezi kuja kwa Kristo isipokuwa watubu kwanza, na kwamba toba ndiyo huandaa msamaha wa dhambi zao. Ni kweli kwamba toba hutangulia msamaha wa dhambi; kwani ni moyo uliovunjika na kupondeka pekee, ndio utakaohisi hitaji la Mwokozi. Lakini Je, mwenye dhambi anapaswa kusubiri hadi atubu kabla ya kuja kwa Yesu? Je, toba inapaswa kufanywa kizuizi kati ya mwenye dhambi na Mwokozi? **{SCsw 26.1}**

Biblia haifundishi kwamba mwenye dhambi lazima atubu kabla hajaitikia mwaliko wa Kristo, ***"Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha.*** **Mathayo 11:28.** Ni nguvu ya wema utokao kwa Kristo, ndiyo unatuoongoza kwenye toba ya Kweli. Petro alilifanya jambo hili kuwa wazi katika kauli yake kwa Waisraeli aliposema, "***Mtu Huyo Mungu amemtukuza kwa mkono Wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi.*** **Matendo ya Mitume 5:31**." Hatuwezi kutubu bila Roho ya Kristo kuamsha dhamiri kama ilivyo kwamba hatuwezi kusamehewa bila Kristo. **{SCsw 26.2}**

Kristo Ndiye chanzo cha kila hisia, msukumo na mtazamo sahihi. Yeye pekee Ndiye anayeweza kupanda chuki dhidi ya dhambi moyoni. Kila shauku ya Ukweli na usafi wa moyo, kila usadikisho wa dhambi zetu, ni ushahidi kwamba Roho Wake anafanya kazi ndani ya mioyo yetu. **{SCsw 26.3}**

Yesu alisema, ***"Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote Kwangu".*** **Yohana 12:32.** Kristo lazima afunuliwe kwa mwenye dhambi kama Mwokozi afaye kwa ajili ya dhambi za ulimwengu; na tunapomwona Mwana-Kondoo wa Mungu juu ya msalaba wa Kalvari, siri ya ukombozi huanza kufunuliwa akilini mwetu, na wema wa Mungu unatuongoza kwenye toba. Kwa kuwafia wenye dhambi, Kristo alionyesha upendo usioweza kueleweka kwa akili za kibinadamu; na mwenye dhambi anapouona upendo huu, unalainisha moyo, unagusa akili, na kuhamasisha majuto katika

roho. {SCsw 26.4}

Ni kweli kwamba wakati mwingine watu huona aibu kwa njia zao za dhambi, na kuacha baadhi ya tabia zao mbaya, kabla hawajajua kwamba wanavutwa kwa Kristo. Lakini wakati wowote wanapojitahidi kurekebisha mambo na kufanya matengenezo, kutokana na hamu ya dhati ya kufanya mema, ni nguvu ya Kristo tu, ndiyo inayowavuta. Ushawishi ambao hawautambui hutenda kazi ndani ya nafsi, na dhamiri huhuishwa, na maisha ya nje yanabadilishwa. Na Kristo anapowavuta watazame katika msalaba Wake, wanamtazama Yeye ambaye dhambi zao zimemchoma, amri ya Mungu huijia dhamiri yao. Uovu wa maisha yao, dhambi iliyozama ndani ya roho, hufunuliwa kwao. Wanaanza kuelewa kwa kiasi fulani kuhusu haki ya Kristo, na kupaza sauti kwa kusema, "Dhambi ni nini? Hata ihitaji dhabihu kama hii kwa ajili ya ukombozi wa mwenye dhambi aliyeathiriwa nayo? Je, upendo huu wote, mateso haya yote, udhalilishaji huu wote, ulihitajika kweli hii dhabihu kubwa, ili tusipotee, bali tuwe na uzima wa milele?" {SCsw 27.1}

Mwenye dhambi anaweza kuupinga upendo huu wa Mungu, anaweza kukataa kuvutwa kwa Kristo; lakini asipopinga atavutwa tu kwa Yesu; Maarifa ya mpango wa wokovu yatamwongoza mpaka chini ya msalaba katika toba kwa ajili ya dhambi zake, ambazo zimesababisha mateso ya Mwana mpendwa wa Mungu. {SCsw 27.2}

Akili ile ile ya Kiungu inayotenda kazi juu ya vitu vya asili ndiyo inayozungumza na mioyo ya wanadamu na kuumba ndani yao shauku kali isiyoweza kuelezeka kwa kitu ambacho hawana. Mambo ya dunia hayawezi kukidhi matamanio/hamu yao. Roho wa Mungu anawasihi watafute vitu pekee ambavyo ndivyo vinaweza kutoa amani na raha—neema ya Kristo, furaha ya utakatifu. Kupitia ushawishi unaoonekana na usioonekana, Mwokozi wetu daima anaendelea na kazi ya kuzivuta akili za

wanadamu kutoka kwenye anasa za dhambi zisizoridhisha moyo hadi kwenye baraka zisizo na kikomo ambazo zinaweza kuwa zao ndani Yake. Kwa roho hizi zote, zinazofanya kazi bure kutafuta kunywa kutoka kwenye mabirika yaliyopasuka na yavujayo ya ulimwengu huu, ujumbe wa Mungu unatolewa, "**Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure"**. **Ufunuo 22:17** {SCsw 28.1}

Ninyi ambao mioyoni mwenu mna matamanio makubwa ya kitu kilicho bora kuliko kile ambacho ulimwengu huu unaweza kutoa, tambueni kwamba tamaa hii ni sauti ya Mungu kwa nafsi zenu. Mwombeni Yeye awape toba ya kweli, na amfunue Kristo kwenu katika upendo Wake usio na kikomo, katika usafi Wake mkamilifu. Katika maisha ya Mwokozi, kanuni za sheria ya Mungu—upendo kwa Mungu na kwa mwanadamu—vilionyeshwa kikamilifu/ukamilifu-katika mtindo wa maisha. Wema, ukarimu na upendo usio na ubinafsi vilikuwa maisha ya nafsi Yake. Ni pale tu tunapomtazama Yeye, kama nuru kutoka kwa Mwokozi wetu inapotuangazia, ndipo tunaona uovu wa mioyo yetu wenyewe. {SCsw 28.2}

Huenda tukajigamba na kujidanganya wenyewe kama Nikodemo alivyofanya, kwamba maisha yetu yamenyooka au tu wakamilifu (Ayubu 1:1), kwamba tabia zetu za maadili ni sahihi, na kufikiri kwamba hatuhitaji kuinyenyekesha mioyo yetu mbele za Mungu, kama mwenye dhambi wa kawaida: lakini pale nuru kutoka kwa Kristo inapoangaza ndani ya roho zetu, tutaona jinsi tulivyo wachafu/najisi; tutatambua ubinafsi wa nia na kujipenda, uadui dhidi ya Mungu, ambao umechafua kila tendo la maisha. Ndipo tutajua kwamba haki yetu wenyewe kwa kweli ni kama matambara machafu tu, na kwamba damu ya Kristo pekee, ndiyo inaweza kutusafisha kutokana na unajisi/uchafu wa dhambi, na kuiumba mioyo yetu upya kwa mfano Wake Mwenyewe. {SCsw 28.3}

Mwale mmoja wa utukufu wa Mungu, mwangaza laini wa

usafi wa Kristo, unaopenya rohoni, hufanya kila doa la uchafu lionekane waziwazi, na kuweka wazi kasoro na madhaifu ya tabia ya mwanadamu. Huweka wazi tamaa zisizo na utakatifu, kukosa uaminifu kwa moyo na uchafu wa midomo. Matendo ya mwenye dhambi ya kutokuwa mwaminifu kwa kuitangua sheria ya Mungu, yanaonekana wazi machoni pake, na roho yake inaathiriwa na kuteswa chini ya ushawishi unaopeleleza, wa Roho wa Mungu. Mtu huyu anajichukia mwenyewe anapotazama tabia safi, isiyo na doa ya Kristo. **{SCsw 29.1}**

Wakati nabii Daniel alipoona utukufu uliomzunguka mjumbe wa mbinguni aliyekuwa ametumwa kwake, alilemewa na hisia ya udhaifu wake mwenyewe na kutokamilika kwake. Akielezea matokeo ya tukio hilo la ajabu, anasema, "***Basi nikaachwa peke yangu, nikaona maono haya makubwa, wala hazikubaki nguvu ndani yangu.***" **Danieli 10:8.** Nafsi iliyoguswa hivyo itachukia ubinafsi wake wa kujishugulikia maslahi yake na starehe zake tu, itachukia kujipenda nafsi yake tu, na itatafuta, kupitia haki ya Kristo, usafi wa moyo unaopatana na sheria ya Mungu na tabia ya Kristo. **{SCsw 29.2}**

Paulo anasema kwamba "***Kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia".*** **Wafilipi 3:6**; lakini tabia ya kiroho ya sheria ilipogunduliwa na kumfanyia kazi moyoni, alijiona kuwa ni mtu mwenye dhambi. Akihukumiwa kwa Andiko la sheria, kama watu wanavyoitumia katika maisha ya nje, alikuwa amejiepusha na dhambi; lakini alipoangalia ndani kwa kina cha maagizo Yake matakatifu, na kujiona kama Mungu alivyomwona, ndipo aliponyenyekea kwa aibu na kukiri hatia yake. Anasema, ***"Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria; ila ilipokuja ile amri, dhambi ilihuika, nami nikafa".*** **Warumi 7:9.** Alipoona asili ya kiroho ya sheria, dhambi ilionekana katika ubaya wake wa kutisha, na kujithathmini kwake kwa kujikuza na kujilinda mwenyewe kukatoweka. **{SCsw 29.3}**

Mungu hazichukulii dhambi zote kuwa zina ukubwa sawa; kuna viwango vya hatia katika makadirio Yake, na kanuni hii inamhusu mwanadamu vile vile; hivyo hata kama tendo hili au lile baya linaweza kuonekana dogo machoni pa wanadamu, hakuna dhambi iliyo ndogo machoni Pake Mungu. Hukumu ya mwanadamu ina upendeleo, ni nusu-nusu na sio kamilifu; lakini Mungu anakadiria vitu vyote kama vilivyo. Mlevi anadharauliwa na anaambiwa kwamba dhambi yake itamkosesha mbingu; huku kiburi, ubinafsi, na tamaa mara nyingi vinaachwa tu bila kukemewa. Lakini hizi ndizo dhambi ambazo zinamchukiza Mungu haswa; kwa vile zinapingana kabisa na wema wa tabia Yake, na upendo Wake huu usio na ubinafsi ambao ni mazingira halisi ya ulimwengu ambao haujaanguka. Yeye anayeanguka katika baadhi ya dhambi za kutisha zaidi, anaweza kuhisi aibu na umaskini wake na hitaji lake la neema ya Kristo; lakini kiburi huwa hakihisi haja au hitaji hilo, na ndivyo kinavyofunga moyo dhidi ya Kristo na baraka zisizo na kikomo, ambazo Yeye Alikuja kutoa. {SCsw 30.1}

Mtoza ushuru maskini aliyeomba, "***Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi***" Luka 18:13, alijiona kama mtu mwovu sana, na wengine walimtazama kwa njia hiyo hiyo; lakini mtu huyu alihisi hitaji lake, na akiwa na mzigo wake wa hatia na aibu alikuja mbele za Mungu, akiomba rehema Zake. Moyo wake ulikuwa wazi kwa Roho wa Mungu kufanya kazi Yake ya neema na kumweka huru kutokana na nguvu ya dhambi. Ombi la Farisayo la kujigamba na kujiona kuwa ndiyo mwenye haki, lilionyesha kwamba moyo wake ulikuwa umefungwa dhidi ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Kwa sababu ya umbali wake na Mungu, hakuhisi kabisa uchafu wake uliokithiri, tofauti kabisa na ukamilifu wa utakatifu wa Kiungu. Mfarisayo huyu, hakuhisi hitaji, na hivyo hakupokea chochote. {SCsw 30.2}

Ukiona maisha yako yenye dhambi, usingoje kujisaidia mwenyewe kuwa bora kwanza. Je, ni watu wangapi wanaofikiri

hawafai vya kutosha kuja kwa Kristo. Je, wewe unatarajia kuwa bora kupitia juhudi zako mwenyewe? "***Je! Mkushi aweza kuibadili ngozi yake, au chui madoa-doa yake? Kama aweza, ndipo na ninyi mwaweza kutenda mema, ninyi mliozoea kutenda mabaya.”*** **Yeremia 13:23.** Msaada wetu uko kwa Mungu peke yake. Hatupaswi kusubiri ili tusukumwe na vishawishi vyenye nguvu zaidi, fursa bora zaidi, au tabia au hulka takatifu zaidi. Hatuwezi kufanya chochote kwa uwezo wetu wenyewe. Ni lazima tumjie Kristo jinsi tulivyo. **{SCsw 31.1}**

Lakini hebu mtu yeyote na asijidanganye mwenyewe kwa wazo kwamba Mungu, katika upendo na rehema Zake nyingi, bado atawaokoa hata wale wanaokataa neema Yake. Uovu mkuu wa dhambi unaweza kutambuliwa tu katika nuru ya msalaba. Wanadamu wanaposisitiza kwamba Mungu ni mwema sana, kumtupilia mbali mwenye dhambi, hebu na watazame Kalvari. Ilikuwa ni kwa sababu hakukuwa na njia nyingine yoyote, ambayo mwanadamu angeweza kuokolewa, kwa sababu bila dhabihu hii haikuwezekana kabisa kwa mwanadamu kuepuka kutoka kwenye nguvu ya uchafu ya dhambi, na kurejeshwa kwenye ushirika na viumbe watakatifu -ambao walikuwa hawajafanya dhambi (malaika na sayari zingine), - haikuwezekana tena kwao wanadamu kushiriki maisha ya kiroho, - ilikuwa kwa sababu hii kwamba Kristo alijitwika juu Yake mwenyewe - hatia ya wanadamu wasiotii/waasi na kuteseka badala ya mwenye dhambi. Upendo na mateso na kifo cha Mwana wa Mungu vyote vinashuhudia ukubwa wa kutisha wa dhambi na kutangaza kwamba haiwezekani kuponyoka kutoka kwenye nguvu zake hiyo dhambi, hakuna tumaini la uzima wa juu zaidi au maisha ya juu zaidi, isipokuwa kupitia kujisalimisha kwa nafsi kwa Kristo-mwanadamu ajisalimishe kwa Kristo. **{SCsw 31.2}**

Watu wasiotubu wakati mwingine hujitolea udhuru kwa kuwarejelea wale wanaojiita Wakristo kwa mdomo tu, “mimi

mbona ni mwema tu kama wao. Wakrito hawa wa maigizo, Hawaiikani nafsi zao, hawajinyimi, sio watu wa kiasi, wala hawana uangalifu na hekima katika mwenendo wao kuliko mimi. Hakika watu hao wanapenda anasa na kujifurahisha kama mimi tu." Hivyo hufanya makosa ya wengine, kuwa kisingizio chao cha kupuuza wajibu wao. Lakini dhambi na kasoro za wengine hazimsamehi au kumpa mtu yeyote udhuru, kwa maana Bwana hajatupa mfano wa kianadamu unaokosea. Mwana wa Mungu asiye na doa, Ndiye pekee ametolewa kuwa mfano wetu, na wale wanaolalamika kuhusu mwenendo mbaya wa watu wanaojiita Wakristo, hawa ndio wanaopaswa kuonyesha mtindo wa maisha bora na mifano mizuri zaidi. Ikiwa wana wazo kubwa la kile ambacho Mkristo anapaswa kuwa, je, dhambi yao wenyewe sio kubwa zaidi? Kwa kuwa watu hawa wanajua lililo jema, lakini wanakataa kulifanya (Yakobo 4:17) Kujua na kuwa na kufanya uovu kwa makusudi, usijali kuhusu wanadamu feki au watu wa maigizo, wewe uwe nuru ili uwasaidie watu wanaohitaji kuona mifano mizuri wakiwemo wanafiki). **{SCsw 32.1}**

Jihadhari na kuahirisha-arisha mambo-(Kesho, Kesho!). Usiahirishe kazi ya kuzitelekeza dhambi zako na kutafuta usafi wa moyo kupitia Yesu. Hapa ndipo maelfu kwa maelfu ya watu wamekosea na kupoteza umilele. Sitazungumzia kuhusu ufupi wa maisha haya na kutokuwa na uhakika wa uhai-(dakika inayofuata); lakini kuna hatari kubwa, inayotisha—hatari isiyoeleweka vya kutosha—katika kuchelewa kukubali sauti ya Roho Mtakatifu wa Mungu inayosihi, katika kuchagua kuishi dhambini; kwa maana ni kweli kwamba uchelewesho huu ndio dhambi yenyewe. Dhambi, haijalishi kama inaweza kupimwa kwa akili yetu wanadamu kwamba ni ndogo, inaweza kuendekezwa na kufurahiwa na kuleta hatari ya kupoteza umilele. Kile ambacho hatutakishinda, hakika kitatushinda na kutuangamiza/kutumaliza. **{SCsw 32.2}**

Adamu na Hawa walijiaminisha wenyewe kwamba, katika

tendo moja dogo kama la kula tunda lililokatazwa, hawangeweza kusababisha matokeo ya kutisha kama ambavyo Mungu alikuwa ametangaza. Lakini jambo hili dogo lilikuwa uvunjaji wa sheria takatifu ya Mungu isiyobadilika, toka uumbaji, na ilimtenganisha mwanadamu na Mungu na kufungua malango ya mafuriko ya kifo, huzuni na ole isiyoelezeka juu ya ulimwengu wetu. Zama baada ya Zama vilio vimepanda juu kutoka kwenye sayari yetu, maombolezo yanayoendelea, na viumbe vyote vinaugua na kuomboleza pamoja kwa utungu mkali, kama matokeo ya uasi/kutotii kwa mwanadamu. Mbingu yenyewe imehisi athari za uasi wake mwanadamu, dhidi ya Mungu. Kalvari inasimama kama kumbukizi ya dhabihu ya ajabu inayohitajika ili kufidia uvunjaji wa sheria ya Mungu. Hebu tusichukulie dhambi kama kitu kidogo tu, kwamba ni mzaha na jambo lisilo na maana. **{SCsw 33.1}**

Kila tendo la uasi, kila kupuuza au kukataa neema ya Kristo, kunaleta jibu/mwitikio katika nafsi yako mwenyewe (react); na kuufanya moyo wako kuota sugu na kuwa mgumu, kuharibu na kupotosha nia, kufifisha na kupooza uelewa ili usihisi kitu, na sio tu hukufanya wewe usipende kujisalimisha kirahisi kwa Bwana, bali pia uwe na uwezekano mdogo sana wa kuisalimisha nia, wakati ombi nyororo la kusihi la Roho Mtakatifu wa Mungu, linatolewa moyoni mwako. **{SCsw 33.2}**

Wengi wanainyamazisha sauti ya dhamiri, inayowasumbua na kuyakoroga-koroga mawazo, kwa maoni kwamba wanaweza kubadilisha mwenendo wao wa uovu kirahisi tu pale wanapochagua; kwamba wanaweza kucheza-cheza na kuifanyia mzaha mialiko ya rehema, na bado wataguswa mioyo yao tena na tena na Roho wa Mungu. Wengi wanafikiri kwamba japokuwa wamemdharau Roho wa neema, baada ya kuweka ushawishi wao upande wa Shetani, katika wakati wa hali za kuogofya na kutisha zaidi (basi wao wanaweza kubadilisha kirahisi mwenendo wao wa dhambi). Lakini hili halifanyiki kwa urahisi. Uzoefu, elimu, ya

maisha yote, imeunda tabia kikamilifu, hivyo ni wachache tu hutamani kupokea sura ya Yesu. {SCsw 33.3}

Hata sifa moja mbaya ya tabia, tamaa moja ya dhambi, inayoendelea kuthaminiwa, kupendwa na kung'ang'aniwa, hatimaye itahafifisha makali yote ya injili- itapunguza matokeo chanya ya injili. Kila uendekezaji na kufurahia dhambi huimarisha na kuongeza uadui na chuki ya mtu kwa Mungu. Mtu anayeonyesha usugu wa kumkana-Mungu, au kutokujali Kweli za Mungu, anavuna tu mavuno ya kile alichopanda mwenyewe. Katika Biblia yote hakuna onyo la kutisha zaidi dhidi ya kufanya mizaha-mizaha na uovu kuliko maneno ya mtu mwenye busara, katika mithali za Sulemani, aliyesema kwamba mwenye dhambi "**atashikwa kwa kamba za dhambi zake**". **Mithali 5:22** {SCsw 34.1}

Kristo Yuko tayari kutuweka huru kutoka dhambini, ila Yeye halazimishi mapenzi yetu au nia zetu; na ikiwa tunaendelea kung'ang'ania kuasi, nia zetu wenyewe zitapindishwa kabisa kuelekea uovu, na hatutamani kuwekwa huru, ikiwa hatutakubali kupokea neema Yake, na Je, Bwana atafanya nini zaidi? Sisi tumejiangamiza wenyewe, kwa kuukataa upendo Wake. ***"Kwa maana Yeye asema, Wakati uliokubalika nalikusikia, Siku ya wokovu nalikusaidia; tazama, wakati uliokubalika ndiyo sasa; tazama siku ya wokovu ni sasa) Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, Leo, kama mtaisikia sauti Yake, Msifanye migumu mioyo yenu"*** **2Wakorintho 6:2, Waebrania 3:7-8** {SCsw 34.2}

**"**Wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo"**1 Samweli 16:7** "—Yeye huutamzama moyo wa mwanadamu, pamoja na hisia zake zinazokinzana za furaha na huzuni; moyo unaotangatanga, uliopotoka, ambao ni makao ya uchafu na udanganyifu mwingi. Yeye Anajua nia zake, na makusudi yake. Nenda Kwake, na roho yako ikiwa imechafuliwa kama ilivyo. Kama mwandishi wa-Zaburi, nawe fungua vyumba vyake kwa jicho linaloona yote, ukisema, "***Ee Mungu, unichunguze,***

***uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele.*" **Zaburi 139:23-24** **{SCsw 34.3}**

Wengi hukubali dini ya kiakili/akilini tu, aina ya utauwa, wakati moyo haujasafishwa. Hebu ombi lako liwe, **"*Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu*" Zaburi 51:10.** Shughulikia kiukweli nafsi yako. Kuwa makini, kuwa na uthabiti, kama ambavyo ungekuwa, endapo maisha yako ya kidunia yangekuwa hatarini. Hili ni jambo la kutatuliwa na kuwekwa sawa kati ya nafsi yako mwenyewe na Mungu, ndiyo, liwekwe sawa milele zote. Tumaini lililodhihirika tu, na sio chochote kingine, litathibitisha uharibifu wako. **{SCsw 35.1}**

Jifunze Neno la Mungu kwa maombi. Neno hilo linawasilisha mbele zako, sheria ya Mungu na maisha ya Kristo, kanuni kuu za utakatifu, ambazo bila hizo ***"Hakuna mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao;* Waebrania 12:14.** Linasadikisha dhambi; linafunua wazi njia ya wokovu. Lisikilize kama sauti ya Mungu ikizungumza na roho yako. **{SCsw 35.2}**

Unapoona uovu wa dhambi unavyotisha zaidi, na kushuhudia ukatili wake unavyokuwa mkubwa-kupindukia, pale utakapojiona jinsi ulivyo kiukweli hasa; wewe usikate tamaa na kuvunjika moyo. Ni watu wenye dhambi, ndio ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Sisi hatuna uwezo wa kujipatanisha na Mungu- sisi wanadamu, hatupaswi kufanya upatanisho na Mungu wenyewe )(kumpatanisha Mungu nasi, siyo jukumu lililo katika uwezo wetu) 1 Wak 5:19 - Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake, asiwahesabie makosa yao; Naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.), lakini—Jamani, jinsi upendo wa Mungu ulivyo wa ajabu!—Mungu katika Kristo, (ameifanya na anaendelea kuifanya kazi hii) "akiupatanisha ulimwengu na Nafsi Yake. 2 Wakorintho 5:19. Amekuwa akiibembeleza na kuisihi mioyo ya watoto Wake wenye hatia na makosa kwa upendo na huruma Yake nyororo.

Hakuna mzazi wa kidunia anayeweza kuwa mvumilivu kwa makosa, uovu na hatia ya watoto wake, kama vile Mungu alivyo kwa wale Anaowatafuta ili kuwaokoa. Hakuna mtu anayeweza kumsihi mkosaji kwa upole zaidi kama Mwenyezi Mungu. Hakuna midomo ya mwanadamu iliyowahi kumwaga maombi zaidi kwa mkosefu kuliko Yeye. Ahadi Zake zote, maonyo Yake, ni pumzi ya upendo usioelezeka. **{SCsw 35.3}**

Wakati Shetani anapokuja kwako kukuambia kwamba wewe ni mwenye dhambi mkuu, wewe mtazame tu Mkombozi wako na uzungumze kuhusu sifa/Stahiki Zake. Kile kitakachokusaidia ni kumtazama katika nuru Yake. Wewe ikiri dhambi yako, ila umwambie adui kwamba "***Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi***" na kwamba wewe unaweza kuokolewa kwa upendo Wake Bwana usio na kifani-mfanano. 1Timotheo 1:15. Yesu alimuuliza Simoni swali kuhusu wadeni wawili. Mmoja alikuwa na deni la Bwana wake kiasi kidogo, na mwingine alikuwa anadaiwa deni kubwa sana; lakini Bwana aliwasamehe wote wawili, na Kristo akamuuliza Simoni ni mdeni gani, ambaye angempenda Bwana wake zaidi. Simoni akajibu, "***yule ambaye alimsamehe nyingi-yule aliyesamehewa makosa mengi.***" **Luka 7:43**. Sisi tumekuwa wadhambi wakubwa, lakini Kristo alikufa, ili sisi tusamehewe. Sifa stahili za dhabihu Yake Kristo, ni tosha kwa sisi, kuwasilishwa kwa Baba kwa niaba yetu. Wale ambao Mwenyezi Mungu, Yeye Amewasamehe katika mengi zaidi hivyo, watampenda Yeye zaidi, na watasimama karibu kabisa na kiti Chake Chake cha enzi ili kumsifu kwa upendo Wake mkuu na dhabihu Yake isiyo na kifani. Ni pale tu tunapopata utambuzi wa upendo wa Mungu kwa kina zaidi, ndipo tunaona jinsi uovu wa dhambi ulivyo, katika uhalisia wake. Tunapoona urefu wa mnyororo ulioshushwa chini sana kwa ajili yetu, tunapofahamu kwa kiasi fulani kuhusu dhabihu isiyo na kikomo ambayo Kristo ametoa kwa niaba yetu, moyo wetu utayeyushwa kwa upole, ulaini,

upendo, na majuto. {SCsw 35.4}

## SURA YA 4 - UNGAMO

*"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; Bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema."* **Mithali 28:13**. {SCsw 37.1}

Masharti ya kupata rehema ya Mungu ni rahisi na ya haki na ya busara. Bwana hatuhitaji tufanye jambo gumu, la hatari au baya na lisilo la kawaida ili tupate msamaha wa dhambi. Hatuhitaji kufanya safari ndefu za hija na zenye kuchosha, au kufanya toba zenye uchungu, kuweka roho zetu kwa Mungu wa mbinguni au kufidia makosa yetu; lakini yeye aziungamaye dhambi, na kuziacha dhambi zake atahurumiwa. {SCsw 37.2}

Mtume anasema, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa*. **Yakobo 5:16**. Ungameni dhambi zenu kwa Mungu, ambaye pekee Ndiye anayeweza kuzisamehe, na makosa yenu ninyi kwa ninyi. Ikiwa umemkosea rafiki yako au jirani yako, unapaswa kukubali kosa lako, na ni wajibu wake kuwa huru kukusamehe. Kisha unapaswa kutafuta msamaha wa Mungu, kwa sababu ndugu uliyemjeruhi ni mali ya Mungu, na kwa kumdhuru ulimtenda dhambi Muumba na Mkombozi wake. Kesi hiyo inaletwa mbele ya Mpatanishi pekee wa kweli, Kuhani wetu Mkuu, ambaye *"alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi."* Naye ambaye "ameguswa na hisia za udhaifu wetu," na anaweza kusafisha kila doa la uovu. **Waebrania 4:15.** {SCsw 37.3}

Wale ambao hawajanyenyekesha roho zao mbele za Mungu katika kukiri hatia yao, bado hawajatimiza sharti la kwanza la kukubalika. Ikiwa hatujapitia toba isiyokuwa na kujuta, na

hatukujidhili roho zetu wala kuvunjika mioyo, tukichukia uovu wetu, hatujatafuta bado msamaha wa dhambi; na ikiwa hatujawahi kutafuta msamaha, hatujapata amani ya Mungu bado. Sababu pekee kwa nini hatuna msamaha wa dhambi zilizopita ni kwamba hatuko tayari kunyenyekesha mioyo yetu na kufuata masharti ya Neno la Kweli. Maelekezo ya wazi yanatolewa kuhusu jambo hili. Ungamo la dhambi, liwe la hadharani au la faraghani, linapaswa kuhisiwa kutoka moyoni na litolewe kwa hiari ya mtu. Mwenye dhambi hapaswi kushurutishwa kulitoa. Halipaswi kufanywa kwa njia ya juuju, kejeli na kutojali, kukosa adabu au kulazimishwa kutoka kwa wale ambao hawana ufahamu wa tabia inayochukiza ya dhambi. Kutubu kwa kumimina moyo, kutokea ndani kabisa, hupata njia ya kumfikia Mungu wa huruma isiyo na kikomo. Mtunga Zaburi anasema, "***Bwana Yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka roho, huwaokoa***. **Zaburi 34:18** **{SCsw 37.4}**

Ungamo la Kweli daima ni la tabia maalum, na hukiri dhambi fulani. Huenda likawa la asili ya kufikishwa mbele za Mungu pekee; linaweza kuwa makosa ambayo yanapaswa kukiriwa kwa watu binafsi ambao wameumizwa majeraha, kutokana nayo; au linaweza kuwa la hadharani, na hivyo linapaswa kukiriwa hadharani. Lakini maungamo yote yanapaswa kuwa dhahiri na bainishi kwa kipengele, yakikiri dhambi zile zile ambazo una hatia nazo. **{SCsw 38.1}**

Katika siku za Samweli, Waisraeli walimwacha Mungu. Walikuwa wakiteseka kutokana na matokeo ya dhambi zao; kwa sababu walikuwa wamepoteza imani yao kwa Mungu, wamepoteza utambuzi wao wa nguvu na hekima Yake Bwana ya kutawala taifa, wamepoteza ujasiri na imani yao katika uwezo Wake Mwenyezi Mungu wa kulinda, kuondoa hatia na kutetea sababu yake. Waligeuka kutoka kwa Mtawala mkuu wa ulimwengu

(mbingu na dunia) na kutamani kutawaliwa kama mataifa yaliyowazunguka. Kabla hawajapata amani walikiri hili dhahiri: "***tumeongeza dhambi zetu zote kwa uovu huu, wa kujitakia mfalme.*** **1 Samweli 12:19.** Dhambi ile ile ambayo walisadikishwa na kuhukumiwa nayo, ilibidi iungamwe. Moyo wao wa kutokuwa na shukrani ulizigandamiza roho zao na kuwatenga na Mungu. {SCsw 38.2}

Ungamo haliwezi kukubalika kwa Mungu bila toba ya dhati na matengenezo. Lazima kuwe na mabadiliko dhahiri yanayodhamiriwa kufanywa katika maisha ili kuachana na dhambi; kila kitu kinachomchukiza Mungu lazima kiondolewe. Haya yatakuwa ni matokeo ya huzuni ya dhati kwa dhambi. Kazi tunayopaswa kufanya kwa upande wetu imewekwa wazi mbele yetu: "***Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho Yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.*** **Isaya 1:16-17**. ***"Kama mtu mwovu akirudisha rehani, na kumrudishia mtu mali yake aliyomnyang'anya, akizifuata sheria za uzima, asitende uovu wowote; hakika ataishi, hatakufa."*** **Ezekieli 33:15.** Paulo anasema, akizungumzia kazi ya toba: ***"Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo."*** **2 Wakorintho 7:11** {SCsw 39.1}

Dhambi inapofisha utashi na mitazamo ya kimaadili, mkosaji hatambui kasoro za tabia yake wala kutambua jinsi uovu alioutenda unavyotisha; na pasipo kujisalimisha kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ambayo inamsadikisha, anabaki katika hali ya nusu-upofu kuhusiana na dhambi yake. Ungamo lake sio la kweli, bidii na dhati. Katika kila kukiri hatia yake, anaongezea kuomba

radhi kwa kutoa udhuru au visingizio vya mwenendo wake au dhambi yake, akitangaza kwamba kama isingekuwa kwa hali fulani, basi yeye hangefanya hiki au kile ambacho anakaripiwa. **{SCsw 40.1}**

Baada ya Adamu na Hawa kula tunda lililokatazwa, walijawa na hisia ya aibu na hofu. Mwanzoni wazo lao pekee lilikuwa jinsi ya kutoa udhuru au kisingizo kwa dhambi yao na hivyo kuepuka hukumu ya kutisha ya kifo. Bwana alipouliza kuhusu dhambi yao, Adamu alijibu swali, akiweka nusu ya hatia kwa Mungu na kwa mwenzi wake, yaani mkewe: "***Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Nyoka alinidanganya, nikala.*** **Mwanzo 3:12, 13.** Kwa nini ulimuumba nyoka? Kwa nini ulimwachia aje kwenye bustani ya Edeni? Haya ndiyo maswali yaliyokuwa kichwani mwake, na aliyomaanisha katika kutoa udhuru wake kwa dhambi yake, ndivyo walivyomshtaki Mungu, kwamba anawajibika kwa anguko lao. Roho ya kujihesabia haki ilianzia kwa baba wa uongo na imeonyeshwa na wana na binti wote wa Adamu. Kukiri kwa utaratibu huu hakuongozwi na Roho wa Mungu na hakutakubaliwa na Mungu. Toba ya kweli itamwongoza mtu kubeba hatia yake mwenyewe na kuikubali bila udanganyifu au unafiki. Kama mtoza ushuru maskini, ambaye ***hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi***. **Luka 18:13-** ndivyo wale wanaokiri hatia yao watahesabiwa haki, kwa kuwa Yesu atatetea kwa damu Yake kwa niaba ya hiyo roho iliyotubu. **{SCsw 40.2}**

Mifano katika Neno la Mungu ya toba ya kweli/dhati na unyenyekevu huonyesha roho ya ungamo ambayo hakuna udhuru wa dhambi au jaribio la kujihesabia haki litafanywa. Paulo hakujaribu kujikinga au kujificha; anapaka rangi nyeusi zaidi, dhambi yake wakati anaisimulia, na wala hajaribu kupunguza hatia yake. Anasema, "***niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu***

***ndani ya magereza, nikiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani; na walipouawa nalitoa idhini yangu. Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru; nikawaonea hasira kama mwenye wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini."*** **Matendo ya Mitume 26:10-11.** Hasiti kutangaza kwamba "***Kristo Yesu alikuja ulimwenguni ili awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.*** **1 Timotheo 1:15** **{SCsw 41.1}**

Moyo mnyenyekevu na uliovunjika, uliotiishwa na toba ya kweli, utathamini upendo wa Mungu na gharama ya Kalvari; na kama vile mwana anavyoungama kwa baba mwenye upendo, ndivyo mtu anayetubu kweli, atakavyoleta dhambi zake zote mbele za Mungu. Na imeandikwa, "***Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*** **1 Yohana 1:9** **{SCsw 41.2}**

## SURA YA 5 - KUJIWEKA WAKFU

Ahadi ya Mungu ni, "***Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote."*** **Yeremia 29:13** **{SCsw 43.1}**

Moyo wote lazima ujisalimishe kwa Mungu, la sivyo mabadiliko hayawezi kamwe kufanywa ndani yetu ambayo kwayo tutarejeshwa katika mfano Wake. Kwa asili tumetengwa na Mungu. Roho Mtakatifu anaelezea hali yetu kwa Maneno kama haya: ***"wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu" "Kichwa chote ni***

***kigonjwa", "moyo wote umezimia" "hamna uzima ndani yake" Tumebanwa kwa nguvu na mtego wa hila wa Shetani, Adui "amewafunga wanadamu wafanye kama apendavyo"*** **Waefeso 2:1, Isaya 1:5-6, 2 Timotheo 2:26** Mungu anatamani kutuponya, kutuweka huru. Lakini kwa kuwa hii inahitaji mabadiliko kamili, kufanywa upya kwa asili yetu yote, ni lazima sisi tujitoe kikamilifu Kwake. **{SCsw 43.2}**

Vita dhidi ya nafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa. Kujisalimisha nafsi, kuyasalimisha yote, kwa mapenzi ya Mungu, kunahitaji mapambano; lakini roho lazima ijisalimishe kwa Mungu kabla haijafanywa upya katika utakatifu. **{SCsw 43.3}**

Utawala wa Mungu, haujajengwa juu ya utii usio na busara, kujinyekekesha kwa Mungu kwa upofu, udhibiti usio na mantiki kama ambavyo Shetani anavyotaka uonekane kwa watu. Utawala wa Mungu, unavutia akili na dhamiri. **"Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana." Isaya 1:18**" Mungu halazimishi mapenzi ya viumbe Vyake. Yeye hawezi kukubali heshima ambayo haitolewi kwa hiari na kwa akili. Utii wa kulazimishwa tu ungezuia ukuaji wote halisi wa akili au tabia; ungemfanya mwanadamu kuwa mashine ya roboti tu. Hilo sio kusudi la Muumba. Yeye Anatamani kwamba mwanadamu, kazi kuu ya nguvu zake za uumbaji, afikie ukuaji wa juu zaidi. Bwana Anaweka mbele yetu kilele cha baraka ambacho Anataka kutuletea kupitia neema Yake. Bwana Anatualika tujitoe Kwake, ili Yeye afanye mapenzi Yake ndani yetu. Inabaki kwetu kuchagua kama tutawekwa huru kutoka katika utumwa wa dhambi, kushiriki uhuru mtukufu wa wana wa Mungu. **{SCsw 43.4}**

Katika kujitoa kwa Mungu, ni lazima tuache yote ambayo yatatutenganisha Naye. Kwa hivyo Mwokozi anasema, ***"Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi Wangu."*** **Luka 14:33**. Chochote kitakachovuta moyo kutoka kwa Mungu lazima kiachwe. Mali ni mungu/sanamu

ya wengi. Kupenda pesa, tamaa ya kuwa tajiri, ni mnyororo wa dhahabu unaowafunga watu kwa Shetani. Sifa na heshima ya kidunia huabudiwa na tabaka lingine. Maisha ya raha ya ubinafsi na uhuru kutoka kwa uwajibikaji ni sanamu ya wengine. Lakini vifungo hivi vya utumwa lazima vivunjwe. Hatuwezi kuwa nusu kwa Bwana na nusu kwa ulimwengu. Sisi sio watoto wa Mungu hadi pale tutakavyokuwa hivyo kikamilifu (na siyo nusu-nusu). {SCsw 44.1}

Kuna wale wanaodai kumtumikia Mungu, huku wakitegemea juhudi zao wenyewe kutii sheria Yake, kuunda tabia sahihi, na kupata wokovu. Mioyo yao haiguswi na hisia yoyote ya kina ya upendo wa Kristo, lakini wanatafuta kutekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo kama yale ambayo Mungu anawataka wafanye ili waipate mbingu. Dini kama hiyo haina thamani. Kristo anapoishi moyoni, roho itajazwa sana na upendo Wake, na furaha ya ushirika Naye, kiasi kwamba itashikamana Naye; na katika kumtafakari Yeye, umimi/nafsi itasahaulika. Upendo kwa Kristo utakuwa chemchemi ya matendo mema. Wale wanaohisi upendo unaowabidisha wa Mungu, hawaulizi ni kidogo kiasi gani wanaweza kutoa ili kukidhi mahitaji ya Mungu; hawaulizi kiwango cha chini kabisa, ili kuwa marafiki wa Mungu, bali wanalenga kufuata kikamilifu mapenzi ya Mkombozi wao. Kwa hamu kubwa wanatoa yote na kuonyesha nia sawa na thamani ya kitu wanachotafuta. Kumkiri Kristo kwa mdomo tu, bila upendo huu wa kina ni mazungumzo tu, utaratibu wenye ratiba kavu-kavu, na shuguli zinazoleta uchovu tu na kuboesha mtu. {SCsw 44.2}

Je, unahisi kwamba ni dhabihu kubwa sana kusalimisha yote kwa Kristo? Hebu jiulize swali, "Je, Kristo ametoa nini kwa ajili yangu?" Mwana wa Mungu alitoa yote—uhai na upendo na mateso—kwa ajili ya ukombozi wetu. Na je, inawezekana kwamba sisi, wale tusiostahili kabisa upendo Wake mkuu hivyo, tuibanie

mioyo yetu ili tusimpe Yeye? Kila wakati wa maisha yetu tumekuwa washirika wa baraka za neema Yake, na kwa sababu hii hasa hatuwezi kutambua kikamilifu kina cha ujinga na mateso ambayo tumeokolewa kwayo. Je, sisi tunaweza kweli kumtazama Yeye ambaye dhambi zetu zimemchoma, na bado tuwe tayari kudharau upendo na dhabihu Yake yote? Kwa kuzingatia kudhalishwa kusiko na kifani kwa Bwana wa utukufu, je, sisi tunung'unike tena, kwamba tutaweza kuingia katika uzima wa milele kupitia migogoro na kujidhalilisha tu? {SCsw 45.1}

Swali la wengi wenye kiburi ni, "Kwa nini ninahitaji kuingia katika toba, kujidhili na unyenyekevu kabla sijaweza kupata uhakika wa kukubalika kwangu na Mungu?" Ninakuelekeza kwa Kristo. Yeye Hakuwa na dhambi, na, zaidi ya haya, Alikuwa Mkuu wa mbinguni; lakini kwaajili yake mwanadamu, Yeye akawa Mdhambi/dhambi kwa ajili ya jamii ya mwanadamu. "***Akahesabiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua dhambi za watu wengi, Na kuwaombea wakosaji.***" **Isaya 53:12.** {SCsw 45.2}

Lakini Je, tunaacha nini, tunapotoa yote? Tunaacha moyo uliochafuliwa na dhambi- Tunamwachia Yesu moyo uliojaa dhambi, ili Yesu ausafishe, autakase kwa damu Yake Mwenyewe, na kutuokoa kwa upendo Wake usio na kifani. Na bado watu wanaona ni vigumu kuacha yote! Ninaona aibu kusikia hili likizungumziwa, ninaona aibu kuandika hili. {SCsw 46.1}

Mungu hatuhitaji tuache chochote, au tukate tamaa kwa lolote ambalo ni la maslahi yetu mema, au manufaa yetu kubaki nacho. Katika yote ambayo Yeye anafanya, macho Yake yanaangalia ustawi wa watoto Wake. Laiti wote ambao hawajamchagua Kristo wangetambua kwamba Yeye ana kitu bora kupindukia cha kuwapa, kuliko vile wanavyojitafutia wenyewe. Mwanadamu anafanya madhara makubwa na dhuluma kwa nafsi yake mwenyewe anapofikiri na kutenda kinyume na mapenzi ya

Mungu. Hakuna furaha ya kweli inayoweza kupatikana katika njia iliyokatazwa na Yeye anayejua kile kilicho bora na anayepanga mema ya viumbe Vyake. Njia ya uasi ni njia ya mateso na uharibifu. {SCsw 46.2}

Ni kosa kuendekeza wazo kwamba Mungu anafurahi kuona watoto Wake wakiteseka. Mbingu yote inapendezwa na furaha ya mwanadamu. Baba yetu wa mbinguni hafungi njia zinazoleta furaha kwa viumbe Vyake vyovyote. Masharti ya Mwenyezi Mungu yanatutaka tuepuke zile starehe ambazo zingeleta mateso na kukatishwa tamaa, ambazo zingetufungia mlango wa furaha na mbingu. Mkombozi wa ulimwengu anawakubali wanadamu jinsi walivyo, pamoja na matakwa yao yote, kutokamilika, na udhaifu; na hatasafisha tu dhambi na kutoa ukombozi kupitia damu Yake, lakini pia Atatosheleza hamu ya moyo ya wote wanaokubali kuvaa nira Wake, kubeba mzigo wake. Ni kusudi Lake kuwapa amani na raha wote wanaomwendea Yeye kwa ajili ya mkate wa uzima. Yeye Anatutaka tufanye tu kazi zile, ambazo zitaongoza hatua zetu hadi kwenye vilele vya furaha ambavyo wanadamu wasiotii hawawezi kamwe kuvifikia. Maisha ya furaha ya kweli ya roho ni kumfanya Kristo aumbike ndani yetu, tumaini la utukufu. {SCsw 46.3}

Wengi wanauliza, “Ninawezaje kujisalimisha kwa Mungu?” Unatamani kujisalimisha Kwake, lakini wewe ni dhaifu katika nguvu za kimaadili, katika utumwa wa shaka, na unadhibitiwa na tabia za maisha yako ya dhambi. Ahadi na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, mihemko yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Ujuzi wa ahadi zako zilizovunjwa na nadhiri zako ambazo hazikutimizwa zimepunguza kujiamini kwamba wewe ni mnyofu kweli au la!, na kukufanya uhisi kwamba Mungu hawezi kukubali; lakini huhitaji kukata tamaa. Unachohitaji kuelewa ni nguvu ya kweli ya mapenzi. Hii ni nguvu inayotawala katika asili ya mwanadamu, nguvu ya uamuzi, au ya

uchaguzi. Kila kitu kinategemea utendaji sahihi wa mapenzi/nia. Nguvu ya uchaguzi ambayo Mungu amewapa wanadamu; ni yao ili waitumie. Huwezi kubadilisha moyo wako, huwezi kwa nguvu zako mwenyewe kumpa Mungu mapenzi ya moyo wako; lakini unaweza kuchagua kumtumikia Yeye. Unaweza kumpa mapenzi yako; kisha Yeye atafanya kazi ndani yako kutaka na kufanya kulingana na mapenzi Yake mema. Hivyo asili yako yote italetwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo (mwili, akili na roho); mapenzi yako yatakita Kwake Yeye, mawazo yako yatakuwa katika maelewano Naye. **{SCsw 47.1}**

Matamanio ya wema na utakatifu yako sahihi kadiri yanavyoenda; lakini ukisimama hapa, hayatafaa chochote. Wengi watapotea huku wakitumaini na kutamani kuwa Wakristo. Hawafikii hatua ya kujisalimisha kwa Mungu. Hawachagui sasa kuwa Wakristo. **{SCsw 47.2}**

Kupitia utumiaji sahihi wa mapenzi, mabadiliko kamili yanaweza kufanywa katika maisha yako. Kwa kujisalimisha kwa Kristo, unajiunganisha na nguvu iliyo juu ya falme na mamlaka zote. Utakuwa na nguvu kutoka juu, ya kukushikilia imara, na hivyo kupitia kujisalimisha kwa Mungu kila mara utawezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya imani. **{SCsw 48.1}**

## SURA YA 6 - IMANI NA KUKUBALI

Kadri dhamiri yako ilivyohuishwa na Roho Mtakatifu, umekwishakuona kitu kuhusu uovu wa dhambi, nguvu zake, hatia yake, huzuni na uharibifu wake; na unaitazama kwa chuki. Unahisi kwamba dhambi imekutenganisha na Mungu, kwamba uko katika utumwa wa nguvu za uovu. Kadiri unavyojitahidi kuepuka, ndivyo unavyozidi kutambua kutokuwa na msaada kwako. Mawazo na nia yako ni chafu; moyo wako ni mchafu. Unaona kwamba maisha yako yamejawa, uchoyo, ubinafsi na dhambi. Unatamani kusamehewa, kusafishwa, na kuwekwa huru. Mapatano na Mungu, kufanana Naye—Je, unaweza kufanya nini ili kuyapata haya? {SCsw 49.1}

Ni amani unayohitaji—msamaha wa Mbinguni na amani na upendo katika nafsi. Pesa haziwezi kuinunua, akili haiwezi kuipata, hekima haiwezi kuipata; huwezi kamwe kutumaini, kwa juhudi zako mwenyewe, uipate. Lakini Mungu anakupa kama zawadi, "**bila fedha na bila bei/gharama." Isaya 55:1**. Ni yako ikiwa utanyoosha mkono wako na kuishika. Bwana anasema, "***Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.*** **Isaya 1:18** ***"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, Nami nitatia roho mpya***

***ndani yenu, Nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, Nami nitawapa moyo wa nyama."*** **Ezekieli 36:26** {SCsw 49.2}

Umeungama dhambi zako, na kuziweka mbali na moyo wako. Umeazimia kujitoa kwa Mungu. Sasa nenda Kwake, na umwombe kwamba Aoshe dhambi zako na kukupa moyo mpya. Kisha amini kwamba Yeye anafanya hivi kwa sababu Yeye Ameahidi. Hili ndilo somo ambalo Yesu alifundisha alipokuwa duniani, kwamba zawadi ambayo Mungu ametuahidi, lazima tuamini nasi, kwamba tumeipokea, na ni yetu. Yesu aliwaponya watu magonjwa yao walipokuwa na imani katika nguvu Zake; hivyo Aliwasaidia katika mambo ambayo wangeweza kuona, Naye akawatia moyo kuweka imani Kwake kuhusu mambo ambayo hawangeweza kuona—kuwaongoza kuamini katika uwezo Wake wa kusamehe dhambi. Hii Alisema waziwazi katika uponyaji wa mtu aliyepooza: "***Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (akwamwambia yule mwenye kupooza) Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako."*** **Mathayo 9:6.** Vivyo hivyo pia Yohana mwinjilisti anasema, akizungumzia miujiza ya Kristo, "***Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu Ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa Jina Lake."*** **Yohana 20:31** {SCsw 49.3}

Kutokana na maelezo rahisi ya Biblia ya jinsi Yesu alivyowaponya wagonjwa, tunaweza kujifunza kitu kuhusu jinsi ya kumwamini Yeye kwa msamaha wa dhambi. Hebu tugeukie kisa cha mtu aliyepooza huko Bethsaida. Mtesekaji masikini, hakuwa na msaada; hakuwa ametumia mikono na miguu yake- viungo- kwa miaka thelathini na minane. Lakini Yesu alimwambia, "***Ondoka, ujitwike kitanda chako uende***." Huenda mgonjwa angeweza kusema, "Bwana, ukitaka kunifanya niwe mzima, nitatii Neno Lako." Lakini, hapana, aliamini Neno la Kristo, akaamini

kwamba alikuwa mzima, na akajitahidi kuondoka mara moja; alitaka kutembea, na akatembea. Alitenda kulingana na Neno la Kristo, na Mungu akampa nguvu. Akawa mzima. {SCsw 50.1}

Vivyo hivyo wewe ni mwenye dhambi. Huwezi kulipia dhambi zako za zamani; huwezi kubadilisha moyo wako na kujifanya mtakatifu mwenyewe. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia Kristo. Wewe unaamini ahadi hiyo. Unakiri dhambi zako na kujitoa kwa Mungu. Nia yako ya kutaka kumtumikia. Kwa hakika unavyoendelea kufanya hivi, Mungu atatimiza Neno Lake kwako. Ukiamini ahadi hiyo,—amini kwamba umesamehewa na kusafishwa,—Mungu hufanya hili liwe uhalisia; umeponywa, umefanywa kuwa kamili, kama vile Kristo—alivyompa mtu aliyepooza nguvu ya kutembea wakati mtu huyo alipoamini kwamba amepona. Itakuwa hivyo kwako, ikiwa utaamini. {SCsw 51.1}

Usingoje kuhisi kwamba umepona, lakini sema, "Ninaamini; ni hivyo, si kwa sababu ninahisi, bali kwa sababu Mungu ameahidi." {SCsw 51.2}

Yesu anasema, "***Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu."*** **Marko 11:24**. Kuna sharti katika ahadi hii—kwamba tuombe kulingana na mapenzi ya Mungu. Lakini ni mapenzi ya Mungu kutusafisha sisi kutoka kwa dhambi, kutufanya sisi watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Kwa hivyo tunaweza kuomba baraka hizi, na kuamini kwamba tunazipokea, na kumshukuru Mungu kwamba tumezipokea. Ni upendeleo wetu kwenda kwa Yesu na kutakaswa, na kusimama mbele ya sheria bila kuumbuka au majuto. "***Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.*** **Warumi 8:1** {SCsw 51.3}

Tangu sasa ninyi sio mali yenu wenyewe; mmenunuliwa kwa

gharama/bei. ***"Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya Mwana-Kondoo asiye na ila, asiye na waa"*** **1 Petro 1:18-19** Ni kupitia tendo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amewezesha uzima mpya uzaliwe moyoni mwako. Wewe ni kama mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, Naye anakupenda kama ampendavyo Mwanawe. **{SCsw 51.4}**

Sasa kwa kuwa umejitoa kwa Yesu, usitembee mbali Naye, usijiondoe Kwake, lakini siku baada ya siku sema, "Mimi ni wa Kristo; Nimejitoa Kwake;" na umwombe Bwana akupe Roho Wake na akulinde kwa neema Yake. Kwa vile, ni kwa kujitoa kwa Mungu, na kumwamini Yeye, ndiyo unakuwa mtoto Wake, ndivyo utakavyoishi ndani Yake. Mtume anasema, "***Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye;*** **Wakolosai 2:6**" **{SCsw 52.1}**

Wengine wanaonekana kuhisi kwamba lazima wawe kwenye majaribio, na lazima wathibitishe kwa Bwana kwamba wamebadilishwa (wamekuwa na matengenezo ya tabia), kabla hawajaweza kudai baraka Zake Bwana. Lakini wanaweza kudai baraka za Mungu hata sasa. Lazima wawe na neema Yake, Roho wa Kristo, ili kuwasaidia katika udhaifu wao, la sivyo hawawezi kuuzuia au kuupinga uovu. Yesu anapenda tuje Kwake kama tulivyo, wenye dhambi, wasiojiweza, na tegemezi. Tunaweza kuja na udhaifu wetu wote, upumbavu wetu, dhambi zetu, na kuanguka miguuni Pake kwa toba. Ni utukufu Wake Bwana, kutuzunguka sisi katika mikono ya upendo Wake na kufunga majeraha yetu, kutusafisha na unajisi/uchafu wote. **{SCsw 52.2}**

Hapa ndipo maelfu wanaposhindwa; hawaamini kwamba Yesu huwasamehe wao binafsi, mtu mmoja mmoja. Hawamchukulii Mungu kama asemavyo-kwa Neno Lake. Ni fursa ya wote wanaofuata masharti kujua wenyewe kwamba msamaha

hutolewa kwa ukarimu/uhuru mwingi, kwa kila dhambi. Ondoa kushuku/shaka kwamba ahadi za Mungu hazikukusudiwa kwako. Ahadi Zake ni kwaajili ya kila mkosaji anayetubu. Nguvu na neema vimetolewa kupitia Kristo ili viletwe na malaika wanaohudumu kwa kila roho inayoamini. Hakuna aliye na dhambi kiasi kwamba hawezi kupata nguvu, usafi wa moyo, na haki katika Yesu, aliyekufa kwa ajili yao. Yeye Anasubiri kuwavua nguo zao zilizotiwa madoa na kuchafuliwa na dhambi, na kuwavalisha mavazi meupe ya haki; Yeye Anawaalika waishi na wasife. {SCsw 52.3}

Mungu hatushughulikii kama wanadamu wenye ukomo wanavyotendeana. Mawazo Yake ni mawazo ya rehema, upendo mwanana, kujali na huruma nyororo. Anasema, ***Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa. Nimeyafuta makosa yako kama wingu zito, na dhambi zako kama wingu; Isaya 55:7, Isaya 44:22*** {SCsw 53.1}

"***Maana Mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana MUNGU; basi ghairini, mkaishi. Ezekieli 18:32.*** Shetani yuko tayari kuiba ahadi za Mungu zilizobarikiwa na kutokomea kisiri, kimya-kimya. Anatamani kuchukua kila miale ya nuru ya tumaini na kila mwanga wa nuru kutoka rohoni; lakini wewe usimruhusu afanye hivi. Usimsikilize mjaribu, bali sema, "Yesu amekufa ili nipate kuishi. Yeye Ananipenda, na Yeye hapendi kwamba niangamie. Nina Baba wa mbinguni Mwenye huruma; na ingawa nimeutumia vibaya upendo Wake, ingawa baraka alizonipa zimefanyiwa ubaradhifu, ***nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana Wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi Wako. Luka 15:18-20-*** Mfano huo unakuambia jinsi mwana mpotevu atakavyopokelewa: "***Alipokuwa angali mbali,***

***baba yake alimwona, akamhurumia, akakimbia, akamwangukia shingoni, akambusu.*"  {SCsw 53.2}

Lakini hata mfano huu, unaoonyesha huruma, mapenzi na kugusa moyo, inashindwa kuelezea huruma isiyo na kipimo ya Baba wa mbinguni.  Bwana anatangaza kupitia nabii Wake, "***Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili Zangu"*** **Yeremia 31:3**

Wakati mwenye dhambi bado yuko mbali na nyumba ya Baba, akifanyia ubaradhifu mali yake katika nchi ya kigeni, moyo wa Baba una matamanio naye sana; na kila hamu inayoamshwa rohoni kumrudia Mungu ni ombi la kusihi la upole la Roho Wake, akimbembeleza, akimsihi, na kumvuta mwana mpotevu kwenye moyo wa upendo wa Baba yake. **{SCsw 54.1}** Ukiwa na ahadi hizi nyingi za Biblia mbele yako, je, unaweza kweli kutoa nafasi ya shaka? Je, unaweza kuamini kwamba wakati mwenye dhambi maskini anapotamani kurudi, anapotamani kuziacha dhambi zake, Bwana atakuwa anamzuia vikali ili asije akasimama miguuni Pake kwa toba? Achana na mawazo kama hayo! Hakuna kitu kinachoweza kuumiza roho yako kama kuendekeza wazo kama hilo kuhusu Baba yetu wa mbinguni. Yeye Anachukia dhambi, lakini anampenda mwenye dhambi, Naye Alijitoa katika nafsi ya Kristo, ili wote wanaotaka kuokolewa na kupata baraka za milele katika ufalme wa utukufu. Je, ni lugha gani yenye nguvu, yenye upendo mwanana, kujali, na huruma nyororo zaidi, ambayo ingeweza kutumika kuliko ile Yeye ambayo amechagua kuonyesha upendo Wake kwetu? Bwana Anatangaza, ***"Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini Mimi sitakusahau wewe."*** **Isaya 49:15{SCsw 54.2}**

Inueni macho, ninyi mnaoona shaka na kutetemeka; Kwa maana Yesu Yu hai kufanya maombezi kwa ajili yetu. Mshukuru Mungu kwa zawadi ya Mwanawe mpendwa na omba kwamba kifo

chake, kisiwe cha bure kwako. Roho anakualika leo. Njoo kwa moyo wako wote kwa Yesu, nawe unaweza kudai baraka Zake. {SCsw 54.3}

Unaposoma ahadi, kumbuka hizi ni kielelezo cha upendo usio na kifani, usioweza kutamkika na sikitiko. Moyo mkuu wa upendo usio na kikomo wa Bwana, unavutwa kwa mwenye dhambi kwa huruma isiyo na kikomo. "***Katika Yeye huyo, kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi,*** **Waefeso 1:7** Ndiyo, amini tu kwamba Mungu Ndiye msaidizi wako. Yeye Anataka kurejesha sura Yake ya maadili ndani ya mwanadamu. Unapomkaribia kwa maungamo na toba, Yeye atakukaribia kwa rehema na msamaha. {SCsw 55.1}

## SURA YA 7 – KIPIMO CHA UANAFUNZI

***"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.*** **2 Wakorintho 5:17** {SCsw 57.1}

Huenda mtu asiweze kueleza wakati au mahali bainishi, au kufuatilia mfululizo/mnyonyoro wa matukio yote katika mchakato wa uongofu; Lakini hii haithibitishi kuwa hajaongoka. Kristo alimwambia Nikodemo, ***"Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.*** **Yohana 3:8.** Kama ilivyo kwa upepo, ambao hauonekani, lakini athari zake zinaonekana na

kuhisiwa wazi, ndivyo Roho wa Mungu anavyofanya kazi moyoni mwa mwanadamu. Nguvu hiyo ya kuzaliwa upya, ambayo hakuna jicho la mwanadamu linaweza kuona, huzaa maisha mapya katika nafsi; Inaumba kiumbe kipya kwa mfano wa Mungu. Ingawa kazi ya Roho iko kimya na haionekani kwa macho au huonekana kwa taratibu sana, athari zake hudhihirika. Ikiwa moyo umefanywa upya na Roho wa Mungu, maisha yatashuhudia Ukweli huo. Ingawa hatuwezi kufanya lolote kubadilisha mioyo yetu au kujileta katika mapatano na Mungu; Ingawa hatupaswi kujiamini sisi wenyewe hata kidogo au kwa matendo yetu mema, maisha yetu yatafichua ikiwa neema ya Mungu inakaa ndani yetu. Mabadiliko yataonekana katika tabia, mazoea, matamanio na zile ndoto tunazozikimbiza. Tofauti itakuwa wazi na kuamuliwa kati ya kile ambacho wamekuwa na kile walicho sasa. Tabia hufichuliwa, si kwa matendo mema machache ya hapa na pale na matendo mabaya ya hapa na pale, bali kwa mwelekeo wa maneno ambayo tuna mazoea kuyatamka, na matendo. **{SCsw 57.2}**

Ni kweli kwamba kunaweza kuwa na usahihi wa nje wa mwenendo bila nguvu ya kufanywa upya na Kristo. Kupenda kuwa na ushawishi na kutamani kuheshimiwa na wengine kwaweza kuzalisha maisha yaliyopangwa vizuri. Kujiheshimu wenyewe kunaweza kusababisha kuepuka mwonekano wa uovu. Moyo wa ubinafsi unaweza kufanya vitendo vya ukarimu. Je, basi, ni kwa njia gani tunaweza kujua tuko upande wa nani? **{SCsw 58.1}**

Nani anao moyo wako? Mawazo yetu yapo na nani? Je, sisi tunapenda kuzungumza juu ya nani? Ni nani aliye na mapenzi yetu yenye joto-joto na nguvu zetu bora? Ikiwa sisi ni wa Kristo, mawazo yetu yako pamoja Naye, na mawazo yetu matamu yatakuwa kuhusu Yeye. Yote tuliyo nayo na tulivyo vimewekwa wakfu Kwake. Tunatamani kubeba sura Yake, kupumua roho Yake, kufanya mapenzi Yake, na kumpendeza katika mambo yote. **{SCsw 58.2}**

Wale watakaokuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu watazaa matunda ya Roho, ***“upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.”*** **Wagalatia 5:22,2** Hawataenenda tena kulingana na tamaa mbaya za mwili za zamani, bali kwa imani ya Mwana wa Mungu watafuata hatua Zake, wataonyesha tabia Yake, na kujitakasa kama Yeye alivyo mtakatifu. Mambo ambayo hapo awali walichukia, sasa wanayapenda, na mambo ambayo hapo awali waliyapenda, wanayachukia sasa. Wenye kiburi na wenye ujasiri juu yao wenyewe na kulazimisha mambo yao, wanakuwa wapole na wanyenyekevu wa moyo. Wale waliokuwa madikteta, na batili kwa kujivuna, na kujidanganya wenyewe, sasa wanakuwa watu waangalifu na wasiojionyesha. Walevi wanakuwa na kiasi kwa kuachana na pombe, na wachafu wa moyo, wasafi. Desturi za ulimwengu zinawekwa kando. Wakristo hawatatafuti “kujipamba kwa nje,” bali “***bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.”*** **1 Petro 3:3-4** **{SCsw 58.3}**

Hakuna ushahidi wa toba ya kweli isipokuwa inafanya kazi ya matengenezo-kubadilisha maisha. Ikiwa mtu atatimiza kiapo chake, atarudisha kile ambacho alikuwa ameiba, na kuungama dhambi zake, na kumpenda Mungu na wanadamu wenzake, basi mwenye dhambi anaweza kuwa na uhakika kwamba amepita kutoka kifo hadi uzima. **{SCsw 59.1}**

Wakati, sisi kama viumbe wapotovu, na wenye dhambi, tunapokuja kwa Kristo na kuwa washiriki wa neema Yake yenye kutupa msamaha, upendo huchipuka moyoni. Kila mzigo ni mwepesi, kwa maana nira ambayo Kristo hutuwekea ni laini. Wajibu unakuwa furaha, na kujitoa dhabihu, raha. Njia ambayo hapo awali ilionekana kufunikwa na giza, inang'aa kwa miale kutoka kwa Jua la haki. **{SCsw 59.2}**

Uzuri wa tabia ya Kristo utaonekana katika wafuasi Wake. Ilikuwa ni furaha Yake kuyafanya mapenzi ya Mungu. Kumpenda Mungu, kwa ari na bidii kwa ajili ya utukufu Wake, vilikuwa ndiyo nguvu iliyotawala katika maisha ya Mwokozi wetu. Upendo ulipamba, na kuboresha, na kuimarisha matendo Yake yote. Upendo ni wa Mungu. Moyo usiowekwa wakfu hauwezi kuuanzisha au kuuzalisha upendo wa namna hi. Unapatikana tu katika moyo ambao Yesu anatawala. "***Sisi twapenda kwa maana Yeye alitupenda sisi kwanza.*** **1 Yohana 4:19** Katika moyo uliofanywa upya na neema ya Mwenyezi Mungu, upendo ndio kanuni ya utendaji. Unabadilisha tabia, unatawala misukumo, unadhibiti tamaa mbaya na nzuri, unashinda chuki, na unajenga upendo. Upendo huu, unaothaminiwa ndani ya roho, unazidisha utamu na furaha ya maisha na unatoa ushawishi unaosafisha na kuleta matokeo mazuri kwa wale walio karibu. **{SCsw 59.3}**

Kuna makosa mawili ambayo yapo dhidi ya watoto wa Mungu—hasa wale ambao ndiyo tu wameanza kuitegemea neema Yake, yaani wameanza tu kumwamini Yeye, na Neema awapayo—hawa wanapaswa kuwa waangalifu-wawe na tahadhari. La kwanza, ambalo limekwisha kuzungumziwa tayari, ni kule kutegemea matendo yao wenyewe, kujiamini kwa chochote kile ambacho wanaweza kufanya, ili kujileta wenyewe kwenye mapatano kati yao na Mungu. Yeye anayejaribu kuwa mtakatifu kwa matendo yake mwenyewe katika kutunza sheria, anajaribu kufanya jambo lisilowezekana kabisa. Chochote kile ambacho mwanadamu anaweza kukifanya bila Kristo kimechafuliwa na maambukizo ya ubinafsi na dhambi. Ni neema ya Kristo pekee yake, kupitia imani, ndiyo inayoweza kutufanya kuwa watakatifu. **{SCsw 59.4}**

Kosa jingine, ambalo liko upande mwingine kabisa, nalo lina hatari inayofanana na kosa la kwanza, ni kwamba imani katika Kristo inawaachilia watu kutoka katika kutunza sheria ya Mungu-inawaacha watu huru, wasitunze sheria; kwamba kwa sababu ni

kwa imani pekee, sisi tunakuwa washiriki wa neema ya Kristo, na hivyo matendo yetu hayahusiani kabisa na ukombozi wetu. {SCsw 60.1}

Lakini weka umakini hapa, kwamba utii sio ushikaji au utekelezaji tu wa sheria kwa nje, bali ni huduma ya upendo. Sheria ya Mungu ni onyesho na ishara ya asili Yake Mwenyewe; ni sehemu iliyo ndani ya kanuni kuu ya upendo, na hivyo ndio msingi wa utawala Wake mbinguni na duniani. Ikiwa mioyo yetu inafanywa upya kwa mfano wa Mungu, ikiwa upendo wa Mwenyezi Mungu umepandikizwa/umewekwa ndani ya nafsi, je, sheria ya Mungu haitatekelezwa katika maisha yetu? Wakati kanuni ya upendo inapoandikwa moyoni mwetu, wakati mwanadamu anapofanywa upya kulingana na mfano wa Yeye aliyemwumba, ahadi ya Agano Jipya hutimizwa, ***"Nitatia sheria Zangu mioyoni mwao, Na katika nia zao nitaziandika" Waebrania 10:16.*** Na ikiwa sheria imeandikwa moyoni, je, haitaumba na kuyabadilisha maisha? Utii—huduma na uaminifu wa upendo—ndiyo ishara halisi ya ufuasi. Hivyo, Maandiko yasema, "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake; ***Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake."1 Yohana 5:3, 2:4*** Badala ya kumwachia mwanadamu awe huru kutoka kwa utii, ni imani, na imani pekee, ndiyo inayotufanya kuwa washirika wa neema ya Kristo, ambayo inatufanya kuwa na uwezo wa kutoa utii. {SCsw 60.2}

Hatuununui wokovu wetu, kwa utii; kwa kuwa wokovu ni kipawa cha bure cha Mungu, kinachopokelewa kwa imani. Lakini utii ni tunda la imani. ***"Nanyi mnajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani Yake. Kila akaaye ndani Yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona Yeye, wala hakumtambua.*** **1 Yohana 3:5-6.** Hapa ndiko kipo kipimo halisi (mtihani). Ikiwa tutaishi ndani ya Kristo, ikiwa upendo wa Mungu utaishi ndani yetu, hisia zetu, mawazo yetu, malengo

yetu, matendo yetu, vitakuwa katika maelewano na mapenzi ya Mungu kama ilivyoonyeshwa katika maagizo ya sheria Yake takatifu. "***Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama Yeye alivyo na haki;*** **1 Yohana 3:7** Haki inafafanuliwa na kipimo cha sheria takatifu ya Mungu, kama ilivyoonyeshwa katika amri kumi zilizotolewa Sinai -Kutoka 20. {SCsw 61.1}

Hiyo inayoitwa imani kama inavyojulikana kuwa ndiyo imani katika Kristo ambayo inadai kuwaachilia watu kutoka kwa wajibu wa utii kwa Mungu, sio imani bali ni ujuvi (presumption-dhana ya udanganyifu). ***"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.*** **Waefeso 2:8, Yakobo 2:17** Yesu alisema kuhusu Yeye Mwenyewe kabla hajaja duniani, ***"Kuyafanya mapenzi Yako, Ee Mungu Wangu, ndiyo furaha Yangu; Naam, sheria Yako imo moyoni Mwangu.*** **Zaburi 40:8** Na kabla hajaondoka tena kwenda mbinguni alitangaza, ***"kama vile Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake.*** **Yohana 15:10** Maandiko yasema, ***"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa tunashika amri Zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani Yake. Lakini Yeye alishikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani Yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani Yake, imempasa kuenenda Mwenyewe vile vile kama Yeye alivyoenenda.*** **1 Yohana 2:3-6.** ***"Maana Kristo Naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake.*** **1 Petro 2:21"** {SCsw 61.2}

Sharti la uzima wa milele sasa, ni kama ilivyokuwa kila wakati kabla—kama ilivyokuwa Paradiso kabla ya anguko la wazazi wetu wa kwanza—utiifu kamili kwa sheria ya Mungu, haki kamili. Ikiwa uzima wa milele ungekubaliwa kwa sharti lolote pungufu ya hili, basi furaha ya ulimwengu mzima ingekuwa hatarini. Njia

ingewekwa wazi  kwa dhambi, pamoja na mateso na huzuni yake, kudumu milele. {SCsw 62.1}

Ilikuwa inawezekana kwa Adamu, kabla ya anguko, kuunda tabia ya uadilifu [haki] kwa kutii sheria ya Mungu. Lakini alishindwa kufanya hivyo, na kwa sababu ya dhambi yake, asili zetu zimeanguka na hatuwezi kujifanya kuwa wenye haki wenyewe. Kwa kuwa sisi ni wenye dhambi, viumbe wasio watakatifu, hatuwezi kutii sheria takatifu kikamilifu. Sisi wanadamu hatuna haki yetu wenyewe ambayo tunaweza kukutana na madai ya sheria ya Mungu. Lakini Kristo ametengeneza njia ya kutoroka, kwaajili yetu. Yeye Aliishi duniani katikati ya majaribu na mitihani kama ile ambayo tunakutana nayo. Yeye Aliishi maisha yasiyo na dhambi. Alikufa kwa ajili yetu, na sasa  Anatupa ofa ya kuchukua dhambi zetu na kutupa haki Yake. Ikiwa wewe utajitoa mwenyewe Kwake, na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako, basi, haijalishi maisha yako yametota dhambini kwa kiasi gani, kwa ajili Yake Yeye, wewe unahesabiwa kuwa mwenye haki. Tabia ya Kristo inasimama mahali pa tabia yako, na unakubalika mbele za Mungu kama vile hukuwahi kutenda dhambi. {SCsw 62.2} 2**2. Mbadilishano mkuu-Great exchange- Wakorintho 5:21**

Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.

Zaidi ya hii, Kristo hubadilisha moyo. Yeye Anakaa katika moyo wako kwa imani. Wewe unapaswa kudumisha muunganiko/uhusiano huu na Kristo kwa imani na kuendelea kuyasalimisha mapenzi yako Kwake daima; na usipoacha kufanya hivi, Yeye atafanya kazi ndani yako kutaka na kutenda kulingana na mapenzi Yake. Hivyo unaweza kusema, ***"na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu.*** **Wagalatia 2:20.** Hivyo Yesu alisema kwa wanafunzi Wake, ***"Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.***

**Mathayo 10:20. Ndipo**, Kristo anapofanya kazi ndani yako, utaonyesha roho ile ile na kutenda matendo yale yale ya wema—matendo ya haki, na utii. {SCsw 62.3}

Hivyo, hatuna chochote ndani yetu cha kujitapa. Hatuna msingi wa kujitukuza. Msingi wetu pekee wa tumaini letu, uko katika sifa na haki ya Kristo inayohesabiwa kwetu, na katika hiyo inayotekelezwa na Roho Wake akifanya kazi ndani na kupitia sisi (Warumi 4:6). {SCsw 63.1}

Tunapozungumzia imani, kuna utofauti ambao unapaswa kuzingatiwa. Kuna aina ya kuamini ambayo ni tofauti kabisa na imani halisi. Uwepo na nguvu za Mungu, Ukweli wa Neno Lake, ni mambo halisi ambayo hata Shetani na majeshi yake hawawezi kuyapinga au kuyakana kwa moyo wao. Biblia inasema ***"mashetani nao waamini/wanasadiki, na kutetemeka"*** lakini hiyo sio imani. **Yakobo 2:19.** Pale ambapo sio tu kuna kuliamini Neno la Mungu, bali kujinyenyekesha kwa kuyatoa mapenzi yetu Kwake; pale ambapo moyo unajisalimisha Kwake, mapenzi yetu yanalenga na kukita Kwake, ndipo inakuwa imani—imani inayofanya kazi kwa upendo na kutakasa roho. Kupitia imani hii, moyo unafanywa upya katika sura ya Mungu. Na ule moyo, ambao kwa kawaida katika hali yake isiyofanywa upya hauko chini ya sheria ya Mungu, wala hauwezi kuwa, sasa unapendezwa na kufurahia maagizo Yake Bwana, yaliyo matakatifu, ukishangilia pamoja na mwandishi wa Zaburi kwa kusema, "***"Sheria Yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa.*** **Zaburi 119:97** Na haki ya sheria inatimizwa ndani yetu, "sisi tusioenenda kwa mwili, bali kwa Roho." **Warumi 8:1.** {SCsw 63.2}

Kuna wale ambao wameujua upendo wa Kristo, unaosamehe dhambi, na ambao kwa kweli wanatamani kuwa watoto wa Mungu, lakini wanatambua kuwa tabia yao sio kamilifu, maisha yao yana makosa, na huwa tayari kutilia shaka uzoefu wao na hujiuliza kama mioyo yao imejengwa upya na Roho Mtakatifu kweli. Kwa

hawa ningesema, Msirudi nyuma kwa kukata tamaa. Mara nyingi itabidi tunyenyekee na kulia mbele za miguu ya Yesu kwa ajili ya mapungufu yetu na makosa, lakini hatupaswi kukata tamaa. Hata pale tunaposhindwa na adui na kuangushwa chini, hatukataliwi au kutupiliwa mbali, hatuachwi wala kupuuzwa, mbali na Mungu. La! Kristo Yuko mkono wa kuume wa Mungu, ambaye pia anafanya maombezi kwa ajili yetu. Yohana mpendwa alisema,

***"Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki,*** **1 Yohana 2:1** Na msisahau Maneno ya Kristo, ***"kwa maana Baba Mwenyewe awapenda. Yohana 16:27***." Yeye Anatamani kukurejesha Kwake, ili kuona usafi na utakatifu Wake unaoakisiwa ndani yenu. Na ikiwa mtajitoa Kwake, Yeye aliyeanza kazi nzuri ndani yenu ataitimiza mpaka siku ya Kristo Yesu. Ombeni kwa bidii zaidi; muamini kwa ukamilifu zaidi. Tunapofikia hatua ya kutotumaini katika nguvu zetu, hebu na tuziamini nguvu za Mwokozi wetu, nasi tutamsifu Yeye ambaye ni afya ya nyuso zetu. {SCsw 64.1}

Kadiri unavyomkaribia Yesu, ndivyo utakavyozidi kujiona kuwa una mapungufu zaidi katika macho yako mwenyewe; kwa kuwa uoni wa macho yako utakuwa wazi zaidi, na makosa na kasoro zako zitajidhihirisha kwa upana nawe utaweza kuona tofauti kubwa kati yako na asili ya Bwana iliyo kamili. Hii ni ishara kwamba udanganyifu wa Shetani umepoteza nguvu yake; kwamba nguvu ya kuleta uhai, na kuhuisha ya Roho wa Mungu inazindua. {SCsw 64.2}

Hakuna upendo wa mwanadamu kwa Yesu, unaoishi ndani kabisa kwenye vina vya moyo, usioweza kutambua jinsi ulivyotota dhambini (sinfulness). Nafsi inayobadilishwa kwa neema ya Kristo itavutiwa, itaitamani na kuithamini tabia Yake ya Mungu/Ki*ungu*, lakini tusipoona upungufu wetu wa maadili, ni ushahidi usiopingika kwamba hatujapata mtazamo

unaotuwezesha kuona jinsi uzuri na ubora wa Kristo ulivyo haswa. **{SCsw 65.1}**

Kadri tutakavyojithamini kwa udogo zaidi, na kupunguza kujikuza machoni petu wenyewe, ndivyo tutakavyozidi kuona thamani ya Mwokozi wetu zaidi, usafi na uzuri Wake usio na kifani. Mtazamo wa dhambi zetu wenyewe, unatusukuma kwake Yeye anayeweza kusamehe; na wakati roho inayotambua haina msaada, inapomfikia Kristo, Yeye atajifunua Mwenyewe kwa uwezo/nguvu. Kadiri hisia zetu za uhitaji zinavyotusukuma kwenda Kwake Yeye na kwa Neno la Mungu, ndivyo tutakavyokuwa na mitazamo iliyoinuliwa zaidi kuhusu tabia Yake, na ndivyo tutakavyoakisi sura Yake kikamilifu. **{SCsw 65.2}**

## SURA YA 8 - KUKUA KATIKA KRISTO

Mabadiliko ya moyo ambayo kwayo tunakuwa watoto wa Mungu yako katika Biblia, nayo yanazungumziwa kama kuzaliwa. Tena, hulinganishwa na kumea kwa mbegu njema iliyopandwa na mkulima. Vivyo hivyo wale ambao wameongoka tu kwa Kristo, ni, "kama watoto wachanga waliozaliwa," ambao wanapaswa "kukua" hadi kufikia kimo cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu. 1 Petro 2:2; Waefeso 4:15. Au kama mbegu nzuri iliyopandwa shambani, hawa wanapaswa kukua na kuzaa matunda. Isaya anasema kwamba ***"wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili Yeye atukuzwe.*** **Isaya 61:3** Kwa hivyo kutokana na maisha ya asili, vielelezo hutolewa, ili kutusaidia kuelewa vyema Ukweli wa mafumbo na siri za maisha ya kiroho. **{SCsw 67.1}**

Hekima, stadi na ujuzi wote wa mwanadamu haviwezi kuleta uhai hata kwa uhai wa kitu kidogo zaidi katika asili. Ni

kupitia tu uhai ambao Mungu Mwenyewe ameutoa, ndipo mmea au mnyama anaweza kuishi. Kwa hivyo ni kupitia uzima kutoka kwa Mungu pekee ndipo uhai wa kiroho huzaliwa katika mioyo ya wanadamu. Isipokuwa mtu "**amezaliwa kutoka juu**," hawezi kuwa mshiriki wa uzima ambao Kristo alikuja kutoa. **Yohana 3:3.** {SCsw 67.2}

Kama ilivyo katika maisha, ndivyo ilivyo kwenye ukuaji. Ni Mungu anayeleta chipukizi kuchanua na ua kuzaa matunda. Ni kwa nguvu Yake kwamba mbegu inamea, ***"Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke.*** **Marko 4:28**. Na nabii Hosea anasema kuhusu Israeli, kwamba ***"naye atachanua maua kama nyinyoro, watafufuka kama ngano, na kuchanua maua kama mzabibu"*** **Hosea 14:5, 7.** Na Yesu anatuambia " ***Yatafakarini maua jinsi yameavyo." Luka 12:27.*** Mimea na maua hukua sio kwa kusumbuka/masumbufu au wasiwasi yao yenyewe au kwa juhudi zao, bali kwa kupokea ugavi na majaliwa ambayo Mungu ameipa tayari ili kuhudumu katika maisha yao. Mtoto hawezi kuongeza kimo chake kwa wasiwasi wa aina yoyote au nguvu zake mwenyewe. Ndivyo ilivyo hata kwako wewe, wewe huwezi kupokea ukuaji wa kiroho, kwa kuwa na wasiwasi au kuweka juhudi zako mwenyewe. Mmea, na mtoto, hukua kwa kupokea kutoka kwenye mazingira yake nyenzo au kile kinachohudumia maisha/uhai wake—hewa, mwanga wa jua, na chakula. Kama vipawa hivi vya asili vilivyo kwa wanyama na mimea, ndivyo Kristo alivyo kwa wale wanaomtumaini Yeye. Yeye Ndiye "nuru yao ya milele," "jua na ngao." Isaya 60:19; Zaburi 84:11. Atakuwa kama ***"kama umande kwa Israeli; Atashuka kama mvua juu ya majani yaliyokatwa. Hosea 14:5,*** **Zaburi 72:6** Yeye Ndiye maji yaliyo hai, ***"chakula cha Mungu ……… kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.*** **Yohana 6:33** {SCsw 67.3}

Katika zawadi isiyo na kifani ya Mwanawe (isiyo na mfanano), Mungu ameuzunguka ulimwengu wote kwa angahewa ya neema

ambayo ni halisi kama ilivyo hewa inayozunguka dunia nzima. Wote wanaochagua kupumua angahewa hii inayotoa uhai wataishi na kukua hadi kufikia kimo cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu. **{SCsw 68.1}**

Kama vile ua linavyogeukia jua, ili miale angavu iweze kusaidia katika kukamilisha uzuri na ulinganifu wake, vivyo hivyo tunapaswa kugeukia Jua la Haki, ili nuru ya mbinguni ituangazie sisi, ili tabia zetu ziweze kukuzwa katika mfano wa Kristo. **{SCsw 68.2}**

Yesu anafundisha jambo lile lile anaposema, "***Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani Yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.*** **Yohana 15:4-5***.* Wewe ni tegemezi kwa Kristo vile vile, ili kuishi maisha matakatifu, kama vile tawi kwenye mti linavyotegemea ukuaji wake na kuzaa matunda kutokana na shina la awali (mama mti au parent stock). Mbali na Kristo, wewe huna uzima. Huna uwezo wa kupinga majaribu au kukua katika neema na utakatifu. Ukiwa ndani Yake, unaweza kustawi na kunawiri. Ukichukua maisha yako kutoka Kwake, hautanyauka wala kukosa matunda. Utakuwa kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji. **{SCsw 68.3}**

Wengi wana wazo kwamba lazima wafanye sehemu fulani ya kazi peke yao. Wamemwamini Kristo kwa msamaha wa dhambi, lakini sasa wanatafuta kuishi ipasavyo, kwa juhudi zao wenyewe. Lakini kila juhudi kama hiyo lazima ishindikane. Yesu anasema, "Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." Ukuaji wetu katika neema, furaha yetu, manufaa yetu,—yote yanategemea muungano wetu na Kristo. Ni kwa ushirika Naye, kila siku, kila

saa,—kwa kukaa ndani Yake,—ndipo tunapaswa kukua katika neema. Yeye sio Mwenye kuianzisha imani yetu tu, bali pia Mwenye kuitimiza imani yetu. Ni Kristo,kwanza, na mwisho na siku zote. Yeye atakuwa pamoja nasi, sio mwanzoni na mwisho wa njia yetu, bali katika kila hatua ya njia. Daudi anasema, "***Nimemweka Bwana mbele yangu daima, Kwa kuwa Yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa."*** **Zaburi 16:8** **{SCsw 69.1}**

Je, wewe unauliza, "Nitakaaje ndani ya Kristo?" Kwa njia ile ile kama uliyompokea mwanzoni." ***"Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye; Lakini mwenye haki Wangu ataishi kwa imani*** **Wakolosai 2:6, Waebrania 10:38** Wewe ulijitoa kwa Mungu, kuwa Wake kikamilifu, kumtumikia na kumtii Yeye, na ukampokea Kristo kama Mwokozi wako. Hukuweza kujifanyia mwenyewe upatanisho kwa dhambi zako au kubadilisha moyo wako mwenyewe; lakini ukiwa umejitoa kwa Mungu, unaamini kwamba Yeye kwa ajili ya Kristo amefanya haya yote kwa ajili yako. Kwa imani ukawa wa Kristo, na kwa imani unapaswa kukua ndani Yake—kwa kutoa na kupokea. Unapaswa kutoa yote,—moyo wako, nia yako, mapenzi yako, huduma yako,—jitoe Kwake kutii matakwa Yake yote, na haya ni lazima uyabebe yote--Kristo utimilifu wa baraka zote, ili akae moyoni mwako, awe nguvu yako, haki yako, msaidizi wako wa milele,—akupe nguvu ya kutii. **{SCsw 69.2}**

Jitoe wakfu kwa Mungu kila asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Hebu Ombi lako na liwe, "Nitwae, Ee Bwana, kuwa wako kikamilifu. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika utumishi Wako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako." Hii ni mada ya kila siku. Kila asubuhi jitoe wakfu mwenyewe kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Salimisha mipango yako yote Kwake Bwana, ili itekelezwe au ibatilishwe/ibadilishwe kama ambayo majaliwa na uongozi Wake Mungu utakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku wewe unaweza

kuyakabidhi maisha yako mikononi mwa Mungu, na ndivyo maisha yako yatakavyoweza kufinyangwa/kuumbwa zaidi na zaidi kwa kufanana na maisha ya Kristo. **{SCsw 70.1}**

Maisha katika Kristo ni maisha ya utulivu. Huenda kusiwe na mihemko ya hisia za furaha, lakini kunapaswa kuwa na kumtegemea Mungu na amani ya kudumu. Tumaini lako haliko ndani yako mwenyewe; bali lipo ndani ya Kristo. Udhaifu wako umeunganishwa na nguvu Zake, ujinga wako na hekima Yake, udhaifu wako na nguvu Zake za kudumu. Kwa hivyo hupaswi kujiangalia mwenyewe, usiruhusu akili kukaa juu yako mwenyewe, bali imtazame Kristo. Acha akili ikae juu ya upendo Wake, juu ya uzuri, na ukamilifu, wa tabia Yake. Kristo katika kujikana Kwake nafsi, Kristo katika kudhalilishwa Kwake, Kristo katika Usafi na utakatifu Wake, Kristo katika upendo Wake usio na kifani/mfanano—hii ndiyo mada ambayo roho inapaswa kutafakari. Ni kwa kumpenda, kumwiga Yeye, na kumtegemea Yeye kikamilifu, ndipo utakapobadilishwa katika mfano Wake. **{SCsw 70.2}**

Yesu anasema, "Kaeni ndani Yangu." Maneno haya yanaonyesha wazo la kupumzika, utulivu, uimara, kujiamini. Tena anaalika, ***"Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha."*** **Mathayo 11:28.** Maneno ya mwandishi wa-Zaburi yanaelezea wazo lile lile: "***Ukae kimya mbele za Bwana, Nawe umngojee kwa saburi; Na Isaya anatoa uhakikisho, na kwa kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini.*** **Zaburi 37:7, Isaya 30:15** Pumziko hili halipatikani katika kutofanya kazi au kuishi bila utendaji; kwani katika mwaliko wa Mwokozi ahadi ya kupumzika imeunganishwa na wito wa kufanya kazi: ***"Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu"*** **Mathayo 11:29** Moyo unaomtegemea Kristo kikamilifu utakuwa dhati na bidii zaidi katika kazi kwa ajili Yake Bwana. **{SCsw 71.1}**

Akili inapokita kwenye kujifikiria yenyewe, inageuzwa mbali na Kristo, Chanzo cha nguvu na uzima. Kwa hivyo ni juhudi ya Shetani endelevu, kuondoa usikivu kutoka kwa Mwokozi na hivyo kuzuia muungano na ushirika wa roho na Kristo. Anasa za dunia, wasiwasi na mashaka ya maisha, makosa ya wengine, au makosa, kasoro na mapungufu yako mwenyewe—kwa yoyote au yote haya, adui atajaribu kugeuza akili. Usidanganyike na mbinu zake adui. Wengi ambao wana dhamiri iliyo makini, na wanaotamani kuishi kwa ajili ya Mungu, mara nyingi huongozwa kufikiria makosa na udhaifu wao wenyewe, na hivyo kwa kuwatenganisha na Kristo, adui anatumaini kupata ushindi. Hatupaswi kuifanya nafsi/umimi kuwa kitovu na kuendekeza wasiwasi na hofu kwamba, Je, tutaokolewa kweli. Haya yote hugeuza roho kutoka kwa Chanzo cha nguvu zetu. Mkabidhi Mungu kutunza roho yako, na umtumaini Yeye. Zungumza na umfikirie Yesu. Acha nafsi ipotee ndani Yake. Weka mbali mashaka yote; ondoa hofu zako. Useme pamoja na mtume Paulo,{SCsw 71.2}

***"lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo Yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu.*** **Wagalatia 2:20**. Pumzika ndani ya Mungu. Yeye Anaweza kukilinda kile ulichokiweka amana Kwake. Ikiwa utajiachia mikononi Mwake,Yeye atakuwezesha uwe zaidi ya mshindi katika shuguli hiyo, kupitia Yeye aliyekupenda. {SCsw 71.2}

Kristo alipochukua asili ya kianadamu juu Yake, Aliufunga ubinadamu Kwake kwa kifungo cha upendo ambacho hakiwezi kuvunjwa na nguvu yoyote isipokuwa chaguo la mwanadamu mwenyewe. Shetani ataendelea kuleta vivutio kila mara ili kutushawishi kuvunja kifungo hiki—kuchagua kujitenga na Kristo. Hapa ndipo tunapohitaji kukesha, kuwa makini, kujitahidi, kupambana, na kuomba, ili kusiwe na kitu kinachoweza kutushawishi kuchagua bwana mwingine; kwani sisi daima tuko

huru kufanya hivi. Lakini sisi tumkazie macho Kristo, Naye atatuhifadhi/atatulinda. Tukimtazama Yesu, tuko salama. Hakuna kile kinachoweza kututoa mkononi Mwake. Kwa kumtazama Yeye kila mara, ***"tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana" 2 Wakorintho 3:18*** {SCsw 72.1}

Ilikuwa hivyo kwamba wanafunzi wa kwanza/awali, walipata kufanana kwao na Mwokozi mpendwa. Wanafunzi hao waliposikia Maneno ya Yesu, walihisi kumhitaji Yeye. Walimtafuta, wakampata, wakamfuata. Walikuwa pamoja Naye nyumbani, mezani, chumbani, shambani. Walikuwa pamoja Naye kama wanafunzi na mwalimu, wakipokea kutoka kinywani Mwake masomo ya Ukweli mtakatifu kila siku. Walimtazama Yeye, kama watumishi wa bwana wao, ili kujifunza wajibu wao. Wanafunzi hao walikuwa binadamu, wenye tabia na "tamaa kama sisi". **Yakobo 5:17.** Walikuwa na vita ile ile ya kupigana na dhambi. Walihitaji neema ile ile, ili kuishi maisha matakatifu. {SCsw 72.2}

Hata Yohana, mwanafunzi mpendwa, yule aliyeakisi kikamilifu mfano wa Mwokozi, hakuwa na tabia hiyo ya kupendeza. Hakuwa tu mwenye kujiamini mwenyewe na mwenye tamaa ya makuu ya kujitakia heshima, bali pia alikuwa anahamaki haraka, na mwenye kinyongo na kuudhika pale anapojeruhiwa. Lakini tabia ya Mungu ilipodhihirishwa kwake, aliona upungufu wake mwenyewe na akanyenyekezwa na maarifa haya. Nguvu na uvumilivu, uwezo na mapenzi, huruma nyororo, kujali, ukuu na upole, ambavyo aliviona katika maisha ya kila siku ya Mwana wa Mungu, viliijaza roho yake kwa upendo na hisia ya kina toka moyoni ya heshima kubwa, shukrani na kuvutiwa na Bwana. Siku baada ya siku moyo wake ulivutwa kwa Kristo, hadi alipoteza tabia ya kujipenda mwenyewe kwa ajili ya kumpenda Bwana wake. Tabia yake ya kuudhika kirahisi, kinyongo na msukumo mkali wa matamanio ya ukuu, kufanikiwa, kujulikana, kufikia malengo na kujipatia heshima,

hivi vyote vilikubali kuumbwa upya na nguvu ya Kristo. Ushawishi wa Roho Mtakatifu unaofufua upya uliufanya moyo wake kuwa mpya. Nguvu ya upendo wa Kristo ilileta mabadiliko ya tabia. Haya ndiyo matokeo ya uhakika ya muungano na Yesu. Kristo anapokaa moyoni, asili yote hubadilishwa. Roho wa Kristo, upendo Wake, hulainisha moyo, hutiisha roho, na kuinua mawazo na matamanio kwa Mungu na mbinguni. **{SCsw 73.1}**

Wakati Kristo alipopaa mbinguni, hisia ya uwepo Wake ilikuwa bado na wafuasi Wake. Ulikuwa uwepo binafsi kwa kila mmoja wao, uliojaa upendo na nuru. Yesu, Mwokozi, Yule aliyetembea, akizungumza, na kuomba nao, ambaye alikuwa akisema yale yenye kuleta matumaini na faraja kwa mioyo yao, wakati ujumbe wa amani, ulipokuwa bado midomoni mwake, alichukuliwa kutoka kwao na kwenda mbinguni, na toni ya sauti Yake ilirejea kwao, wakati wingu la malaika lilipokuwa likimpokea—***"na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*** **Mathayo 28:20** Alikuwa amepaa mbinguni katika umbo la mwanadamu/ubinadamu. Walijua kwamba alikuwa mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, kwamba bado alikuwa Rafiki na Mwokozi wao; kwamba huruma Zake hazikubadilika; kwamba bado alikuwa akijitambulisha na wanadamu wanaoteseka. Alikuwa akiwasilisha mbele za Mungu haki/sifa ya damu Yake ya thamani, akionyesha mikono na miguu Yake iliyojeruhiwa, kwa ukumbusho wa gharama/bei aliyolipa kwa ajili ya waliokombolewa. Walijua kwamba alikuwa amepaa mbinguni kuwaandalia mahali, na kwamba angerudi tena na kuwachukua Kwake. **{SCsw 73.2}**

Walipokutana pamoja baada ya kupaa mbinguni walikuwa na hamu ya kuwasilisha maombi yao kwa Baba katika Jina la Yesu. Kwa kicho na kustaajabu, walinyenyekea katika maombi, wakirudia uhakikisho, "***Mkimwomba Baba neno lolote atawapa kwa Jina Langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa Jina Langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.*** **Yohana 16:23-24.**

Walinyoosha mkono wa imani juu zaidi na zaidi kwa hoja yenye nguvu, ***"Kristo Yesu Ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, Naye Yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena Ndiye anayetuombea."*** **Warumi 8:34** Na Pentekoste iliwaletea uwepo wa Mfariji, ambaye Kristo alisema, "Naye atakuwa ndani yenu" Na zaidi ya hayo alisema, "***yawafaa ninyi Mimi niondoke, kwa maana Mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali Mimi nikienda Zangu, nitampeleka kwenu.Yohana 14:17,*** **Yohana 16:7** Tangu wakati huo, kupitia Roho, Kristo angekaa daima mioyoni mwa watoto Wake. Muunganiko wao Naye ulikuwa wa karibu zaidi kuliko wakati Kristo akiwa pamoja nao kimwili. Nuru, upendo, na nguvu za Kristo aliye ndani yao iling'aa kupitia kwao, hata watu waliona, ***"wakastaajabu; wakatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu."*** **Matendo 4:13.** {SCsw 74.1}

Yote aliyokuwa Kristo kwa wanafunzi, anataka kuwa hivyo kwa watoto Wake leo; kwa maana katika sala hiyo ya mwisho, akiwa na kundi dogo la wanafunzi waliomzunguka, alisema, **"Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao" Yohana 17:20** {SCsw 75.1}

Yesu aliomba kwa ajili yetu, na aliiomba ili tuwe wamoja Naye, kama vile Yeye alivyo mmoja na Baba. Umoja huu ni upi! Mwokozi alisema kuhusu Yeye Mwenyewe, ***"Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; lakini Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake."*** **Yohana 5:19, 14:10** Basi, ikiwa Kristo anakaa katika mioyo yetu, atafanya kazi ndani yetu ***"kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema.*** **Wafilipi 2:13** Sisi tunapaswa kufanya kazi kama Yeye alivyofanya; tutaidhihirisha roho ile ile. Na kwa hiyo, tukimpenda Yeye na kukaa ndani Yake, tutakua "***hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye aliye kichwa, Kristo.*** **Waefeso 4:15** {SCsw 75.2}

•

## SURA YA 9 - KAZI NA UZIMA

Mungu Ndiye chanzo cha uzima na nuru na furaha kwa ulimwengu. Kama miale ya mwanga kutoka jua, kama vijito vya maji vinavyobubujika kutoka kwa chemchemi hai, baraka hutiririka Kwake hadi kwa viumbe Vyake vyote. Na popote uzima wa Mungu ulipo mioyoni mwa wanadamu, utatiririkia kwa wengine kwa upendo na baraka. {SCsw 77.1}

Furaha ya Mwokozi wetu ilikuwa katika kuinua na kukomboa wanadamu walioanguka. Kwa hili, Yeye hakuhesabu maisha Yake kuwa ya thamani Kwake, bali alivumilia msalaba, akiidharau aibu. Ndivyo malaika wanavyojishughulisha kila wakati, kufanya kazi kwa ajili ya furaha ya wengine. Hii ndiyo furaha yao. Kile ambacho mioyo yenye ubinafsi, ingeiona kama huduma ya aibu, kuwahudumia wale walio wanyonge na kwa kila njia duni katika tabia na cheo, ni kazi ya malaika wasio na dhambi. Roho ya upendo wa Kristo ya kujitoa mhanga ni roho iliyosheheni mbinguni

na ndiyo kiini cha furaha Yake. Hii ndiyo roho ambayo wafuasi wa Kristo watakuwa nayo, kazi watakayofanya. {SCsw 77.2}

Upendo wa Kristo unapotunzwa na kuthaminiwa ndani ya moyo, kama harufu tamu ya manukato, hauwezi kufichwa. Ushawishi wake mtakatifu utahisiwa na wote tunaowafikia au kuwasiliana nao. Roho ya Kristo moyoni ni kama chemchemi jangwani, ikitiririka ili kuburudisha wote na kuwafanya wale walio tayari kuangamia, wawe na hamu ya kunywa maji ya uzima. {SCsw 77.3}

Upendo kwa Yesu utaonyeshwa katika hamu ya kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kwa ajili ya baraka na kuinua ubinadamu. Itamwongoza mtu kuwa na upendo, mahusiano ya karibu, kujali, mapenzi, huruma nyororo, kwa viumbe vyote vya utunzaji wa Baba yetu wa mbinguni. {SCsw 77.4}

Maisha ya Mwokozi duniani hayakuwa maisha ya raha, yaliyo rahisi na ya kujishugulikia Yeye Mwenyewe, lakini Aliendelea kufanya kazi kwa dhati, kwa kudhamiria, kwa bidii, na juhudi zisizochoka kwa ajili ya wokovu wa wanadamu waliopotea. Kuanzia horini hadi Kalvari Alifuata njia ya kujikana-nafsi na hakutafuta kuwekwa huru na kazi ngumu zenye kuhenyesha, safari zenye uchungu na masumbufu yenye uchovu na shuguli zenye masumbufu. Alisema, ***"kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi Yake iwe fidia ya wengi."*** **Mathayo 20:28.** Hili lilikuwa ndilo lengo moja kuu la maisha Yake. Kila kitu kingine kilikuwa cha pili na chenye kipaumbele cha chini. Ilikuwa chakula na kinywaji Chake kuyafanya mapenzi ya Mungu na kukamilisha kazi Yake. Ubinafsi/umimi na maslahi binafsi hayakuwa na sehemu katika kazi Yake. {SCsw 78.1}

Kwa hivyo, wale walio washiriki wa neema ya Kristo watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote, ili wengine ambao Aliwafia

waweze kushiriki zawadi ya mbinguni. Watafanya yote wawezayo kuifanya dunia iwe bora kwa ajili ya kukaa kwao ndani yake. Roho hii ni ukuaji wa hakika wa roho iliyoongoka kweli. Mara tu mtu anapomjia Kristo ndipo huzaliwa moyoni mwake hamu ya kuwajulisha wengine jinsi alivyompata rafiki wa thamani katika Yesu; Ukweli unaookoa na kutakasa hauwezi kufungwa moyoni mwake. Ikiwa tunavikwa haki ya Kristo na kujazwa furaha ya Roho Wake anayekaa ndani yetu, hatutaweza kunyamaza. Kama tumeonja na kuona kwamba Bwana ni mwema, tutakuwa na jambo la kuzungumza. Kama pale Filipo alipompata Mwokozi, nasi tutawaalika wengine mbele Zake. Tutajitahidi kuwaonyesha vivutio vya Kristo na mambo yasiyoonekana ya ulimwengu ujao wa mbinguni. Kutakuwa na shauku kubwa ya kufuata njia ambayo Yesu aliipitia. Kutakuwa na hamu kubwa kwamba wale wanaotuzunguka waweze "***kumwona Mwana-Kondoo wa Mungu, Aichukuaye dhambi ya ulimwengu."*** Yohana 1:29. {SCsw 78.2}

Na juhudi za kuwabariki wengine zitatoa mwitikio kwa kurudisha baraka juu yetu wenyewe. Hili lilikuwa kusudi la Mungu katika kutupa sehemu ya kutenda katika mpango wa ukombozi. Yeye Amewapa wanadamu upendeleo wa kuwa washiriki wa asili ya Kiungu na, kwa upande wao, waweze kusambaza baraka kwa wanadamu wenzao. Hii ni heshima ya juu zaidi, furaha kubwa zaidi, kwamba inawezekana kwa Mungu kuwatunukia wanadamu. Wale wanaoshiriki katika kazi za upendo, huletwa karibu zaidi na Muumba wao. {SCsw 79.1}

Mungu angeweza kuwakabidhi malaika wa mbinguni, ujumbe wa injili, na kazi yote ya huduma ya upendo. Angeweza kutumia njia zingine za kutimiza kusudi Lake. Lakini katika upendo Wake usio na kikomo alichagua kutufanya tuwe watendakazi pamoja Naye Mwenyewe, pamoja na Kristo na malaika, ili tuweze kushiriki baraka, furaha, na kuinuliwa kiroho, ambayo huleta huduma hii isiyo na ubinafsi. {SCsw 79.2}

Tunaletwa katika huruma na Kristo kupitia ushirika wa mateso Yake. Kila tendo la kutoa dhabihu nafsi kwa ajili ya mema ya wengine huimarisha roho ya ukarimu katika moyo wa mtoaji, na kumunganisha kwa karibu zaidi na Mkombozi wa ulimwengu, ambaye "Yeye ingawa ***Alikuwa tajiri,…………Alijifanya masikini kwaajili yenu, ili ninyi mpate kuwa matajiri kutokana na umaskini Wake.*** **2 Wakorintho 8:9** Na ni pale tu tunapotimiza kusudi la Mungu katika uumbaji wetu ndipo maisha yanaweza kuwa baraka kwetu. **{SCsw 79.3}**

Ukienda kufanya kazi kama Kristo alivyodisaini/alivyopanga kwamba wanafunzi Wake wafanye, na kuleta roho kwa ajili Yake, utahisi hitaji la uzoefu wa kina zaidi na ujuzi mkubwa zaidi katika mambo ya Mungu, na utakuwa na njaa na kiu ya haki. Utamsihi Mungu, na imani yako itaimarishwa, na roho yako itakunywa maji mengi zaidi kwenye kisima cha wokovu. Kukabiliana na upinzani na majaribu kutakusukuma wewe kwenye Biblia na maombi. Utakua katika neema na ujuzi wa Kristo, na utakua na uzoefu mwingi wenye thamani. **{SCsw 80.1}**

Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine hutoa kina, uthabiti, na uzuri tabia ya Kikristo, na kuleta amani na furaha kwa mwenye tabia hiyo. Matarajio yanainuliwa. Hakuna nafasi ya uvivu au ubinafsi. Wale wanaotumia neema za Kikristo kwa njia hiyo watakua na kuwa na nguvu ya kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Watakuwa na mitazamo ya kiroho iliyo wazi, imani thabiti na inayokua, na nguvu iliyoongezeka katika maombi. Roho wa Mungu, akitembea juu ya roho zao, huleta mapatano matakatifu ya roho kama jibu la mguso wa Kiungu. Wale wanaojitolea kwa juhudi zisizo na ubinafsi kwa ajili ya mema ya wengine hakika wanafanyia kazi wokovu wao wenyewe. **{SCsw 80.2}**

Njia pekee ya kukua katika neema ni kufanya kazi bila ubinafsi, bila kujifikiria wenyewe, kazi ile ambayo Kristo ametuagiza tuifanye—kushiriki, kwa kiwango cha uwezo wetu,

katika kuwasaidia na kuwabariki wale wanaohitaji msaada tunaoweza kuwapa. Nguvu huja kwa mazoezi; utendaji hai, na kujishugulisha, ndiyo sharti halisi la maisha. Wale wanaojitahidi kudumisha maisha ya Kikristo kwa kukubali baraka zinazokuja kupitia njia ya neema, bila kufanya chochote kwa ajili ya Kristo, wanajaribu tu kuishi kwa kula bila kufanya kazi. Na katika ulimwengu wa kiroho kama ilivyo katika ulimwengu wa kimwili/asili, hii daima husababisha kuzorota, kushuka chini kwa ufanisi na kuoza. Mtu ambaye anayekataa kutumia miguu na mikono yake, hivi karibuni atapoteza nguvu zote, za kuvitumia viungo hivi. Hivyo Mkristo ambaye hatatumia nguvu zake alizopewa na Mungu siyo tu kwamba atashindwa kukua na kuwa kama Kristo, bali pia anapoteza nguvu alizokuwa nazo tayari. {SCsw 80.3}

Kanisa la Kristo ni wakala, chombo kilichoteuliwa na Mungu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Utume wake ni kupeleka injili ulimwenguni. Na huu, wajibu upo juu ya Wakristo wote. Kila mtu, kwa kadiri ya kipaji chake na fursa yake, anapaswa kutimiza agizo la Mwokozi. Upendo wa Kristo, uliofunuliwa kwetu, unatufanya tuwe wadeni kwa wote wasiomjua Yeye. Mungu ametupa nuru, sio kwa ajili yetu wenyewe peke yake, bali kuipeleka kwa wote wasiomjua Yeye. {SCsw 81.1}

Kama wafuasi wa Kristo wangekuwa macho kwa wajibu waliopewa, kungekuwa na maelfu pale ambapo kuna mtu mmoja tu leo, anayetangaza injili katika nchi za kipagani. Na wote ambao binafsi, hawangeweza kushiriki moja kwa moja katika kazi hiyo, wangeitegemeza kwa mali zao, huruma zao, na maombi yao. Na kungekuwa na kazi ya dhati na bidii zaidi kwa ajili ya roho katika nchi za Kikristo. {SCsw 81.2}

**[Angalia JoshuaProject.Org-Kuna makundi 7400 kati ya makundi 14,000 ambayo hayajafikiwa. Asilimia 42% ya watu bado hawajafikiwa na injili, na ujio wa Masihi wa hivi karibuni.**

Wayahudi, Wakomunisti, Hindu, Buddha, Shintoism, watu wenye udunia-secular, Confusias, wanaoabudu mizimu ya mababu, na miungi mingine]

Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani au kwa Wakana-Mungu, au hata kuondoka kutoka kwenye kikundi kidogo cha duru ya nyumbani, ikiwa wajibu wetu upo hapo, katika kumfanyia kazi Kristo. Tunaweza kufanya hivi katika mzunguko wa nyumbani, kanisani, na miongoni mwa wale tunaoshirikiana nao, na ambao tunafanya nao biashara. {SCsw 81.3}

Sehemu kubwa ya maisha ya Mwokozi wetu duniani ilitumika katika kazi ngumu yenye kuhenyesha kwa subira, katika karakana ya seremala huko Nazareti. Malaika wahudumu, walimhudumia Bwana wa uzima alipotembea pamoja na wakulima na wafanyakazi, bila kutambuliwa na kuheshimiwa. Alikuwa akitimiza utume Wake kwa uaminifu huku akifanya kazi ya tasnia Yake ya unyenyekevu kama alivyowaponya wagonjwa au kutembea kwenye mawimbi ya Galilaya yaliyorushwa na dhoruba. Kwa hivyo katika majukumu haya ya unyenyekevu na duni kabisa na ya nafasi za chini kabisa maishani, sisi tunaweza kutembea na kufanya kazi pamoja na Yesu. {SCsw 81.4}

Mtume anasema, **“kila mtu na akae mbele za Mungu katika hali iyo hiyo aliyoitwa nayo.” 1Wakorintho 7:24** Mfanyabiashara anaweza kuendesha biashara au shughuli zake kwa njia ambayo itamtukuza Bwana wake kwa sababu ya uadilifu wake. Ikiwa yeye ni mfuasi wa kweli wa Kristo, atabeba dini yake katika kila kitu kinachofanyika na kuwafunulia wanadamu roho ya Kristo. Fundi mitambo anaweza kuwa mwakilishi mwenye bidii na mwaminifu wa Yeye aliyefanya kazi kwa bidii katika maisha ya chini/duni, kati ya vilima vya Galilaya. Kila mtu anayetaja Jina la Kristo anapaswa kufanya kazi ili wengine, kwa kuona matendo yake mema, waweze kuongozwa kumtukuza Muumba na Mkombozi wao. {SCsw 82.1}

Wengi wamejitetea na kujitolea udhuru ili wasitoe vipawa vyao kwa huduma ya Kristo kwa sababu wengine walitunukiwa vipawa vikuu, urithi, bahati, uwezo na faida fulani kubwa kuliko wao (advantages). Maoni yameenea kwamba ni wale tu walio na vipaji maalum ndio wanaohitajika kuweka wakfu stadi na uwezo wao kwa huduma ya Mungu. Imeeleweka na wengi kwamba talanta hutolewa kwa watu fulani tu, waliopendelewa, na wengine ambao bila shaka hawahitaji kushiriki katika kazi ngumu au zawadi, hutengwa, na hivyo hawapokei hivi vipawa. Lakini haijaonyeshwa hivyo katika mfano wa Yesu. Wakati bwana wa nyumba alipowaita watumishi wake, aliwapa kila mtu kazi yake. {SC

Kwa roho ya upendo tunaweza kutekeleza majukumu ya maisha yaliyo ya unyenyekevu "kama kwa Bwana." Wakolosai 3:23. Ikiwa upendo wa Mungu uko moyoni, utaonyeshwa katika maisha. Harufu ya manukato nzuri ya Kristo itatuzunguka, kwa ushawishi

Haupaswi kusubiri matukio makubwa au kutarajia ustadi au uwezo wa ajabu kabla ya kuanza kumfanyia Mungu kazi. Huna haja ya kuwa na mawazo kuhusu kile ambacho ulimwengu utafikiria kukuhusu wewe. Ikiwa maisha yako ya kila siku ni ushuhuda wa usafi wa moyo na unyofu wa imani yako, na wengine wanasadiki kwamba wewe unatamani kuwanufaisha, juhudi zako hazitapotea kabisa. {SCsw 83.1}

Wanafunzi wa Yesu walio wanyenyekevu na maskini zaidi wanaweza kuwa baraka kwa wengine. Huenda wasitambue kwamba wanafanya mema yoyote maalum, lakini kwa ushawishi wao ambao hata wao wanaweza kuutoa bila ufahamu, unaweza kuanzisha mawimbi ya baraka ambayo yatapanuka na kuongezeka kwa kina, na kuwa na matokeo yenye baraka ambayo huenda watu wasijue, hadi siku ya mwisho duniani, kutoa thawabu. Hawajisikii au hawajui kwamba wanafanya jambo lolote kubwa. Hawahitajiki kujipa uchovu kwa wasiwasi kuhusu mafanikio. Wanapaswa tu

kuendelea mbele kimya kimya, wakifanya kwa uaminifu kazi ambayo Mungu amewapa katika majaliwa na uongozi Wake, na maisha yao hayatakuwa bure. Nafsi/tabia zao wenyewe zitakuwa zikikua zaidi na zaidi katika mfano wa Kristo; wao ni watendakazi pamoja na Mungu katika maisha haya na hivyo wanafaa kwa kazi ya juu zaidi na furaha isiyo na kivuli ya maisha yajayo mbinguni. {SCsw 83.2}

## SURA YA 10 - MAARIFA YA MUNGU

Kuna njia nyingi ambazo Mungu anatafuta kujitambulisha kwetu na kutuleta katika ushirika Naye. Asili, uumbaji, huzungumza na hisia zetu bila kukoma. Moyo ulio wazi utavutiwa na upendo na utukufu wa Mungu kama ulivyofunuliwa kupitia kazi za mikono Yake. Sikio linalosikiliza linaweza kusikia na kuelewa mawasiliano ya Mungu kupitia vitu vya asili. Mashamba ya kijani kibichi, miti mirefu, machipukizi na maua, mawingu yanayopita, mvua inayonyesha, kijito kinachotoa sauti, utukufu wa mbingu, huzungumza na mioyo yetu, na kutualika kumfahamu Yeye aliyeviumba vyote. {SCsw 85.1}

Mwokozi wetu aliunganisha masomo Yake ya thamani na vitu vya asili. Miti, ndege, maua ya mabonde, vilima, maziwa, na mbingu nzuri, pamoja na matukio na mazingira ya maisha ya kila siku, yote yaliunganishwa na maneno ya Kweli, ili masomo Yake yaweze kukumbukwa na kuletwa mara nyingi akilini, hata katikati ya shughuli nyingi za maisha ya mwanadamu ya kazi ngumu. {SCsw 85.2}

Mungu angependa watoto Wake wathamini kazi Zake na kufurahia uzuri wenye usahili tulivu ambao amepamba nao makao yetu ya kidunia. Yeye ni mpenda uzuri, na zaidi ya uzuri wote unaovutia kwa nje, Yeye Anapenda uzuri wa tabia; Angependa tukuze na kupalilia usafi wa moyo, usahili na unyenyekevu, na

neema za utulivu wa maua. {SCsw 85.3}

Kama tukisikiliza tu, kazi za Mungu zilizoumbwa zitatufundisha masomo ya thamani na muhimu ya utii na uaminifu. Kuanzia nyota ambazo zinazotembea katika njia zao zisizo na alama, kupitia angani zikifuata kwa umakini njia yao iliyoamriwa kutoka zama hadi zama, hadi chembe ndogo zaidi ya atomi, vitu vya asili hutii mapenzi ya Muumba. Na Mungu hujali kila kitu na hukitegemeza kila alichokiumba. Yeye anayeshikilia idadi za sayari zizohesabika kwa wingi (worlds/malimwengu!), wakati huo huo hujali mahitaji ya shomoro mdogo wa kahawia anayeimba wimbo wake wa unyenyekevu bila woga. Wakati wanadamu wanapoenda kwenye kazi zao ngumu kila siku, kama wanavyoshiriki katika maombi; wanapolala usiku, na wanapoamka asubuhi; Tajiri anapokula karamu katika jumba lake la kifalme, au maskini anapowakusanya watoto wake kwenye meza ndogo, iliyo na chakula haba, kila mmoja anaangaliwa kwa huruma nyororo, upendo mwanana, kujali na mahusiano ya kina na Baba wa mbinguni. Hakuna machozi yanayomwagika ambayo Mungu hayaoni. Hakuna tabasamu ambalo Yeye haliangalii. {SCsw 85.4}

Kama tungeamini kikamilifu hili, wasiwasi wote usiofaa au unaopitiliza, ungeondolewa. Maisha yetu hayangejawa na kukatishwa tamaa kama sasa; kwani kila kitu, kiwe kikubwa au kidogo, kingeachwa mikononi mwa Mungu, ambaye hashangazwi na wingi wa masumbufu, au kuzidiwa na uzito wake. Tunapaswa kufurahia pumziko la roho ambalo wengi wamekuwa wageni kwa hilo, kwa muda mrefu. {SCsw 86.1}

Hisia zako zinapofurahia uzuri wa kuvutia wa dunia, fikiria ulimwengu ujao, ambao hautawahi kujua doa la dhambi na kifo; ambapo uso wa asili hautavaa tena kivuli cha laana. Hebu mawazo yako yafikirie nyumba ya waliookolewa, na ukumbuke

kwamba itakuwa tukufu zaidi kuliko mawazo yako angavu zaidi yanavyoweza kuonyesha. Katika vipawa mbalimbali vya Mungu katika maumbile tunaona mng'ao hafifu tu, wa utukufu Wake. Imeandikwa, **"jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.** *1 Wakorintho 2:9* {SCsw 86.2}

Mshairi na mtaalamu wa asili, wana mambo mengi ya kusema kuhusu asili, lakini ni Mkristo ndiye anayefurahia uzuri wa dunia kwa kuthamini haya, kwa moyo wa shukrani kubwa zaidi, kwa sababu anatambua kazi ya mikono ya Baba yake na anaona upendo Wake katika maua, vichaka na miti. Hakuna anayeweza kuthamini kikamilifu umuhimu wa kilima na bonde, mto na bahari, ambaye hatazami kazi hizi kama onyesho na tamko la upendo wa Mungu kwa mwanadamu. {SCsw 87.1}

Mungu huzungumza nasi kupitia utendaji Wake wa majaliwa/maongozi na kupitia ushawishi wa Roho Wake moyoni. Katika hali zetu na mazingira yetu, na katika mabadiliko yanayotuzunguka yanayotokea kila siku, tunaweza kupata masomo ya thamani ikiwa mioyo yetu iko wazi kuyatambua. Mwandishi wa Zaburi, akifuatilia kazi ya majaliwa ya Mungu, anasema, ***"Nchi imejaa fadhili za Bwana. Aliye na hekima na ayaangalie hayo; Na wazitafakari fadhili za Bwana. Zaburi 33:5, 107:43.***

Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake. Hapa tuna ufunuo ulio wazi zaidi wa tabia Yake, jinsi alivyoshughulika na wanadamu, na kazi kubwa ya ukombozi. Hapa historia ya wazee wa imani na manabii na watu wengine watakatifu wa kale inafunuliwa kwetu. Hawa walikuwa watu "walikuwa binadamu, wenye tabia kama sisi." Yakobo 5:17. Tunaona jinsi walivyopambana na kukata tamaa kama sisi, jinsi walivyoanguka chini ya majaribu kama sisi, lakini wakajipa moyo tena na kushinda kupitia neema ya Mungu; na, tukiwatazama, tunatiwa moyo katika

kutafuta uadilifu. Tunaposoma kuhusu uzoefu wa thamani waliopewa, kuhusu nuru na upendo na baraka ambazo zilikuwa zao kufurahia, na kuhusu kazi waliyoifanya kupitia neema waliyopewa, na roho iliyowaongoza/iliyowahuisha, inawasha mwali wa njia takatifu ya kuiga mioyoni mwetu na hamu ya kuwa kama wao katika tabia—kama wao, kutembea na Mungu. {SCsw 87.3}

Yesu alisema kuhusu Maandiko ya Agano la Kale,—na je, hii sio kweli zaidi kuhusu Maandiko ya Agano Jipya—***"Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi,*** **Yohana 5:39.** Ndiyo, Biblia nzima inasimulia kuhusu Kristo. Kuanzia rekodi ya kwanza ya uumbaji—kwa maana "pasipo Yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika"—hadi ahadi ya mwisho inayofunga Biblia, "Tazama, Naja upesi," tunasoma matendo Yake na kusikiliza sauti Yake. Yohana 1:3; Ufunuo 22:12. Kama unataka kumjua Mwokozi, jifahamishe Maandiko Matakatifu {SCsw 88.1}

Ujaze moyo wote kwa maneno ya Mungu. Hayo ndiyo maji yaliyo hai, yakitoa kiu yako inayofanya koo likauke na kupungukiwa na maji mwilini. Hayo ndiyo mkate ulio hai kutoka mbinguni. Yesu anatangaza, "***Msipoula mwili Wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu Yake, hamna uzima ndani yenu.*** Na anajieleza kwa kusema, ***Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima. Yohana 6:53, 63."*** Miili yetu hujengwa kutokana na kile tunachokula na kunywa; na kama ilivyo katika uchumi wa asili, vivyo hivyo katika uchumi wa kiroho: kile tunachotafakari ndicho kitakachoipa asili yetu ya kiroho, toni, hekima, sauti na nguvu. {SCsw 88.2}

Mada ya ukombozi ni ile ambayo malaika wanatamani kuiangalia; hii itakuwa sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika zama zote zisizokuwa na mwisho, za umilele. Je, haistahili

basi kutafakariwa na kusomwa kwa makini sasa? Rehema na upendo usio na kikomo wa Yesu, dhabihu iliyotolewa kwa ajili yetu, inahitaji tafakari nzito, umakini adhimu na kicho. Tunapaswa kukita katika tabia ya Mkombozi na Mwombezi wetu mpendwa. Tunapaswa kutafakari utume wa Yeye aliyekuja kuwaokoa watu Wake kutoka kwa dhambi zao. Tunapotafakari mada za mbinguni, imani na upendo wetu vitakuwa na nguvu zaidi, na maombi yetu yatakubalika zaidi na zaidi kwa Mungu, kwa sababu yatachanganyika zaidi na zaidi na imani na upendo. Yatakuwa yenye akili na bidii. Kutakuwa na ujasiri na imani zaidi katika Yesu, na uzoefu wa kila siku, ulio hai katika uwezo Wake wa kuwaokoa kabisa wote wanaomjia Mungu kupitia Kwake. **{SCsw 88.3}**

Tunapotafakari ukamilifu wa Mwokozi, tutatamani kubadilishwa kabisa na kufanywa upya katika sura ya usafi Wake. Kutakuwa na njaa na kiu ya roho ya kuwa kama Yeye tunayemwabudu na kumthamini. Kadiri mawazo yetu yanavyozidi kukaa juu ya Kristo, ndivyo tutakavyozungumza kumhusu kwa wengine na kumwakilisha kwa ulimwengu. **{SCsw 89.1}**

Biblia haikuandikwa kwa ajili ya msomi pekee yake; kinyume chake, ilikusudiwa kwa watu wa kawaida. Kweli kuu na muhimu kwa wokovu zinawekwa wazi kama adhuhuri; na hakuna atakayekosea na kupoteza njia yake isipokuwa wale tu wanaofuata maamuzi na hukumu zao wenyewe badala ya mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa waziwazi. **{SCsw 89.2}**

Hatupaswi kuchukua ushuhuda wa mtu yeyote kuhusu kile ambacho Maandiko Matakatifu yanafundisha, bali tunapaswa kujifunza Maneno ya Mungu kwa ajili yetu wenyewe. Tukiruhusu wengine kufikiri kwa niaba yetu, tutakuwa na nguvu dhaifu, na zenye ulemavu na misuli ya kiroho iliyosinyaa na kugangamaa. Nguvu bora na tukufu za akili zinaweza kuwa mbilikimo kwa ukosefu wa mazoezi kwenye mada zinazostahili umakini, kiasi cha kupoteza uwezo wake wa kuelewa maana ya kina ya Neno la

Mungu. Akili itakua ikitumika katika kufuatilia uhusiano wa mada za Biblia, kulinganisha Andiko na Andiko na mambo ya kiroho na mambo ya kiroho. **{SCsw 89.3}**

Hakuna kitu kingine kilichokorokotolewa/kilichoratibiwa kuimarisha akili kuliko kusoma Maandiko Matakatifu. Hakuna kitabu kingine chenye nguvu kama hicho cha kuinua mawazo, kutoa nguvu kwa vitivo, kama Ukweli mpana, bora na wa kuheshimika wa Biblia. Kama Neno la Mungu lingejifunzwa kama linavyopaswa, wanadamu wangekuwa na upana wa akili, ubora, utukufu wa tabia, na uthabiti wa kusudi unaoonekana kwa nadra sana katika nyakati hizi. **{SCsw 90.1}**

Lakini kuna faida ndogo tu inayopatikana kutokana na kusoma haraka Maandiko. Mtu mmoja anaweza kusoma Biblia nzima lakini akashindwa kuona uzuri wake au kuelewa maana yake ya kina na iliyofichwa. Fungu moja la Maandiko linalosomwa hadi umuhimu wake uwe wazi kwenye akili na uhusiano wake na mpango wa wokovu uonekane, lina thamani zaidi kuliko kusoma sura nyingi bila kusudi dhahiri na pasipo mafundisho chanya yanayopatikana. Kaa na Biblia yako. Unapopata fursa, isome; weka Maandiko katika kumbukumbu yako-kariri Maandiko. Hata unapotembea mitaani unaweza kusoma ibara au fungu na kutafakari juu yake, ndivyo unavyoweza kuiweka akilini. **{SCsw 90.2} [D nne za kukariri Maandiko- Desire Determination Discipline and Divine help, Tamani, Amua, Nidhamu na Msaada wa Mungu]**

Hatuwezi kupata hekima bila umakini wa dhati, na bidii katika kujifunza kwa maombi. Baadhi ya sehemu za Maandiko, hakika ziko wazi kupita kiasi cha kutoweza kutiliwa shaka, lakini kuna zingine ambazo maana yake haionekani kwa haraka. Maandiko lazima yalinganishwe na Maandiko. Lazima kuwe na utafiti wa makini na tafakari ya maombi. Na masomo kama haya yatazaa matunda mengi [yaani juhudi ya kuyasoma Maandiko kwa kicho na

kuyaishi, italipa sana katika maisha yetu hapa duniani na mbinguni (richly repay)]. Kama vile mchimbaji anavyogundua mifereji ya madini ya thamani iliyofichwa chini ya uso wa dunia, ndivyo yeye anayelichunguza Neno la Mungu bila kuchoka, kama hazina iliyofichwa itakavyopata Ukweli wa thamani kubwa zaidi, ambao umefichwa kutoka kwa macho ya mtafutaji mwenye bidii. Maneno yaliyovuviwa, yanayotafakariwa moyoni, yatakuwa kama vijito vinavyotiririka kutoka kwenye chemchemi ya uzima. **{SCsw 90.3}**

e cannot obtain wisdom without earnest attention and prayerful study. Some portions of Scripture are indeed too plain to be misunderstood, but there are others whose meaning does not lie on the surface to be seen at a glance. Scripture must be compared with scripture. There must be careful research and prayerful reflection. And such study will be richly repaid. As the miner discovers veins of precious metal concealed beneath the surface of the earth, so will he who perseveringly searches the word of God as for hid treasure find truths of the greatest value, which are concealed from the view of the careless seeker. The words of inspiration, pondered in the heart, will be as streams flowing from the fountain of life.

Never should the Bible be studied without prayer. Before opening its

Biblia haipaswi kamwe kusomwa bila maombi. Kabla ya kufungua kurasa zake tunapaswa kuomba nuru ya Roho Mtakatifu, nayo itatolewa. Nathanaeli alipomjia Yesu, Mwokozi alisema, "***Tazama, Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake. Nathanaeli akamwambia, Umepataje kunitambua? Yesu akajibu, akamwambia, Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini nilikuona.*** **Yohana 1:47-48** Naye Yesu atatuona nasi pia katika sehemu za siri za maombi, ikiwa tutamtafuta kwa ajili ya nuru ili tujue Ukweli ni nini. Malaika kutoka ulimwengu wa nuru watakuwa pamoja na wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo wanatafuta mwongozo wa Mwenyezi Mungu (mbingu). **{SCsw 91.1}**

Roho Mtakatifu humwinua na kumtukuza Mwokozi. Ni kazi Yake kumwasilisha Kristo, katika usafi wa haki Yake, na wokovu mkuu tulio nao kupitia Yeye. Yesu anasema, "***Yeye atanitukuza Mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo Yangu na kuwapasha habari***" **Yohana 16:14**. Roho wa Kweli Ndiye mwalimu pekee wa Ukweli, anayefaa na wa Kiungu/mbinguni. Jinsi Mungu anavyoithamini jamii ya wanadamu, kwani alimtoa Mwanawe afe

kwa ajili ya wanadamu na kumteua Roho Wake kuwa Mwalimu wa mwanadamu na Kiongozi wa daima! {SCsw 91.2}

## SURA YA 11 - FURSA YA MAOMBI

### UPENDELEO WA MAOMBI

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa na uongozi Wake Bwana, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu huzungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; sisi tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake Yeye Bwana. Ili tuweze kuwa na uzima wa maisha ya kiroho na nguvu, ni lazima tuwe na ushirika na uhusiano halisi na Baba yetu wa mbinguni. Akili zetu zinaweza kuvutwa kumwelekea Yeye; tunaweza kutafakari kazi Zake, rehema Zake, baraka Zake; lakini hii sio kwa maana kamili, kuwa na ushirika Naye. Ili kuwasiliana na Mungu, ni lazima tuwe na kitu cha kumwambia Yeye kuhusu maisha yetu halisi-[yale yanayotendeka kila siku]. {SCsw 93.1}

Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni lazima kumjulisha Mungu, kuwa sisi tukoje au tulivyo, bali ili kutuwezesha kumpokea Yeye. Maombi hayamshushi Mungu chini, bali yanatunyanyua juu Kwake. {SCsw 93.2}

Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za Mungu, na kumtwika Yeye mahangaiko yao yote. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikilizwa na Yeye,

ni uhakikisho wetu pia. {SCsw 93.3}

Yesu Mwenyewe, alipokuwa akiishi miongoni mwa wanadamu, mara nyingi alikuwa katika maombi. Mwokozi wetu alijitambulisha na mahitaji na udhaifu wetu, katika hilo, Yeye akawa mwombaji, mtu Anayesihi kwa niaba yetu, akitafuta kutoka kwa Baba Yake nyongeza ya nguvu mpya, ili apate kwenda akiwa imara, mwenye utayari na aliyejiandaa kabisa, kwa ajili ya kazi, majukumu na majaribu. Yeye ni mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, "katika mambo yote alijaribiwa kama sisi;" lakini kama Yule asiye na dhambi, asili yake ilijiepusha na uovu; Alivumilia mapambano na mateso ya roho katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu Wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima, kipaumbele, upendeleo na fursa. Alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Na ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa Mungu, alihisi hitaji la maombi, Je, ni kwa kiasi gani, wanadamu wanyonge, dhaifu na wenye dhambi wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi ya bidii, yenye ari na ya kudumu. {SCsw 93.4}

Baba yetu wa mbinguni anatusubiri ili atupe ukamilifu wa baraka Zake. Ni fursa yetu kunywa kwa kiasi kikubwa, kwenye chemchemi ya upendo usio na mipaka. Inashangaza sana kwamba tunaomba kidogo sana! Mungu ameridhia na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya mtoto Wake aliye mnyenyekevu zaidi, na bado kuna kusita-sita sana kwa upande wetu, kumjulisha Mungu mahitaji/matakwa yetu. Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini kuhusu wanadamu dhaifu na maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa Mungu wa upendo usio na kifani, una shauku kwao, ukiwahitaji, na uko tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria, na bado wao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana? Malaika hupenda kusujudu mbele za Mungu; wanapenda kuwa karibu Naye. Huona ushirika na Mungu kama ndiyo furaha yao kuu; na bado

watoto wa dunia, ambao wanahitaji msaada tele, ambao Mungu pekee Ndiye anayeweza kutoa, wanaonekana kutosheka, kutembea bila nuru ya Roho Wake, kuandamana na uwepo Wake. **{SCsw 94.1}**

Giza la yule mwovu huwafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya adui yanayonong'oneza, huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii upendeleo ambao Mungu amewapa katika miadi na Mungu katika maombi. Kwa nini wana na binti za Mungu wasitake kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala la mbinguni, ambapo hazina zisizo na kikomo za Mwenyezi Mungu zimehifadhiwa? Bila maombi yasiyokoma na (kukesha) maombi yasiyochoka, na ya bidii, tuko katika hatari ya kuwa wazembe na kupotoka kutoka kwenye njia sahihi. Adui anatafuta daima kufunga njia ya kwenda kwenye kiti cha rehema, ili tusipate neema na nguvu za kupinga majaribu kwa bidii, kwa maombi na imani. **{SCsw 94.2}**

Kuna masharti fulani ambayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kuyajibu maombi yetu. Mojawapo ya haya ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Yeye Ameahidi, ***"Kwa maana nitamimina maji juu yake aliye na kiu, na vijito vya maji juu ya mahali pakavu.*** **Isaya 44:3** Wale wenye njaa na kiu ya haki, wenye matamanio na Mungu (wenye shauku na Mungu), wanaweza kuwa na uhakika kwamba watajazwa-watashibishwa. Moyo lazima uwe wazi kwa ushawishi wa Roho, la sivyo baraka za Mungu haziwezi kupokelewa. **{SCsw 95.1}**

Haja yetu kuu yenyewe, ni hoja tosha na inasihi kwa kujieleza kwa umbuji/ufasaha zaidi kwa niaba yetu. Lakini Bwana anapaswa kutafutwa ili afanye haya mambo kwa niaba yetu. Bwana Anasema, ***ombeni, nanyi mtapewa; Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?*** **Mathayo 7:7, Warumi**

8:32 {SCsw 95.2}

Tukiendekeza au kuzingatia uovu mioyoni mwetu, tukishikilia/tukishikamana na dhambi yoyote inayojulikana, Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu, na kukiri hukubaliwa daima. Wakati makosa yote yanayojulikana yanaporekebishwa, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu. Haki na Sifa zetu wenyewe hazitatufanya kamwe "tukubaliwe na Mungu; ni haki na sifa ya Yesu tu, ndiyo ambazo" zitatuokoa, damu Yake itatusafisha; lakini tuna kazi ya kufanya kwa kuzingatia masharti ya kukubalika. {SCsw 95.3}

Kipengele kingine cha maombi yanayoshinda, na yanayoendana na mapenzi ya Mungu na yasiyochoka ni Imani ***"kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Waebrania 11:6, Marko 11:24"*** Je, tunamkubali na kumwendea Bwana  kama asemavyo, katika Neno Lake? {SCsw 96.1}

Uhakikisho ni mpana na hauna kikomo, na Yeye Aliye Mwaminifu ambaye ameahidi, atatenda. Tusipopokea mambo bainishi tuliyoomba, wakati tunapoomba, bado tunapaswa kuamini. Sisi ni wakosefu sana na hivyo hatuoni mbali kiasi kwamba, wakati mwingine huwa tunaomba mambo ambayo hayatakuwa baraka kwetu, na Baba yetu wa mbinguni kwa upendo, hujibu maombi yetu kwa kutupa kile ambacho kitakuwa kwa faida yetu kuu zaidi—kile ambacho sisi wenyewe tungetamani tukipate, ikiwa tungeangaziwa na maono yenye nuru ya Kiungu na kuweza kuona mambo yote kama yalivyo kweli.  Wakati maombi yetu yanapoonekana kutojibiwa, tunapaswa kuishika ahadi kwa kuing'ang'ania; kwani wakati wa kujibiwa hakika utakuja, na tutapokea baraka tunayohitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi yetu daima yatajibiwa kwa njia ileile tuliyotaka na kwa jambo fulani

maalum tunalotamani na kuomba, ni dhana/ujuvi tu (presumption). Mungu ni Mwenye hekima sana, hata asiweze kamwe kukosea, na ni mwema sana, hata asiweze kuwanyima kitu chochote chema wale wanaotembea kwa unyoofu. Basi usiogope kumwamini Bwana, ingawa hauoni majibu ya haraka kwa maombi yako. Tegemea ahadi Yake ya uhakika, "Ombeni, nanyi mtapewa." **{SCsw 96.2}**

Tukiruhusu mashaka na hofu zetu kutushauri na kutuongoza, kwamba zijaribu kutatua kila tatizo au kitu ambacho hatuwezi kukiona waziwazi, kabla hatujawa na imani, matatizo yataongezeka tu na kuzidi kuwa makubwa. Lakini tukimjia Mungu, tukihisi hatuna msaada na tegemezi, kama tulivyo, na kwa imani ya unyenyekevu na ya kumtumaini, tunamjulisha Yeye ambaye ujuzi Wake hauna kikomo, ambaye anaona kila kitu katika uumbaji, na anayetawala kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, Anaweza na Atasikiliza kilio chetu, na Ataacha nuru iangaze mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati tunaunganishwa na akili isiyo na ukomo. Huenda tusiwe na ushahidi wa ajabu wakati huo kwamba uso wa Mkombozi wetu unainama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini hata hivyo, ndivyo ilivyo. Huenda tusihisi mguso Wake unaoonekana na kuhisiwa, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo, sikitiko na huruma nyororo, na kujali. **{SCsw 96.3}**

Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa Mungu tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha mioyoni mwetu. Tunawezaje kuomba, ***“utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu”*** wakati bado tuna roho ya kutosamehe? **Mathayo 6:12**. Tukitarajia maombi yetu yasikilizwe, ni lazima tuwasamehe wengine kwa njia ile ile na kwa upana/kiwango kile kile tunachotumaini kusamehewa. **{SCsw 97.1}**

Uvumilivu katika maombi umefanywa kuwa sharti la kupokea. Lazima tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu. Tunapaswa kuwa “wenye kukesha ***katika kusali, Dumuni***

***sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani;*** **Warumi 12:12, Wakolosai 4:2.** Petro anawasihi waumini kuwa ***iweni na akili, mkeshe katika sala. 1 Petro 4:7*** Paulo anaelekeza, ***bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Wafilipi 4:6***. "Lakini ninyi, wapenzi," Yuda anasema, ***na kuomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu. Yuda 1:20-21.*** Maombi yasiyokoma ni muungano usiovunjika wa roho na Mungu, ili uhai kutoka kwa Mungu utiririke katika maisha yetu; na kutoka kwenye maisha yetu, usafi na utakatifu utiririke kwa Mungu. {SCsw 97.2}

Kuna ulazima wa bidii na uadilifu katika maombi; hebu usiruhusu chochote kikuzuie. Fanya kila juhudi kuweka wazi ushirika kati ya Yesu na nafsi yako. Tafuta kila fursa ya kwenda mahali ambapo maombi yamezoeleka kufanywa. Wale wanaotafuta ushirika na Mungu wataonekana katika mkutano wa maombi, wakiwa waaminifu kufanya wajibu wao na wenye bidii na hamu ya kuvuna faida zote wanazoweza kupata. Wataboresha kila fursa ya kujiweka mahali ambapo wanaweza kupokea miale ya nuru kutoka mbinguni. {SCsw 98.1}

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwani haya ndiyo uzima wa nafsi. Haiwezekani roho kustawi huku maombi ya faragha yamepuuzwa. Sala ya familia au ya hadharani pekee yake haitoshi. Katika upweke ruhusu roho yako inanikwe wazi kwa jicho la ukaguzi la Mungu linalochunguza. Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa na Mungu tu, anayesikia maombi. Hakuna sikio la udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi kama hayo. Katika maombi ya siri, nafsi inakuwa huru kutokana na ushawishi unaoizunguka, huru dhidi ya msisimko. Kwa utulivu, lakini kwa bidii, yatamfikia Mungu. Mvuto utakaotoka Kwake Yeye aonaye sirini, utakuwa mzuri na wa kudumu, Yeye ambaye sikio Lake liko wazi kusikia maombi yanayotoka moyoni. Kwa imani tulivu na iliyo

sahili, roho hushirikiana na Mungu na kukusanya miale ya nuru ya Bwana ili kuiimarisha na kuitegemeza katika pambano na Shetani. Mungu Ndiye ngome yetu ya nguvu. **{SCsw 98.2}**

Omba chumbani kwako, na unapoendelea na kazi yako ya kila siku ruhusu moyo wako uinuliwe juu kwa Mungu, mara nyingi. Ndivyo Henoko alivyotembea na Mungu. Maombi haya ya kimya-kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yeye ambaye moyo wake umesimama na kujitegemeza kwa Mungu. **{SCsw 98.2}**

Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa Mungu. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu kwa roho ya maombi ya dhati. Katika umati wa watu barabarani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kuomba mwongozo wa Bwana, kama Nehemia alivyofanya alipoomba mbele ya Mfalme Artashasta. Chumba cha ushirika kinaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuendelea kuacha mlango wa moyo ukiwa wazi kila wakati na mwaliko wetu ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje, na kukaa ndani ya moyo kama mgeni wa mbinguni katika nafsi. **{SCsw 99.1}**

Ingawa kunaweza kuwa na mazingira machafu na yaliyoharibika yanayotuzunguka, hatuhitaji kupumua hewa yake chafu, na yenye harufu mbaya, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango kwa fikra chafu na mawazo yasiyo matakatifu kwa kuinua roho mbele za Mungu kupitia maombi ya dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea usaidizi na baraka za Mungu watatembea katika angahewa takatifu zaidi kuliko ile ya dunia na watakuwa na ushirika wa kudumu na mbingu. **{SCsw 99.2}**

Tunahitaji kuwa na mitazamo na maoni dhahiri, na bainishi zaidi kuhusu Yesu na ufahamu kamili wa thamani wa uhalisia wa milele. Uzuri wa utakatifu unapaswa kuijaza mioyo ya watoto wa

Mungu; na ili hili liweze kutimizwa, tunapaswa kutafuta mafunuo ya Bwana yahusuyo mambo ya mbinguni. {SCsw 99.3}

Hebu nafsi ivutwe nje na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya angahewa ya mbinguni. Tunaweza kukaa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotazamiwa, mawazo yetu yatamgeukia Yeye kama asili, yaani kama kawaida ya ua linavyoligeukia jua (phototropism). {SCsw 99.4}

Weka matakwa yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu. Huwezi kumlemea Bwana; huwezi kumchosha Mwenyezi Mungu. Yeye ahesabuye nywele za kichwa chako hayupo kinyume cha matakwa ya watoto Wake. ***"Bwana ni mwingi wa rehema, Mwenye huruma."*** **Yakobo 5:11** Moyo Wake wa upendo huguswa na huzuni zetu na hata na matamshi yetu. Mpelekee Bwana kila kitu kinachosumbua akili. Hakuna kitu kikubwa sana Kwake kukibeba, kwa maana Yeye hushikilia ulimwengu, Anatawala mambo yote ya ulimwengu. Hakuna kitu ambacho kwa namna yoyote kinahusu amani yetu ambacho ni kidogo sana Kwake kukiona. Hakuna sura katika uzoefu wetu iliyo giza sana Kwake kusoma; hakuna mkanganyiko ambao ni mgumu sana Kwake kuutatua. Hakuna msiba unaoweza kumpata hata mmoja wa watoto Wake wadogo, hakuna wasiwasi unaosumbua roho, hakuna furaha ya furaha, hakuna sala ya dhati inayotoka midomoni, ambayo Baba yetu wa mbinguni haoni, au ambayo hataonyesha kujali mara moja (upesi). Yeye ***"Huwaponya waliopondeka moyo, Na kuziganga jeraha zao. Zaburi 147:3.*** Mahusiano kati ya Mungu na kila mtu ni bainishi na dhahiri, nayo yamesheni kana kwamba hakuna nafsi nyingine duniani, inayoshiriki uangalizi Wake, hakuna roho nyingine kwa ajili yake ambayo Yeye alimtoa Mwanawe mpendwa. {SCsw 100.1}

Yesu alisema, ***"mtaomba kwa Jina Langu, wala siwaambii ya kwamba Mimi nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe awapenda kwa kuwa ninyi mmenipenda Mimi, na***

***kusadiki ya kwamba Mimi nalitoka kwa Baba-bali ni Mimi niliyewachagua ninyi; Nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa Jina Langu awapeni.*****Yohana 16:26-27, 15:16** Lakini kuomba katika Jina la Yesu ni zaidi ya kutaja tu Jina hilo mwanzoni na mwisho wa sala. Ni kuomba katika akili na roho ya Yesu, huku tukiamini ahadi Zake, tukitegemea neema Yake, na kutenda kazi Zake. **{SCsw 100.2}**

Mungu hamaanishi kwamba yeyote kati yetu awe mtawa au awaepe watu kwa kujitenga na ulimwengu, ili kujitoa wakfu kwa matendo na shuguli za ibada. Maisha lazima yawe kama maisha ya Kristo—kati ya mlima na umati. Yeye ambaye hafanyi chochote isipokuwa kuomba, hivi karibuni ataacha kuomba, au vinginevyo maombi yake yatakuwa ya kaida na ratiba tu. Wanadamu wanapojiondoa katika maisha ya kijamii, mbali na nyanja ya wajibu wa Kikristo na kubeba msalaba; wanapoacha kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Bwana, aliyewafanyia kazi kwa bidii, wanapoteza mada ya maombi na hawana motisha wa ibada au kujiweka wakfu. Maombi yao huwa yanawahusu wao tu na ya ubinafsi. Hawawezi kuomba kuhusu matakwa ya ubinadamu au ujenzi wa ufalme wa Kristo, hawataomba nguvu ya kufanya kazi ya Bwana. **{SCsw 101.1}**

Tunajipatia hasara kwa kuzembea kuchangamkia fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo na wenzetu, katika kumtumikia Mungu-[huduma kwa kazi ya Mungu]. Kweli za Neno Lake Bwana hupoteza uwazi, picha zenye hisia na kumbukumbuku angavu, uhai na umuhimu wake katika bongo zetu. Mioyo yetu inaacha kuangazwa na kuzinduliwa kwa ushawishi ule unaotakasa, na tunashuka kwenda chini katika hali mionjo ya kiroho. Katika ushirikiano wetu kama Wakristo, tunapoteza mengi kwa kukosa huruma kwa kila mmoja wetu. Yeye anayejifungia mwenyewe, huwa hajazi nafasi ambayo Mungu alikusudia

kuitimiza. Ukuzaji sahihi wa vipengele vya kijamii katika asili yetu hutuleta katika huruma na wengine na ni njia ya maendeleo na nguvu kwetu katika huduma/utumishi wa Mungu. **{SCsw 101.2}**

Ikiwa Wakristo wangeshirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Ukweli wa thamani wa ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa kwa kufanywa upya na wao kwa wao wenyewe pia wangewasaidia wenzao kuburudishwa, na kufanywa upya. Tunaweza kujifunza zaidi kuhusu Baba yetu wa mbinguni kila siku, tukipata uzoefu mpya wa neema Yake; ndipo tutatamani kuzungumza juu ya upendo Wake; na tunapofanya hivi, mioyo yetu wenyewe itapata joto-joto na kutiwa moyo. Kama tungewaza na kumzungumzia zaidi Yesu, badala yetu sisi wenyewe, tungekuwa na uwepo Wake tele zaidi. **{SCsw 101.3}**

Ikiwa tungemfikiria Mungu mara nyingi kadiri tunavyopata ushahidi wa ulinzi na utunzaji Wake kwetu, tungeweza kumweka Yeye katika mawazo yetu kila wakati na ndipo tutajikuta tunafurahia kuzungumza kumhusu Yeye na kumsifu. Tunazungumzia mambo ya kidunia yanayopita kwa sababu tunapendezwa nayo. Tunazungumzia kuhusu marafiki zetu kwa sababu tunawapenda; furaha na huzuni zetu zimefungana pamoja nao. Ila sisi tuna sababu kubwa zaidi ya kumpenda Mungu kuliko hata kuwapenda marafiki zetu wa kidunia; inapaswa kuwa jambo la kawaida zaidi duniani kumfanya Bwana awe wa kwanza katika mawazo yetu yote, kuzungumza kuhusu wema Wake na kusimulia nguvu Zake.

Zawadi nyingi za thamani, alizotupa Yeye, hazikukusudiwa kufyonza mawazo na upendo wetu kiasi kwamba tunakosa kitu chochote cha kumpa Mungu; hizi zawadi zinapaswa kutukumbusha kuhusu Yeye kila wakati na kutufunga katika vifungo vya upendo na moyo wa shukrani kwa Mfadhili wetu wa

mbinguni. Tunaishi karibu sana na nyanda za chini za dunia. Hebu na Tuyainue macho yetu kuelekea mlango ulio wazi wa Patakatifu pa juu mbinguni, ambapo nuru ya utukufu wa Mungu inang'aa kwenye uso wa Kristo, ambaye "aweza kuwaokoa kabisa" wote wanaomjia Mungu kwa Yeye. Waebrania 7:25. {SCsw 102.1}

Tunahitaji kumsifu Mungu zaidi ***"kwa fadhili Zake, na maajabu Yake kwa wanadamu.* Zaburi 107:8** Mazoezi yetu ya ibada hayapaswi kuhusisha kuomba na kupokea peke yake. Hebu tusiwe tunafikiria mahitaji/matakwa yetu tu daima, na kamwe tusifikirie maslahi/faida tunazopokea. Hatuombi sana, nasi tunaacha kutoa shukrani kwa Mungu. Sisi ndio "wapokeaji wa rehema za Mungu kila mara, na bado ni shukrani ndogo kiasi gani tunayoonyesha, ni mara chache kiasi gani, sisi tunamsifu Bwana kwa yale ambayo ametufanyia." {SCsw 102.2}

Hapo awali, Bwana aliwaagiza Israeli, walipokutana pamoja kwa ajili ya huduma Yake, "***mtakula mbele za Bwana, Mungu wenu, nanyi furahini katika yote mtakayotia mikono yenu, ninyi na wa nyumbani mwenu, aliyokubarikia Bwana, Mungu wako.* Kumbukumbu la Torati 12:7** Kile kinachofanywa kwa utukufu wa Mungu kinapaswa kufanywa kwa furaha, kwa nyimbo za sifa na shukrani, sio kwa huzuni, masikitiko na uchungu. {SCsw 103.1}

Mungu wetu ni Baba mpole, Mwenye mapenzi, anayejali na Mwenye huruma nyororo. Huduma Yake haipaswi kuchukuliwa kama zoezi gumu la kuhenyesha na la kusononesha moyo na kuleta msongo. Inapaswa kuwa furaha kumwabudu Bwana na kushiriki katika kazi Yake. Mungu hangetaka watoto Wake, ambao wokovu mkuu umetolewa kwao, watende kana kwamba Yeye ni msimamizi mgumu, mnyapara mkali, asiye na huruma, Mwenye kutubebesha majukumu mazito. Yeye Ndiye rafiki yetu/yao mkubwa; na tunapomwabudu, Yeye anatazamia kuwa pamoja nasi, kutubariki na kutufariji, akiijaza mioyo yetu kwa furaha na upendo. Bwana anatamani watoto Wake tufarijike katika huduma Yake na

kupata raha zaidi, kuliko shida na ugumu katika kazi Yake. Yeye Anatamani kwamba wale tunaokuja kumwabudu Yeye, tutarudi tukiwa na mawazo ya thamani ya ulinzi, utunzaji na upendo Wake, ili tuweze kuchangamshwa na kushangilia katika shuguli zote za maisha ya kila siku, ili tupate neema ya kutenda kwa uadilifu/kiukweli na uaminifu katika mambo yote. **{SCsw 103.2}**

Ni lazima tukusanyike kuzunguka msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa anapaswa kuwa mada ya kutafakari, mazungumzo, na hisia zetu za furaha na shangwe zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu, kumbukumbu ya kila baraka tunayopokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini, kwa kuweka kila kitu kwenye ule mkono uliopigiliwa misumari msalabani kwa ajili yetu.**{SCsw 103.3}**

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mabawa ya sifa. Mungu anaabudiwa kwa wimbo na muziki katika makao ya juu, na tunapoonyesha shukrani zetu, basi tunakaribia ibada ya majeshi ya mbinguni. ***"Atoaye dhabihu za kushukuru, Ndiye anayenitukuza. kushukuru, na sauti ya kuimba. Zaburi 50:23, Isaya 51:3*** **{SCsw 104.1}**

## SURA YA 12 – NINI KIFANYIKE KUHUSU MASHAKA

Wengi, hasa wale walio wachanga bado, katika maisha ya Kikristo, wakati mwingine husumbuliwa na mapendekezo ya kutilia shaka (skepticism). Wana mambo mengi ambayo wanashindwa kuyaelezea ndani ya Biblia au hata kuyaelewa, na Shetani hutumia haya kutikisa imani yao katika Maandiko, kwamba Je, ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Wanauliza, "Nitajuaje njia sahihi? Ikiwa Biblia kweli ni Neno la Mungu, ninawezaje kuwekwa huru kutokana na mashaka na misukosuko hii?" **{SCsw 105.1}**

Mungu hajawahi kututaka/kutuomba tuamini, bila kutoa ushahidi wa kutosha ambao tunapaswa kutegemeza imani yetu katika huo msingi. Uwepo Wake, tabia Yake, Ukweli wa Neno Lake, vyote vimethibitishwa na ushuhuda unaovutia, kwa akili zetu; na ushuhuda huu ni tele-mwingi. Lakini Mungu hajawahi kuondoa uwezekano wa shaka-[au mtu kutilia shaka kwani siyo kuona kwa macho bali ni kumtumaini Mungu kulingana na tabia Yake, si kwa kuhitaji uthibitisho au ishara kabla ya kuamini.]. Imani yetu lazima itegemee ushahidi, na sio uthibitisho. Wale wanaotaka kutilia shaka watapata fursa hiyo; huku wale wanaotaka kweli kujua, Ukweli watapata ushahidi mwingi wa kuipumzisha imani yao katika msingi huo. {SCsw 105.2}

Haiwezekani kwa akili zenye mipaka au ukomo kuelewa kikamilifu tabia au kazi za Yule Asiye na Mwisho. Hata kwa akili iliyo makini zaidi, na iliyoelimika zaidi, Nafsi hii Takatifu ya Mungu, lazima ibaki ikiwa imevikwa kwa fumbo na siri. **"Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? Waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi? Ni juu mno kama mbingu; waweza kufanya nini wewe? Ni wenye kina kuliko kuzimuni; waweza kujua nini wewe? Ayubu 11:7-8** {SCsw 105.3}

Mtume Paulo anapaza sauti yake kwa kushangilia ghafla, akisema, **"Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu Zake hazichunguziki, wala njia Zake hazitafutikani! Warumi 11:33.** Lakini ingawa ***"Mawingu na giza vyamzunguka, Haki na hukumu ndio msingi wa kiti Chake." Zaburi 97:2.*** Tunaweza kuelewa kwa kiasi fulani tu, kama wanadamu, namna Bwana anavyotutendea na kuchukuliana nasi, na nia ambazo ndiyo kigezo anachokitumia, ili tuweze kutambua upendo, huruma na rehema zisizo na ukomo/mipaka zilizounganishwa na nguvu zisizo na kikomo. Tunaweza kuelewa makusudi Yake mengi kama vile ilivyo, kwa faida yetu wenyewe, kujua; na zaidi ya haya yote, ambayo sisi kama wanadamu tunayajua, bado, tunapaswa

kuuamini mkono wenye nguvu zote, na moyo uliojaa upendo (hata pale ambapo hatuelewi yote). **{SCsw 106.1}**

Neno la Mungu, kama tabia ya Mwandishi Wake wa Kiungu, linawasilisha mafumbo na siri ambazo haziwezi kueleweka kikamilifu na viumbe vyenye kikomo-mwisho. Kuingia kwa dhambi ulimwenguni, Kristo kufanyika mwili, kuzaliwa upya, ufufuo, na mada zingine nyingi zilizowasilishwa katika Biblia, ni mafumbo na siri zenye kina kirefu sana kwa akili ya mwanadamu kuelezea, au hata kuelewa kikamilifu. Lakini sisi hatuna sababu ya kutilia shaka Neno la Mungu, eti kwa sababu tu hatuwezi kuelewa mafumbo, siri za majaliwa, uongozi, na utunzaji Wake. Katika ulimwengu wa kawaida, tunazungukwa na mafumbo, vitendawili na siri ambazo hatuwezi kuzielewa, wala hata kujua kwa udogo maana ya mambo yanayoendelea. Maisha ya viumbe wanyenyekevu na wadogo au tunaowaona ni duni kabisa huleta utata ambao hata wanafalsafa wenye akili na busara nyingi zaidi hawana uwezo wa kuelezea (amoeba, bakteria, euglena nk). Kila mahali mbinguni na kwenye sayari zote, kuna maajabu zaidi ya ufahamu wetu. Je, basi, ni jambo la ajabu kwetu pale tunapogundua kwamba katika ulimwengu wa kiroho pia kuna siri ambazo ziko nje kabisa ya uwezo wetu kuzielewa? Ugumu huu, upo tu katika udhaifu na ufinyu wa akili ya mwanadamu. Mungu ametupa ushahidi wa kutosha katika Maandiko kuhusu tabia ya Kiungu, naam tabia Yake Mwenyewe, nasi hatupaswi kutilia shaka Neno Lake kwa sababu tu, hatujaweza kuzielewa siri zote za majaliwa Yake-[Majaliwa/Providence-Ukuu Wake wenye shughuli nyingi, umakini ambao Mungu hutegemeza, hutunza, huruzuku, hutawala, huongoza, na kusimamia viumbe Vyake wote, katika sayari zote—ikiwa ni pamoja na chaguzi za wanadamu na matukio ya asili—ili kutimiza makusudi Yake makuu na mema.] **{SCsw 106.2}**

Mtume Petro anatuhamasisha kwa kusema kwamba katika Maandiko kuna ***“mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na***

***mambo hayo ambayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na Maandiko mengine, na kujiletea maangamivu yao wenyewe.*** **2 Petro 3:16.** Ugumu wa Maandiko umeanishwa na watu wenye shaka kama hoja dhidi ya Biblia; lakini mbali na hili, jambo hili la ugumu wa Maandiko, hakika ndilo linanaunda ushahidi thabiti wa uvuvio Wake wa Kiungu (mbingu). Endapo Maandiko yasingehusisha maajabu ya Mungu ila yale ambayo tunaweza kuyaelewa kwa urahisi; kama ukuu na utukufu Wake ungeweza kueleweka na akili zetu zenye mipaka au ukomo, basi Biblia isingekuwa na sifa zisizo na shaka, za mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Ukuu na mafumbo, na siri ya mada zinazowasilishwa zinapaswa kuhamasisha imani ndani yake kama hakika, hili ndilo Neno la Mungu. **{SCsw 107.1}**

Biblia hufunua Ukweli kwa usahili kabisa na kuratibiwa kikamilifu kwa mahitaji na matamanio ya moyo wa mwanadamu, ambayo yameshangaza na kuvutia akili zilizokuzwa, zilizoelimishwa na kusafishwa (cultured mind), huku ikiwawezesha watu wanyenyekevu, wasio na visomo vikubwa na wasio na utamaduni kutambua njia ya wokovu. Na bado, hizi Kweli zilizotamkwa kwa urahisi zinashikilia mada zilizoinuliwa juu sana, zenye upana unaofika mbali, na zisizo na kikomo, zaidi ya uwezo wa ufahamu wa mwanadamu, kiasi kwamba sisi tunaweza kuzikubali tu kwa sababu Mungu Mwenyewe amezitangaza. Hivyo mpango wa ukombozi umefunuliwa kwetu, ili kila mwanadamu, aweze kuona hatua anazopaswa kuchukua katika toba kwa Mungu na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ili aweze kuokolewa kwa njia ambayo Mungu ameiweka; lakini chini ya Kweli hizi, ambazo zinaeleweka kwa urahisi, ziko siri na mafumbo ya utukufu Wake ambayo yamesitirika—mafumbo na siri zinazoizidi akili ya mwanadamu kwa nguvu, katika utafiti wake, lakini Yeye humvuvia na kumtia moyo mtafutaji wa ile Kweli kwa kicho na imani. Kadiri mwanadamu anavyochunguza Biblia, ndivyo anavyozidi

kusadikishwa zaidi, na imani inayokua, kwamba hili ni Neno la Mungu aliye hai, na ndipo akili ya mwanadamu inainama na kuabudu mbele ya ukuu wa ufunuo wa Mungu. {SCsw 107.2}

Kukubali kwamba sisi hatuwezi kuelewa kikamilifu Ukweli mkuu wa Biblia ni kukubali tu kwamba akili yetu yenye ukomo ni finyu kuelewa umilele au kile kisicho na ukomo; kwamba mwanadamu, kwa ujuzi wake mdogo wa kianadamu, hawezi kuelewa madhumuni ya Yule Mwenye Ujuzi Wote. {SCsw 108.1}

Kwa sababu hawawezi kuelewa mafumbo na siri zake zote, watu wenye shaka na wakana-Mungu wanakataa Neno la Mungu; na si wote wanaodai kuiamini Biblia wako huru kutokana na hatari katika jambo hili. Mtume anasema, "***Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Waebrania 3:12.*** Ni sawa kujifunza mafundisho ya Biblia kwa makini na kuchunguza "mambo ya ndani ya Mungu" kadiri yanavyofunuliwa katika Maandiko. ***Mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. 1 Wakorintho 2:10-11***. Ingawa "***mambo ya siri ni ya Bwana Mungu wetu," "Mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi- Kumbukumbu la Torati 29:29*** Lakini ni kazi ya Shetani kupotosha nguvu za akili katika uchunguzi na utafiti. Kiburi fulani huchanganywa na kuakisi Ukweli wa Biblia, ili watu wahisi kukosa subira na kushindwa, kwamba hawawezi kuelezea kila sehemu ya Maandiko kwa kiasi cha kujiridhisha, au watu kuridhika. Ni aibu sana kwao kukubali kwamba hawayaelewi maneno yaliyovuviwa na Roho Mtakatifu. Wanadamu hawako tayari kusubiri kwa uvumilivu hadi Mungu atakapoona inafaa kuwafunulia kwao Ukweli. Wanahisi kwamba hekima yao ya kianadamu isiyo na usaidizi, inatosha kuwawezesha kuelewa Maandiko, na wanaposhindwa kuelewa, wanakana mamlaka Yake. Ni kweli kwamba nadharia nyingi na mafundisho mengi, yanayopendwa na maarufu, na yanayodhaniwa kuwa yanatokana na Biblia, kwa kweli hayana msingi katika mafundisho yake, na

kwa hakika, yapo kinyume na msingi mzima wa uvuvio. Mambo haya yamekuwa chanzo cha shaka na mkanganyiko, kwa akili nyingi. Hata hivyo, Neno la Mungu haliwezi kushtakiwa kwa kuwajibika na chanzo cha watu kuwa na mashaka, bali hili limetokana na upotoshaji wa mwanadamu. **{SCsw 108.2}**

Kama ingewezekana kwa viumbe vilivyoumbwa kufikia uelewa kamili wa Mungu na kazi Zake, basi, baada ya kufikia hatua hii, hakungekuwa na ugunduzi zaidi wa ile Kweli, hakuna ukuaji katika maarifa ambao ungetokea, na kusingekuuweko maendeleo zaidi ya akili au moyo. Mungu hangekuwa Mkuu kupita nafsi yoyote duniani; na mwanadamu, baada ya kufikia kikomo cha maarifa na magoli aliyoweka ya mafanikio, angeacha kusonga mbele. Hebu na tumshukuru Mungu kwamba sivyo hivyo. Mungu hana mwisho; ndani Yake Yeye zimesitirika "hazina zote za hekima na maarifa." Wakolosai 2:3. Na kwa milele yote wanadamu wanaweza kuwa wakitafuta, wakijifunza, lakini hawatawahi kuimaliza hazina ya hekima Yake, wema Wake, na nguvu Zake. **{SCsw 109.1}**

Mungu anakusudia kwamba hata katika maisha haya, Ukweli wa Neno Lake utakuwa ukiendelea kufunuliwa kwa watu Wake. Kuna njia moja tu ambayo maarifa haya yanaweza kupatikana. Sisi tunaweza kufikia uelewa wa Neno la Mungu, kupitia mwangaza wa Roho Mtakatifu tu, ambaye Neno hilo lililetwa Naye. **“Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake?** Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. "***Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Kwa maana Roho huchunguza yote, naam, mambo ya ndani kabisa ya Mungu." 1 Wakorintho 2:11, 10.*** Na ahadi ya Mwokozi kwa wafuasi Wake ilikuwa, **"Lakini Yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awatie kwenye Kweli yote; kwa kuwa atatwaa**

**katika yaliyo Yangu na kuwapasha habari. Yohana 16:13-14** {SCsw 109.2}

Mungu anatamani mwanadamu atumie nguvu zake za kufikiri, na kupembua hoja (reasoning power); na kujifunza Biblia kutaimarisha na kuinua akili kuliko utafiti mwingine unavyoweza kufanya. Lakini tunapaswa kujihadhari na kuweka fikra, au upembuaji, au utafiti tunaoufanya uwe ndiyo mungu, kwani upembuaji, ukosoaji na udadavuaji wa fikra zetu unakabiliwa na udhaifu na unyonge wa mwanadamu (donot deify reasoning - upembuaji, ukosoaji na udadavuaji wa mwanadamu haufanyi kupembua hoja kuwa mungu). Kama tungetaka kuacha tabia ya kuyafunika Maandiko kwa ukungu ulio katika ufahamu wetu, ili Ukweli ulio wazi ueleweke, lazima tuwe na unyenyekevu na imani ya mtoto mdogo, tayari kujifunza, na kuomba msaada wa Roho Mtakatifu. Hisia ya nguvu na hekima ya Mungu, na kutoweza kwetu kuelewa ukuu Wake, inapaswa kutuvuvia moyo kwa unyenyekevu, nasi tunapaswa kufungua Neno Lake, kama tunavyoingia mbele Zake, kwa hofu takatifu. Tunapokuja kwenye Biblia, fikra za kupembua, kudadavua, na kukosoa (reason) lazima ikubali mamlaka iliyo juu yake, na moyo na akili lazima zimsujudie MIMI NIKO aliye mkuu. {SCsw 109.3}

Kuna mambo mengi ambayo yanaonekana kuwa magumu, yasiyoeleweka, na yamefunikwa na pazia, ambayo Mungu atayaweka wazi na kuwa rahisi kwa wale wanaotafuta kuyaelewa. Lakini bila mwongozo wa Roho Mtakatifu, tutaendelea kuwa na uwezekano wa kuyapotosha Maandiko daima, au kuyatafsiri vibaya. Kuna usomaji mwingi wa Biblia ambao hauna faida na katika visa vingi huleta majeraha kabisa. Neno la Mungu linapofunguliwa bila kicho na bila maombi; mawazo na mapenzi ya mtu yasipoelekezwa kwa Mungu, au kupatana na mapenzi Yake, akili hufunikwa na ukungu wa mashaka; na hata katika wakati wa kujifunza Biblia hiyo, mashaka huimarishwa. Adui huchukua

udhibiti wa mawazo, na anapendekeza tafsiri ambazo sio sahihi. Wakati wowote katika Neno na utendaji, wanadamu wasipotafuta kuwa na mapatano na Mungu, basi, hata kama wameelimika kwa kiasi cha juu namna gani, wataegemea kwenye upande wa kukosea katika uelewa wao wa Maandiko, na hakika sio salama kabisa, kwa mwanadamu yeyote kuamini maelezo yao. Wale wanaoyasoma Maandiko ili kupata tofauti zilizomo au kutoafikiana, hawana uoni/ufahamu wa kiroho. Kwa maono yaliyopotoka wataona sababu nyingi za kutilia shaka na kutoamini mambo, ambayo ni rahisi na wazi kabisa kueleweka. {SCsw 110.1}

Hata kama inawekewa barakoa kiasi gani, ili hali halisi ifichwe, chanzo halisi cha shaka na kushuku au kutoamini Maandiko (doubt, skepticism, cynism or pessism), mara nyingi, ni kupenda dhambi. Mafundisho, makatazo na vizuizi vya Neno la Mungu havikaribishwi kwenye moyo wenye kiburi, unaopenda dhambi, na wale ambao hawako tayari kutii matakwa yake, hakika watu kama hawa kwa kawaida, wako tayari kutilia shaka mamlaka yake. Ili kufikia Ukweli, ni lazima tuwe na hamu ya dhati ya kujua Ukweli na utayari wa moyo wa kuyatii. Na wote wanaokuja katika roho hii, ili kujifunza Biblia watapata ushahidi tele, kwamba hakika hili ni Neno la Mungu, na wanaweza kupata uelewa wa Ukweli Wake Bwana, ambao utawafanya wawe na hekima hata kufikia wokovu. {SCsw 111.1}

Kristo amesema, ***"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafunzo, Yohana 7:17***" Badala ya kuhoji na kulalamika, kukosoa, kupuuza kile ambacho hukielewi, zingatia nuru ambayo tayari inakuangazia, nawe utapokea nuru kubwa zaidi. Kwa neema ya Kristo, wewe tenda kila jukumu ambalo limewekwa wazi kwenye ufahamu wako, nawe utawezeshwa kuelewa na kutekeleza yale ambayo sasa una shaka nayo. {SCsw 111.2}

Kuna ushahidi ulio wazi kwa wote,—walioelimika sana, na

wasiojua kusoma na kuandika,—ushahidi wa uzoefu. Mungu anatualika tuthibitishe wenyewe Ukweli wa Neno Lake, Ukweli wa ahadi Zake. Yeye Anatuamuru kwa kuesma ***"Onjeni mwone ya kuwa Bwana Yu mwema; Heri mtu yule anayemtumaini". Zaburi 34:8.*** Badala ya kutegemea Neno la mwingine, tunapaswa kulionja sisi wenyewe. Anatangaza, "***ombeni, nanyi mtapata" Yohana 16:24.*** Ahadi Zake lazima zitatimizwa. Hazijawahi kushindwa; kamwe haziwezi kushindwa. Na tunapomkaribia Yesu, na kufurahi katika ukamilifu wa upendo Wake, mashaka yetu na giza vitatoweka katika mwangaza wa uwepo Wake. {SCsw 111.3}

Mtume Paulo anasema kwamba Mungu ***"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo Lake; Wakolosai 1:13."*** Na kila mtu aliyepita kutoka mautini na kuingia uzimani anaweza kuwa "***ametia muhuri ya kwamba Mungu ni Kweli" Yohana 3:33*** mtu huyu anaweza kushuhudia, "Nilihitaji msaada, nami nikaupata katika Yesu. Kila hitaji lilitimizwa, kila upungufu ulijazwa, njaa ya roho yangu ilitoshelezwa; na sasa Biblia kwangu ni ufunuo wa Yesu Kristo. Unauliza kwa nini ninamwamini Yesu? Kwa sababu Yeye ni Mwokozi wangu. Kwa nini ninaamini Biblia? Kwa sababu nimeiona kuwa ni sauti ya Mungu kwa roho yangu." Tunaweza kuwa na ushuhuda ndani yetu kwamba Biblia ni ya Kweli, kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu. Tunajua kwamba hatufuati hekaya zilizobuniwa/zilizotungwa kwa ujanja. {SCsw 112.1}

Petro anawasihi ndugu zake ***"kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo" 2 Petro 3:18*** Watu wa Mungu wanapokua katika neema, wataendelea kupata/kupewa uelewa wazi zaidi wa Neno Lake kila mara. Watatambua nuru mpya na uzuri katika Ukweli Wake mtakatifu. Hili limekuwa kweli katika historia ya kanisa katika Zama/vizazi vyote, na hivyo litaendelea hadi mwisho wa wakati katika dunia hii. ***"Bali njia ya wenye haki ni kama nuru ing'aayo, Ikizidi kung'aa hata mchana***

***mkamilifu. Mithali 4:18"*** {SCsw 112.2}

Kwa imani tunaweza kutazama maisha ya baadaye, kule mbinguni, na kuishika ahadi ya Mungu kwa bidii, kwa ajili ya ukuaji wa akili kwa makini na nguvu (grasp), vitivo vya ubinadamu unaoungana na Uungu, na kila nguvu ya roho inapogusana moja kwa moja na Chanzo cha nuru. Tunaweza kufurahi kwamba yote yaliyotukang'anya katika uongozi, ukuu, utunzaji na majaliwa ya Mungu yatawekwa wazi, mambo magumu kueleweka, yatapata maelezo; na pale ambapo akili zetu zenye kikomo ziligundua mkanganyiko na makusudi yaliyovunjika-vunjika vipande tu, tutaona upatanifu na maelewano kamili na mazuri. ***"Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. 1 Wakorintho 13:12*** {SCsw 112.3}

## SURA YA 13 - KUFURAHI KATIKA BWANA

Watoto wa Mungu wameitwa kuwa wawakilishi wa Kristo, wakionyesha wema na rehema ya Bwana. Kama jinsi Yesu alivyotufunulia tabia ya Kweli ya Baba, vivyo hivyo tunapaswa kumfunua Kristo kwa ulimwengu usiojua upendo Wake na huruma Yake nyororo yenye kutusikitikia sisi wanadamu. "Kama ulivyonituma ulimwenguni," alisema Yesu, "vivyo hivyo mimi pia niliwatuma ulimwenguni." "**Mimi ndani yao, nawe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda Mimi. Yohana 17:18, 23.** Mtume Paulo anawaambia wanafunzi wa Yesu, ***"mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo inayojulikana na kusomwa na watu wote 2 Wakorintho 3:3, 2*** Kwa kila mmoja wa watoto Wake, Yesu anatuma barua kwa ulimwengu. Kama wewe ni mfuasi wa Kristo, Yeye anakutumia barua kwenye

familia, kijiji, na barabara ile unayoishi. Kuishi na Yesu ndani yako (kupitia Roho Mtakatifu) kunakufanya utamani kuzungumza na mioyo ya wale watu ambao hawamfahamu. Labda hawasomi Biblia, au hawasikii sauti inayozungumza nao katika kurasa zake; hawaoni upendo wa Mungu kupitia kazi Zake. Lakini ikiwa wewe ni mwakilishi wa kweli wa Yesu, huenda kupitia wewe watu wataongozwa kuelewa jambo fulani la wema Wake Bwana na kuongolewa, na hivyo kumpenda na kumtumikia. {SCsw 115.1}

Wakristo wamewekwa kama wabeba nuru walio safarini kwenda mbinguni. Wanapaswa kuakisi kwa ulimwengu nuru inayowaangazia, kutoka kwa Kristo. Maisha na tabia zao zinapaswa kuwa ya namna ambayo kupitia kwao wengine watapata dhana sahihi ya Kristo na huduma Yake. {SCsw 115.2}

Ikiwa tunamwakilisha Kristo, tutaifanya huduma Yake ionekane ya kuvutia, kama ilivyo kweli. Wakristo wanaokusanya simanzi na huzuni kwenye nafsi zao, na kunung'unika na kulalamika, wanawapa wengine uwakilishi wa uongo wa Mungu na maisha ya Kikristo. Wanatoa hisia kwamba Mungu hafurahi watoto Wake wakiwa na furaha, na katika kufanya hivi wanabeba ushuhuda wa uwongo dhidi ya Baba yetu wa mbinguni. {SCsw 116.1}

Shetani hushangilia anapoweza kuwaongoza watoto wa Mungu katika kutoamini na kukatishwa tamaa, na kukosa tumaini. Anafurahi anapotuona sisi wanadamu tukimshuku Mungu, na kutomtumaini Yeye, tukitilia shaka nia na nguvu Zake za kutuokoa. Adui anapenda kutufanya tuhisi kwamba Bwana atatudhuru kwa majaliwa na uongozi Yake. Ni kazi ya Shetani kumwakilisha Bwana kama Yule asiye na huruma na asiyewasikitikia wanadamu. Adui anauweka Ukweli kumhusu Mungu isivyo kabisa. Anayajaza mawazo na fikra za udanganyifu kumhusu Mungu; na badala ya kukaa juu ya Ukweli kumhusu Baba yetu wa mbinguni. Mara nyingi sisi wanadamu tunaweka akili zetu juu ya uwakilishi unaopotosha

wa Shetani na kutomwamini Mungu na kunung'unika dhidi Yake. Shetani hutafuta kila mara kufanya maisha ya kidini kuwa ya majonzi na huzuni. Adui anatamani maisha katika Kristo, yaonekane kuwa ni magumu na ya kuhenyesha; na Mkristo anapoishi katika mtindo wake wa maisha, mtazamo huu wa dini, yeye pia, kupitia kutoamini kwake, anaunga mkono uongo wa Shetani. {SCsw 116.2}

Wengi, wakitembea safarini, katika njia ya maisha, wanakaa katika makosa yao na kushindwa na kukatishwa tamaa, na mioyo yao imejaa majonzi na moyo kuhuzunika. Nilipokuwa Ulaya, dada mmoja ambaye alikuwa akifanya hivi, na ambaye alikuwa akihangaika kwa dhiki kubwa, aliniandikia, akiomba neno la kumtia moyo. Usiku uliofuata baada ya kusoma barua yake niliota ndoto kwamba nilikuwa kwenye bustani, na Mmoja ambaye alionekana kuwa mmiliki wa bustani alikuwa akiniongoza katika ziara, kupitia njia za hii bustani. Nilikuwa nikikusanya maua na kufurahia harufu yake, wakati dada huyu, ambaye alikuwa akitembea kando yangu, alipoelekeza umakini wangu kwenye miiba mibaya iliyokuwa ikimzuia njia yake. Hapo alikuwa akiomboleza na kuhuzunika. Hakuwa akitembea katika njia, kwa kumfuata kiongozi, bali alikuwa akitembea kati ya miiba na michongoma. "Loo," aliomboleza, "sio jambo la kusikitisha kwamba bustani hii nzuri imeharibiwa na miiba?" Kisha kiongozi akasema, "Wee achana na miiba, kwani itakuumiza tu. Kusanya mawaridi, yungiyungi, na maua ya rangi ya pinki." {SCsw 116.3}

Je, hakukuwa na vipande vizuri katika sehemu ya maisha na uzoefu wako? Je, hujapata nyakati nzuri ambapo moyo wako uligubikwa na furaha ulipomwitikia Roho wa Mungu? Unapotazama nyuma katika sura za uzoefu wako wa maisha, je, hupati kurasa nzuri katika maisha yako? Je, ahadi za Mungu, hazifanani kama maua yenye harufu nzuri, yanayostawi kando ya njia yako kila upande? Je, wewe hutaruhusu uzuri na harufu yake

nzuri iujaze moyo wako kwa furaha? {SCsw 117.1}

Michongoma na miiba itakuumiza na kukuhuzunisha tu; na kama ukikusanya vitu hivi tu, na kuviwasilisha kwa wengine, je, mbali na wewe mwenyewe kumkosea Mungu adabu na kuudharau wema Wake,huoni kwamba unawazuia wale wanaokuzunguka kutembea katika njia ya uzima pia? {SCsw 117.2}

Sio busara kukusanya kumbukumbu zote zisizopendeza za maisha ya zamani,—maovu na tamaa zake,—kuzizungumzia tena na tena na kuziombolezea hadi tutakapolemewa kwa kushindwa na mawazo na kisha kukata tamaa. Nafsi iliyokata tamaa imejaa giza, ikiifungia nje nuru ya Mungu isiingie moyoni na kuweka kivuli kwenye njia ya wengine. {SCsw 117.3}

Tumshukuru Mungu kwa picha angavu ambazo ametuonyesha. Hebu tuunganishe pamoja uhakikisho uliobarikiwa wa upendo Wake, ili tuweze kuzitazama mandhari hizi daima: Mwana wa Mungu alikiacha kiti cha enzi cha Baba Yake, akiuvika Uungu Wake ubinadamu, ili aweze kumwokoa mwanadamu kutoka kwa nguvu za Shetani; Ushindi Wake kwa niaba yetu, umefungua mbingu kwa ajili ya wanadamu, akifunua kwa maono ya wanadamu chumba cha uwepo wa Mungu, mahali ambapo Mungu hufunua utukufu Wake; jamii iliyoanguka imeinuliwa kutoka shimo la uharibifu ambalo dhambi iliitumbukiza humo, na kuletwa tena kwenye muunganiko na Mungu asiye na ukomo/mwisho, na baada ya kuvumilia jaribio la Kiungu kupitia imani katika Mkombozi wetu, tukivikwa haki ya Kristo, na kuinuliwa kwenye kiti Chake cha enzi—hizi ndizo picha ambazo Mungu angependa tuzifikirie. {SCsw 118.1}

Tunapoonekana kutilia shaka upendo wa Mungu na kutoziamini ahadi Zake na kumshuku, sisi tunamkosea heshima na kumhuzunisha Roho Wake Mtakatifu. Je, Mama angehisije ikiwa watoto wake wangekuwa wakiendelea kulalamikla mara

kwa mara, kana kwamba hakuwa na nia njema kwao, wakati juhudi zake zote za maisha zilikuwa katika kuendeleza maslahi yao na kuwapa faraja-(kuwaondolea usumbufu)? Je, ingekuwaje kama wangetilia shaka upendo wake mama; hii ingemvunja moyo. Mzazi yeyote angehisije kutendewa hivyo na watoto wake? Na Baba yetu wa mbinguni anatuchukuliaje tunaposhuku uaminifu Wake, na kutoamini upendo Wake kwetu, ambao umemfanya Yeye amtoe Mwanawe pekee ili tupate uzima? Mtume anaandika, ***"Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye? Warumi 8:32*** Na bado ni wangapi, kwa matendo yao, kama sio kwa maneno, wanasema, "Bwana hamaanishi hili kwangu. Labda Yeye anawapenda wengine, lakini hanipendi mimi." **{SCsw 118.2}**

Yote haya yanakuumiza roho yako mwenyewe tu; Kila neno la mashaka unalotamka, linakaribisha majaribu ya Shetani; linaimarisha ndani yako tabia ya kuwa na shaka, na linawahuzunisha malaika wanaokuhudumia. Shetani anapokujaribu, usitamke neno la mashaka au giza. Ukiamua kufungua mlango wa mapendekezo yake adui, akili yako itajazwa na kutomwamini au kutomtegemea Mungu na maswali ya uasi. Ukipenda kuzungumza kuhusu hisia zako, kila shaka unalotoa mdomoni, halitoi tu mwitikio kwako mwenyewe tu, ila pia ni mbegu itakayoota na kuzaa matunda katika maisha ya wengine, ina uwezekano wa kutoweza kupingwa, au kupikua ushawishi wa maneno yako. Wewe mwenyewe unaweza kupona kutokana na msimu wa majaribu na kutoka kwenye mtego wa Shetani, lakini wengine ambao wamevurugwa kwa kupindishwa na ushawishi wako huenda wasiweze kuepuka kutokuamini ulikopendekeza. Ni muhimu sana tuseme tu yale mambo ambayo yatatoa nguvu na uzima wa kiroho! **{SCsw 119.1}**

Malaika wanasikiliza ili wapate kusikia aina ya ripoti

unayobeba na kuitoa kwa ulimwengu kuhusu Bwana wako wa mbinguni. Acha mazungumzo yako yawe juu ya Yeye anayeishi kukuombea mbele za Baba. Unaposhika mkono wa rafiki, acha sifa kwa Mungu ziwe midomoni mwako na moyoni mwako. Hii itavutia mawazo yake rafiki huyo, kwa Yesu. **{SCsw 119.2}**

Wanadamu wote wana majaribu; huzuni ambazo ni ngumu kuzibeba, majaribu ambayo ni magumu kuyapinga. Usimwambie mwanadamu wenzako shida zako, bali beba kila kitu na kukipeleka kwa Mungu katika maombi. Ifanye hii kuwa sheria yako, kutotamka hata neno moja la mashaka au la kukatisha tamaa. Unaweza kufanya mengi kuangazia maisha ya wengine na kuimarisha juhudi zao, kwa maneno ya matumaini na furaha takatifu. **{SCsw 119.3}**

Kuna roho nyingi jasiri zilizoshinikizwa sana na majaribu, zipo karibu tayari kuzimia katika pambano na nafsi na nguvu za uovu. Usimkatishe tamaa mtu kama huyo katika mapambano yake magumu. Mtie moyo kwa maneno ya ujasiri, mshangilie na kumchangamsha kwa maneno yenye matumaini ambayo yatambariki na kumtia moyo, katika njia yake. Ndivyo nuru ya Kristo inaweza kung'aa kutoka kwako. "***Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu aishiye kwa nafsi yake. Warumi 14:7.*** Kwa ushawishi wetu, ambao hata katika fahamu zetu hatujaugundua kwamba upo, huu umetumika kuwahamasisha wenzetu nao (unconscious), wengine wanaweza kutiwa moyo na kuimarishwa, au wanaweza kukata tamaa, na kuchukizwa, na kusukumwa mbali kutoka kwa Kristo na hata ile Kweli. **{SCsw 120.1}**

Kuna wengi ambao wana wazo potofu kuhusu maisha na tabia ya Kristo. Wanafikiri kwamba Yeye hakuwa na jotojoto la uchangamfu na mwanga wa jua, kwamba alikuwa mkali, asiye na huruma, aliyekuwa na uso makini (serious), mwenye kukunja uso, mwenye mamlaka kama ya kidikteta (stern), na asiye na furaha. Mara nyingi uzoefu wote wa kidini huchafuliwa na mitazamo hii ya

huzuni. {SCsw 120.2}

Mara nyingi husemwa kwamba Yesu alilia (Yohana 11:35), lakini haikujulikana kamwe kama alitabasamu. Hakika Mwokozi wetu alikuwa Mtu wa Huzuni, na aliyejua sikitiko, kwani aliufungua moyo Wake kwa majonzi na taabu zote za wanadamu. Lakini ingawa maisha Yake yalikuwa ya kujikana nafsi, na kufunikwa na maumivu na masumbufu, moyo Wake haukuvunjika kwa kukatishwa tamaa, kuudhika, au kutoridhika. Uso Wake haukuwa na ishara ya huzuni na uchungu, bali ulikuwa na utulivu, usioonesha masumbufu na wenye amani kila wakati. Moyo Wake ulikuwa chemchemi ya uzima, na popote alipoenda alibeba pumziko, utulivu, amani, shangwe na furaha tele. {SCsw 120.3}

Mwokozi wetu alikuwa mtu dhati na makini sana na mwenye bidii, lakini kamwe hakuwa na huzuni au uchungu. Maisha, ya wale wanaomwiga Yeye yatakuwa yenye kusudi la dhati na bidii; watakuwa na hisia kubwa ya uwajibikaji binafsi. Purukushani za kejeli au futuhi zitathibitiwa; Hakutakuwa na vicheko visivyothibitiwa, vinavyosikika kwa sauti za juu, kama wale walio katika karamu za watu wa dunia wasio na adabu au staha (boisterous merriment), hakuna mizaha yenye jeuri; lakini dini ya Yesu hutoa amani kama mto unaotiririka maji. Haizimi mwanga wa furaha; haizuii furaha wala kuficha uso wenye jua na tabasamu. Kristo hakuja kutumikiwa bali kutumika; na upendo Wake utakapotawala mioyoni mwetu, sisi tutafuata mfano Wake. {SCsw 120.4}

Tukiweka kipaumbele kikubwa zaidi katika akili zetu kwenye matendo yasiyo ya fadhili na yasiyo ya haki ya wengine (watu wasiotenda mema kwetu au kwa wengine), tutaona kuwa haiwezekani kuwapenda watu hao kama Kristo alivyotupenda sisi; lakini mawazo yetu yakiweka umakini kwenye upendo wa ajabu na huruma ya Kristo kwetu, roho hiyo hiyo itawatiririkia wengine.

Tunapaswa kupendana na kuheshimiana, licha ya makosa na mapungufu ambayo hatuwezi kujizuia kuyaona. Unyenyekevu na kutokujitumainia nafsi, vinapaswa kukuzwa, kisha huruma nyororo, kujali, mapenzi kwa wengine na uvumilivu kwa makosa ya wengine. Hii itaua ubinafsi wote unaotufanya tuwe na mawazo finyu na kutufanya kuwa wema, wenye kusaidia wengine na wakarimu. {SCsw 121.1}

Mtunga Zaburi anasema, ***"Umtumaini BWANA ukatende mema, Ukae katika nchi, upendezwe na uaminifu. Zaburi 37: 3*** "Mtumaini Bwana." Kila siku ina mizigo yake, masumbufu, wasiwasi na mashaka yake; na tunapokutana na wenzetu, jinsi tunavyokuwa na utayari wa kuzungumzia kuhusu shida zetu na majaribu. Shida nyingi za kujitakia au kujitwika wenyewe hujitokeza (borrowed troubles), mizigo mizito ya hofu inaendekezwa, na wasiwasi mkubwa huzungumzwa na kuonekana nyusoni, kiasi kwamba mtu anaweza kudhani kwamba sisi hatuna Mkombozi anayetusikitia kwa huruma, anayetujali na kutufariji, aliye tayari kusikia maombi yetu yote na kuwa msaada kwetu katika kila wakati wa hitaji. {SCsw 121.2}

Baadhi ya watu, daima wana hofu, na kujitwisha au kujiletea shida wenyewe bila hata sababu. Kila siku wanazungukwa na ishara za upendo wa Mungu; kila siku wanafurahia neema na ukarimu uliosheheni wa majaliwa na mipango Yake kwao; lakini wanapuuza baraka hizi zilizopo. Akili zao, daima huweka umakini kwenye vitu visivyopendeza ambavyo wana hofu kwamba vinaweza kutokea; au pengine wana magumu fulani ambayo yaweza kuwepo ambayo, ingawa ni madogo, haya hupofusha macho yao kwa mambo mengi yanayohitaji moyo wa shukrani. Matatizo au magumu, wanayokutana nayo, badala ya kuwafanya wamsogelee Mungu, ambaye Ndiye Chanzo pekee cha msaada wao, huwatenganisha Naye kwa sababu huamsha machafuko, majuto, kuudhika, kutoridhika, kukosa furaha na kujilaumu. {SCsw

121.3}

[Je, wewe unafanya vyema kweli kwa kutilia shaka, kuwa na hofu na kutoamini ahadi, upendo na utunzaji wa Mungu?] Kwa nini sisi wanadamu tunakosa moyo wa shukrani na tunaacha kumwamini na kumtumaini Mungu? Yesu ni rafiki yetu; mbingu zote zinapendezwa nasi, na kujihusisha na maslahi/ustawi wetu. Hatupaswi kuruhusu matatizo, mambo magumu na wasiwasi wa maisha ya kila siku kusumbua akili, na kufanya tuudhike na kuleta mawingu ya huzuni kwenye paji la nyuso zetu. Tukifanya hivyo, tutakuwa na kitu cha kutuhangaisha na kutufanya tuudhike kila wakati. Hatupaswi kuendekeza masumbufu ya maisha haya ambayo hutuletea maudhi tu na kutuchakaza/kutuchosha, lakini hayatusaidii kuvumilia majaribu. {SCsw 122.1}

Unaweza kuchanganyikiwa katika shuguli au biashara; matarajio yako yanaweza kuendelea kuleta giza, naam giza nene, na unaweza kutishiwa na hasara; lakini wewe usikate tamaa; umtwike Mungu mizigo na masumbufu yako, na uendelee kubakia mtu mtulivu na mwenye furaha. Omba hekima ya kusimamia mambo yako kwa busara, na hivyo kuzuia hasara na maafa-majanga. Masihi ameahidi msaada Wake, lakini hatauleta bila juhudi zetu. Unapomtegemea Msaidizi wetu, wakati ambapo wewe umefanya yote uwezayo kwa upande wako ili kuleta matokeo mazuri, kubali matokeo, naam kubali matokeo kwa uchangamfu. {SCsw 122.2}

Sio mapenzi ya Mungu kwamba watu Wake walemewe mzigo wa masumbufu ya maisha haya. Lakini Bwana wetu hatudanganyi. Hatuambii kwamba, "Ninyi msiogope; hakuna hatari katika njia yenu." Yeye Anajua kuna majaribu na hatari, Naye anatuweka wazi kuhusu haya yote. Yeye hakusudii kuwatoa watu Wake katika ulimwengu huu wa dhambi na uovu, lakini anawaelekeza kwenye kimbilio lisiloshindwa. Maombi Yake kwa wanafunzi Wake yalikuwa, "Siombi kwamba uwatoe duniani, bali uwalinde na yule

mwovu." "Katika ulimwengu," anasema, ***"Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Yohana 17:15 Anasema Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; Mimi nimeushinda ulimwengu. Yohana 16:33*** {SCsw 122.3}

Katika Mahubiri Yake Mlimani, Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake masomo ya thamani kuhusu umuhimu wa kumtumaini Mungu. Masomo haya yalikusudiwa kuwatia moyo watoto wa Mungu katika zama zote, nasi yametufikia pia, kwa wakati wetu yakiwa yamesheheni mafundisho na faraja. Mwokozi aliwaelekeza wafuasi Wake kwa ndege walio angani walipokuwa wakiimba nyimbo zao za sifa, bila kujali masumbufu na mawazo ya kuwa wataishije, kwani "hawapandi, wala hawavuni." Na bado Baba mkuu wa mbinguni huwapa mahitaji yao. Mwokozi anauliza, **"Ninyi je! Si bora kupita hao? Mathayo 6:26** Mtoaji mkuu wa riziki zote za wanadamu na wanyama hufungua mkono Wake na kuwapa viumbe Vyake ugavi wa mahitaji yao yote. Ndege wa angani sio wadogo kiasi cha kuponyoka jicho Lake (uoni Wake). Yeye Hawadondoshei ndege chakula moja kwa moja kwenye midomo yao, lakini Yeye huwapa mahitaji yao. Lazima wakusanye nafaka ambayo Yeye Ameitawanya kwaajili yao. Lazima waandae malighafi kwa ajili ya kujenga viota vyao vidogo. Lazima wawalishe watoto wao wadogo. Hutoka wakiimba wanapofanya kazi zao, "Baba yenu wa mbinguni huwalisha." Na Je "Ninyi je! Siyo bora kupita hao?" Je, ninyi, mnaofanya ibada Kwake Mungu kwa utashi, na roho, sio wenye thamani zaidi kuliko ndege wa angani? Je, Mwenye kuanzisha uwepo wetu, na Mwenye kuuhifadhi/kuutegemeza uhai wetu, Yeye aliyetuumba Mwenyewe kwa mfano Wake wa Kiungu (Kwa sura Yake), hatatupatia mahitaji yetu ya lazima ikiwa tutamwamini na kumtumaini Yeye? {SCsw 123.1}

Kristo aliwaelekeza wanafunzi Wake kwenye maua mengi ya kondeni, yaliyokuwa yanastawi kwa fahari na kung'aa katika uzuri

ambao Baba wa mbinguni alikuwa ameyapa, kama kielelezo cha upendo Wake kwa mwanadamu. Akasema, "Fikirini maua ya mashambani" Uzuri na usahili wa maua haya ya asili unazidi uzuri, ukuu na fahari ya Sulemani. Mavazi mazuri zaidi yanayotokana na ustadi wa disaina/sanaa hayawezi kulinganishwa na neema ya asili na urembo unaong'aa wa maua ya uumbaji wa Mungu. Yesu anauliza, "Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti" Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?" Mathayo 6:28, 30. Ikiwa Mungu, Disaina/Msanii wa Kiungu, huyapa maua yenye kuharibika baada ya siku moja, rangi zao maridadi, na zinazovutia na zenye utofauti, je, kwa jinsi gani atawajali ninyi zaidi, wanadamu aliowaumba kwa mfano Wake Mwenyewe? Somo hili la Kristo ni kemeo kwa fikra za wanadamu wenye wasiwasi, utata, masumbufu, mahangaiko, mkanganyiko na mashaka, ya moyo usio na imani. **{SCsw 123.2}**

Bwana anapenda wana na binti Zake wote, wawe na furaha, amani, na watiifu. Yesu anasema, ***"amani Yangu nawapa; niwapavyo Yimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga. Hayo nimewaambia, ili furaha Yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe"*** **Yohana 14:27, 15:11 {SCsw 124.1}**

Furaha ambayo watu huitafuta kwa nia za ubinafsi, nje ya njia ya wajibu, haina balansi/msawaziko mwema na uimara, ni ya kupitapita tu, inakuja na kuondoka, na ni ya muda mfupi; inapopita, na roho inajaa upweke na huzuni; lakini kuna furaha na moyo wa kuridhika katika utumishi wa Mungu; Mkristo haachiwi atembee katika njia zisizo na uhakika; haachiwi kwenye majuto batili ambayo hayasaidii kubadilisha mambo bali kukatisha tamaa. Ikiwa hatuna raha na starehe za maisha haya, bado tunaweza kuwa na furaha kwa kutazamia maisha ya baadaye. **{SCsw 124.2}**

Lakini hata hapa ulimwenguni, Wakristo wanaweza kuwa na furaha ya ushirika na Kristo; Wanaweza kuwa na nuru ya upendo Wake, faraja ya kudumu ya uwepo Wake. Kila hatua maishani inaweza kutuleta karibu na Yesu, inaweza kutupa uzoefu wa kina wa upendo Wake, na inaweza kutuleta hatua moja karibu zaidi na makao ya amani, na yenye baraka. Basi tusitupe ujasiri wetu, bali tuwe na uhakika thabiti, ulio imara zaidi kuliko hapo awali. Hata sasa Bwana ametusaidia Naye atatusaidia hadi mwisho.1Samweli 7:12. Hebu tuangalie nguzo kuu, kumbukumbu ya kile ambacho Bwana amefanya ili kutufariji na kutuokoa kutoka mkononi mwa mwangamizi. Hebu tukumbuke upya rehema zote, mapenzi, kujali, na huruma nyororo ambazo Mungu ametuonyesha,—machozi aliyoyafuta, maumivu aliyoyatuliza, wasiwasi aliouondoa, hofu zilizoondolewa, mahitaji yaliyotolewa, baraka zilizotolewa,—hivyo sisi, tujiimarishe kwa ajili ya yote yaliyo mbele yetu katika kipindi kilichobaki cha safari yetu ya hija, ya hapa duniani. **{SCsw 125.1}**

Hatuwezi kujizuia kuangalia ya mbeleni, na kuona mambo magumu na mikanganyiko mipya katika mgogoro unaokuja, ila tunaweza kutazama yale yaliyopita na pia yale yatakayokuja, na kusema, “Hata sasa Bwana ametusaidia.” “Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.” Kumbukumbu la Torati 33:25 Jaribu linalotujia, halitazidi nguvu tutakazopewa kulistahimili. Basi hebu na tuanze kufanya kazi yetu pale tunapoipata, tukiamini kwamba, haijalishi chochote kile kinakachokuja kwetu, kwani nguvu zinazolingana na jaribu zitatolewa. **{SCsw 125.2}**

Na malango ya mbinguni yatafunguliwa ili kuwaruhusu watoto wa Mungu kuingia, kisha kutoka kinywani mwa Mfalme wa utukufu, baraka itashuka masikioni mwao kama muziki mtamu na ulioshehení zaidi, "Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu” Mathayo 25:34 **{SCsw 125.3}**

Kisha wale watu waliokombolewa watakaribishwa nyumbani ambapo Yesu anawaandalia sasa. Huko wenzao hawatakuwa waovu wa dunia, waongo, waabudu sanamu, watu wachafu (najisi), na wasioamini; lakini watashirikiana na kuishi na wale waliomshinda Shetani na kupitia neema ya Mungu, hawa wameumbiwa tabia kamilifu. Kila mwelekeo au shauku ya dhambi, kila kutokuwa na ukamilifu, kulikowatesa kwa kuwapa shida, hapa kumeondolewa kwa damu ya Kristo, na sasa ubora na mng'ao wa utukufu Wake, unaozidi mwangaza wa jua, unatolewa kwao. Na uzuri wa maadili, ukamilifu wa tabia Yake, unang'aa kupitia kwao, kwa thamani inayozidi fahari na uzuri huu wa nje. Hawana hatia mbele ya kiti cha enzi kikuu cheupe, wakishiriki hadhi/heshima, mapendeleo na fursa za malaika. {SCsw 126.1}

Kwa kuzingatia urithi mtukufu ambao unaweza kuwa wake mwanadamu, ***"mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?" Mathayo 16:26.*** Anaweza kuwa maskini, lakini ana utajiri, hadhi na heshima ambayo ulimwengu huu hauwezi kamwe kutoa. Mtu aliyekombolewa na kusafishwa kutoka dhambini, pamoja na uwezo wake wa juu na bora uliowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi wa Mungu, ana thamani kubwa sana; na kuna furaha mbinguni mbele za Mungu na malaika watakatifu kwa ajili ya mtu huyu mmoja tu aliyekombolewa, furaha inayoonyeshwa na kuhisiwa katika nyimbo za ushindi mtakatifu. {SCsw 126.2}

## Ngazi ya Kufika Mbinguni - Mwongozo wa Kujifunzia

*Kitabu cha Ngazi ya Kufika mbinguni, ambacho kimetafsiriwa kutoka kwenye Kingereza 'Steps to the Messiah'* ni mojawapo ya vitabu vyenye mionjo ya kiroho zaidi, vinavyozingatia Masihi na kazi Yake ya ukombozi na jinsi anavyotufikisha mbinguni. Nakala ya kwanza ilichapwa mwaka wa 1891. Kitabu hiki kimetafsiriwa kwenye lugha zaidi ya 160 (hadi Mei 1985).

Asili yake ni tofauti kidogo na *The Great Controversy* . Haikutegemea maono fulani maalum. Kuanzia mwaka 1890, Ellen White aliandaa kitabu hiki kipya, akielezea kwa urahisi na kwa uwazi hatua za kuchukuliwa na wenye dhambi katika kumjia Mungu. Kitabu hicho pia kilikidhi wito wa vitabu vidogo ambavyo vingeweza kutumiwa na wainjilisti katika kuwafikia watu.

Tuna uhakika kwamba kusudi la awali la mwandishi litatimizwa tena kadri kitabu cha Ngazi ya Kufika mbinguni, kitakavyosomwa na sehemu kubwa ya kanisa kwa msaada wa Mwongozo wa Kujifunza. Hii itakuwa fursa nzuri sana ya kuwafikia washiriki wapya kwa kitabu hiki cha ibada kinachopendwa sana.

## Somo la Kwanza - Kurasa 9-36

1. Ni vyanzo gani viwili muhimu vinavyoshuhudia upendo wa Mungu? Kila kimoja kinatuambia nini? (9 , 10 )

2. Ingawa uvunjaji wa sheria ya Mungu umeleta huzuni na kifo, tunaweza kujifunza nini kutokana na laana hiyo? (9 , 10)

3. Shetani amejaribuje kumwakilisha Mungu vibaya kwa wenye dhambi? (10 , 11 )

4. Yesu alipokuja kuishi miongoni mwa wanadamu, Je, alimwakilishaje Mungu? (11)

5. Kazi ya Yesu ilikuwa “kuwahubiri maskini ________________, kuwaponya ________________, kuwahubiria wafungwa ________________, kuwaponya vipofu ________________, kuwaweka ________________ walioumizwa.” ( 11 )

6. Kwa nini Yesu alichukua asili ya mwanadamu? ( 12 )

7. Unafikiri kwa nini watoto wadogo walivutiwa na Yesu? ( 12 )

8. Eleza jinsi Yesu alivyorekebisha au kukemea dhambi. ( 12 )

9. Kwa sababu gani Yesu alikuwa “Mtu wa Huzuni”? ( 13 )

10. Ni nini hasa kilichovunja moyo wa Mwana wa Mungu? ( 13 )

11. Upendo wa Mungu kwa mwanadamu na dhabihu iliyotolewa vinahusianaje hasa? ( 13 )

12. Kwa nini Yesu alikuwa dhabihu pekee inayowezekana kutolewa kwa ajili ya dhambi? ( 14 )

13. Zaidi ya dhabihu Yake kwa ajili ya wenye dhambi, Yesu amejiunganishaje na wanadamu? ( 14 )

14. Kristo ametufanyia nini zaidi ya msamaha wa dhambi? ( 15 )

## "Haja ya Mwenye Dhambi kwa Kristo"

15. Dhambi imeathirije akili ya mwanadamu? ( 17 )

16. Eleza hali ya moyo usiofanywa upya. ( 17 )

17. Mbingu ingekuwaje kwa mwenye dhambi asiyetubu? ( 17 , 18 )

18. Kwa nini elimu, utamaduni, utekelezaji wa nia, na juhudi za kibinadamu, havitoshi kumleta mtu kwenye utakatifu? ( 18 )

19. Kweli au Si kweli. Kukuza wema uliopo ndani ya mwanadamu kwa asili ndiyo pekee kunakohitajika ili kuokolewa. ( 18 , 19 )

20. Kwa nini haitoshi kujua kuhusu Mungu? Toa Maandiko yanayounga mkono jibu lako. ( 19 )

21. Ngazi katika ndoto ya Yakobo inawakilisha nini? ( 20 )

Kumbuka matumizi ya hii ngazi kwa Agano Jipya.

22. Andika orodha ya mawakala yaliyoorodheshwa kwa niaba ya mwanadamu ili kumwokoa. ( 21 )

23. Mungu hutumia njia gani kutuonya dhidi ya kumtumikia Shetani? ( 21 , 22 )

## "Toba"

24. Fafanua toba. ( 23 )

25. Ni nini kilikuwa kibaya na toba ya Esau na Yuda? ( 23 , 24 )

26. Moyo unapofunguliwa kwa Roho wa Mungu, mwenye dhambi huathiriwaje? ( 24 )

27. Daudi alipotubu, aliomba mambo yapi? ( 25 )

28. Ni kipi kinachotangulia - toba au kuja kwa Yesu? ( 26 )

29. Maliza sentensi—"Hatuwezi kutubu tena ." ( 26 )

30. Je, inawezekana kuionea aibu dhambi bila kumjua Kristo? Kuwa tayari kujadili jibu lako. ( 27 )

31. Nini kitatokea kwa mwenye dhambi ambaye hapingi upendo wa Kristo? ( 27 )

32. Swali la mawazo: Je, nimepata jibu la hamu yangu ya kitu ambacho sina ndani ya Kristo? Kama sivyo, kwa nini sivyo? ( 28 )

33. Ni nini hutokea wakati nuru kutoka kwa Kristo inapoangaza ndani ya roho zetu? Jadili uzoefu wa Danieli na Paulo. ( 28 , 29 )

34. "Mungu haoni dhambi zote kuwa sawa kwa ukubwa; kuna viwango vya hatia katika makadirio yake, na vile vile katika makadirio ya mwanadamu." Hii ina maana gani? Jiandae kujadili. ( 30 , 31 ).

35. Kwa nini tusingoje na kujitahidi wenyewe kuwa bora zaidi kabla ya kuja kwa Kristo? ( 31 )

36. Ungemjibuje mtu anayependekeza kwamba Mungu ni mwema sana kuwaangamiza wenye dhambi? ( 31 , 32 )

37. Ungempa jibu gani mtu anayesema, "Mimi ni sawa na wanaojiita Wakristo?" ( 32 )

38. Je, kuna hatari gani ya kuahirisha mambo katika kuacha dhambi? ( 37 , 38 )

39. Kupuuza au kukataa neema ya Kristo kutaathirije mwenye dhambi? ( 33 , 34 )

40. Ni faraja gani inayotolewa kwa wale wanaojaribiwa kukata tamaa kuhusu dhambi zao? ( 35 , 36 )

1. Kulingana na Mithali 28:13, hatupaswi tu kukiri dhambi zetu, bali tunapaswa kuzi ________________. ( 37 )

2. Kwa nini hija na toba hazina manufaa kwa wenye dhambi? ( 37 )

3. Inapendekezwa kwamba tuungame dhambi kwa Mungu na makosa kwa kila mmoja. Hii ina maana gani? ( 37 )

4. Sharti la kwanza la kukubalika na Mungu ni lipi? ( 37 , 38 )

5. Malizia sentensi ifuatayo: "Sababu pekee kwa nini hatuna ondoleo la dhambi zilizopita ni ____________________________________________." ( 38 )

6. Ungamo: Linapaswa kufanywaje? Linapaswa kutofanywaje? ( 38 )

7. Kwa nini ungamo liwe maalum, kwa kuikiri dhambi fulani? ( 38 )

8. Jadili mfano wa dhambi ya Israeli na kwa nini ungamo maalum lilipaswa kufanywa. ( 38 , 39 )

9. Baada ya kukiri dhambi, ni hatua gani mbili za ziada zinazopaswa kuchukuliwa? Jadili mifano ya Maandiko. ( 39 )

10. Kwa nini ni muhimu kwa mwenye dhambi kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu ili kurekebisha kasoro za tabia? ( 40 )

11. Dhambi ya Adamu na Hawa iliathirije hisia yao ya kuwajibika kwa matendo yao? ( 40 )

12. Kwa upande mwingine, toba ya kweli itamwongoza mtenda dhambi kufanya nini? ( 40 , 41 ) Jadili mifano kadhaa ya Biblia.

## "Utakaso"

13. Pitia maelezo ya Maandiko kuhusu hali yetu ya asili kama wenye dhambi. ( 43 )

14. Ni vita gani kubwa zaidi iliyowahi kupiganwa? ( 43 )

15. Fupisha:
A. Uwakilishi wa Shetani kuhusu serikali ya Mungu: ( 43 )

B. Serikali ya Mungu kama ilivyo kweli:

16. Kwa nini Mungu halazimishi utii wetu? ( 43 , 44 )

17. Orodhesha baadhi ya sanamu zinazoweza kutuzuia kumkaribia Mungu. ( 44 )

18. Ni aina gani ya dini inayopendekezwa hapa kuwa "haina thamani"? ( 44 )

19. Badala ya kuuliza ni kiasi gani tunapaswa kumpa Mungu, lengo letu linapaswa kuwa nini? ( 45 )

20. Ni jibu gani linaloweza kutolewa kwa wale wanaofikiri kawmba dhabihu kubwa sana kutoa yote kwa Kristo? ( 45 )

21. Tunabakiwa na nini tunapotoa "yote"? ( 46 )

22. Jadili kauli hii: “Mungu hatuhitaji tuache chochote ambacho ni kwa faida yetu kukihifadhi.” ( 46 )

23. Je, Mungu anawaomba watoto Wake wahifadhi furaha na furaha yote kwa ajili ya wakati ujao? Unafikiri Mkristo anawezaje kuwa na amani hata katika shida? ( 46 , 47 )

24. Unaelewaje matumizi ya nguvu ya kuchagua, au utashi? ( 47 )

25. Kuna tofauti gani kati ya kutamani kuwa mwema na kuchagua kuwa Mkristo? ( 47 , 48 )

## "Imani na Kukubali"

26. Hali ya asili ya mwenye dhambi mwenye hatia inaelezewaje? ( 49 )

27. Ni zipi baadhi ya njia zipi ambazo hatuwezi kuwa na amani ya roho? ( 49 )

28. Ni kwa njia gani pekee amani inaweza kupatikana? ( 49 )

29. Ni hatua gani zinazopaswa kuchukuliwa baada ya kukiri dhambi? ( 49 , 50 )

30. Kwa nini tunapaswa kuamini kwamba dhambi zetu zimesamehewa? ( 50 ) Toa mfano kutoka kwa huduma ya Yesu.

31. Kwa nini mtu aliyepooza aliweza kutembea? ( 50 , 51 ) Tumia uzoefu huu katika hali yako kama mwenye dhambi.

32. Inawezekanaje kwetu kusimama mbele ya sheria ya Mungu bila aibu au majuto? ( 51 )

33. Kwa nini haiwezekani kwetu kuja kwa Mungu kwa majaribio, ili kujithibitisha? ( 52 )

34. Kwa nini maelfu hushindwa katika uzoefu wao wa Kikristo? ( 52 )

35. Tunapaswa kuwa huru kutokana na tuhuma gani? Kwa nini? ( 52 , 53 )

36. Mtenda dhambi aliyetubu anapaswa kuitikiaje juhudi za Shetani za kuiba uhakikisho wake wa kukubaliwa na Mungu? ( 53 )

37. Yeremia anaongezaje somo la upendo wa Baba yetu wa mbinguni kama linavyoonyeshwa katika mfano wa mwana mpotevu? ( 54 )

38. Isaya anatoa ulinganisho gani kati ya upendo wa Mungu na upendo wa kianadamu kwa mtoto? ( 54 )

39. Tunapomkaribia Mungu kwa ________________ na ________________, Yeye atatukaribia kwa ________________ na ________________. ( 55 )

## Somo la Tatu - Kurasa 57-84

1. KWELI AU SI KWELI. Ili kujua kama ameongoka kweli au la, mtu anapaswa kuwa na uwezo wa kufuatilia hali na wakati wa kuongoka kwake. ( 57 )

2. Yawezekanaje kujulikana kwamba Roho wa Mungu anafanya kazi katika maisha ya mtu? ( 57 )

3. Ni kwa nini tabia hiyo haifunuliwi? Na Je, inafunuliwa na nini? ( 57 , 58 )

4. Ni mambo gani yanaweza kutoa usahihi wa nje tu wa mwenendo? ( 58 )

5. Ni ushahidi gani wa ndani unaoonyesha kwamba sisi ni wa Kristo? ( 58 )

6. Tunapokuwa viumbe wapya katika Kristo, nini hutokea kwa vipaumbele vyetu, ladha zetu, na tabia zetu? ( 58 )

7. Hakuna toba ya kweli isipokuwa kuna ______________________________. ( 59 )

8. Mkristo wa kweli ana mtazamo gani kuhusu wajibu au dhabihu? ( 59 )

9. Tengeneza orodha ya matokeo saba katika maisha ambapo upendo ndio kanuni ya vitendo. ( 59 )

10. Wakristo wapya wanahitaji kujilinda dhidi ya makosa gani mawili? ( 59 , 60 )

11. Unafikiri tunawezaje kuepuka makosa yoyote kati ya hayo? ( 59 , 60 )

12. Ishara ya kweli ya uanafunzi ni ipi? ( 60 )

13. Unaelewaje kauli hizi: “Hatupati wokovu wetu kwaaajili ya utii wetu.” “Utii ni tunda la imani.” ( 61 )

14. Dhana au imani ya uongo hufafanuliwaje? ( 61 )

15. Hali ya uzima wa milele ikoje? ( 62 )

16. Kwa maneno yako mwenyewe, fupisha jinsi “Kristo alivyotufanyia njia ya kutorokea.” ( 62 )

17. Linganisha "imani ambayo ni tofauti kabisa na imani" na imani ambayo imeunganishwa na imani. ( 63 )

18. Kadiri tunavyomkaribia Yesu, ndivyo tutakavyoonekana kuwa na makosa zaidi. Badala ya kusababisha kukata tamaa, hii ni ushahidi wa nini? ( 64 , 65 )

19. Hisia ya dhambi zetu inapaswa kutusukuma kufanya nini? ( 65 )

20. Toa mifano miwili kutoka kwa uumbaji/maumbile iliyotumika katika Biblia kuelezea kuzaliwa kama watoto wa Mungu. ( 67 )

21. Ukuaji wa Kikristo unaonyeshwaje kutoka kwa maumbile? ( 67 )

22. Ni kwa njia gani asili inaonyesha kwamba hapapaswi kuwa na wasiwasi au tashwishwi katika ukuaji wa Kikristo? ( 68 )

23. Ukuaji endelevu wa Kikristo unahakikishwaje? ( 69 )

24. Kazi ya kwanza kabisa ya siku inapaswa kuwa ipi? ( 70 )

25. Tutapangaje kila siku? ( 70 )

26. Unaelewaje kauli ifuatayo: "Maisha katika Kristo ni maisha ya utulivu"? ( 70 )

27. "Ni kwa _________________ Yeye, _________________ Yeye, _________________ kikamilifu juu Yake, kwamba mtabadilishwa kuwa _________________ Yake." ( 71 )

28. Wale wanaomtegemea Kristo kikamilifu watapata uzoefu gani? ( 71 )

29. Shetani atajaribu kugeuza mawazo yetu kwa watu gani? ( 71 )

30. Ni kwa jinsi gani tu uhusiano wa upendo kati ya Kristo na ubinadamu unaweza kuvunjika? ( 72 )

31. Yohana, mwanafunzi, hakuwa na upendo wa kawaida. Alipataje kuwa hivyo? ( 73 )

32. Ni masomo gani tunayoweza kujifunza kutokana na uzoefu wa wanafunzi baada ya Yesu kurudi mbinguni? ( 74 , 75 )

"Kazi na Maisha"

33. Ni masomo gani ya kujifunza kutokana na huduma ya malaika? ( 77 )

34. Upendo kwa Yesu utaonyeshwaje katika matendo yetu? ( 77 , 78 )

35. Ni nini kilikuwa “lengo moja kuu” la maisha ya Kristo duniani? ( 78 )

36. Ni nini kitakachoonekana kama matokeo ya neema ya Kristo katika maisha yetu? ( 78 , 79 )

37. Juhudi za kuwabariki wengine zitatutendeaje? ( 79 )

38. Kwa nini Mungu hakuruhusu kuhubiriwa kwa injili na malaika? ( 79 )

39. Orodhesha baadhi ya faida tunazopata kutokana na kufanya kazi kwa ajili ya wengine. ( 80 )

40. Ni kwa jinsi gani tu tutaweza kukua katika neema? ( 80 , 81 )

41. Tunaweza kujifunza nini kutokana na miaka ya mapema ya Yesu kama seremala? ( 81 , 82 )

42. Ni somo gani muhimu linalopendekezwa kuhusu matumizi ya talanta katika mfano? ( 82 , 83 )

## Somo la Nne - Kurasa 85-104

1. Mungu huzungumza nasi kwa njia gani nne leo? ( 85 na 87 )

2. Kwa nini asili ni mojawapo ya njia bora zaidi za Mwokozi za kutufundisha? ( 85 )

3. Tengeneza orodha ya baadhi ya masomo muhimu zaidi tunayoweza kujifunza kutokana na maumbile. ( 85-87 )

4. Kwa nini Mkristo ana faida zaidi ya mtunga mashairi au mtaalamu wa asili anaposoma maumbile? ( 87 )

5. Ni masomo gani maalum ya kujifunza kutokana na utafiti wa wahusika wa Biblia? (87 , 88 )

6. Tunawezaje “kula mwili na kunywa damu” ya Kristo? ( 88 )

7. Sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika vizazi vyote itakuwaje? ( 88 )

8. Je, faida chanya ya kujifunza somo hili itakuwa nini hata sasa? ( 89 )

9. “Kadiri _________________ yetu inavyozidi kumhusu Kristo, ndivyo tutakavyozidi _________________ kwake kwa wengine na _________________ kwake kwa ulimwengu?” ( 89 )

10. Matokeo chanya ya kujifunza na kutafakari kwetu Maandiko Matakatifu yatakuwa nini? ( 89 , 90 )

11. Ni mapendekezo gani yanayotolewa kuhusu mbinu za kujifunza Maandiko? ( 90 , 91 )

12. Ni nini kinachopaswa kutangulia kujifunza Biblia? Kwa nini? ( 91 )

13. Ni msaada gani wa kianadamu unaoahidiwa katika funzo letu la Biblia? ( 91 )

14. Ni nani  ambaye ni mwalimu es pekee Mwenye ufanisi wa Ukweli wa Kiungu? ( 91 )

## "Haki ya Maombi"

15. Angalia marudio ya njia nne ambazo Mungu huzungumza nasi. ( 93 )

16. Ushirika na Mungu ni wa pande mbili. Je, sehemu yetu ni ipi? ( 93 )

17. Maliza sentensi: “Sala ni _____________________________________________________.” ( 93 )

18. Ni madhumuni gani yanayopendekezwa kwa ajili ya maombi? ( 93 )

19. Taja sababu kadhaa za Yesu kuomba mara nyingi alipokuwa duniani. ( 93 , 94 )

20. Ni nini kinachowapata wale wanaopuuza maombi? ( 94 )

21. Maombi huitwa ________________ katika mkono wa imani. Andika sentensi kamili. ( 94 , 95 )

22. Masharti manne ya kujibiwa kwa maombi yametolewa. Yaorodheshe. ( 95-97 )

23. Mungu wakati mwingine hujibuje maombi yetu tunapoomba kitu ambacho hakitakuwa baraka? ( 96 )

24. Dhana inafafanuliwaje kuhusiana na sala? ( 96 )

25. Ni katika hali gani pekee tunaweza kutarajia rehema na baraka kutoka kwa Mungu tunapoomba? ( 97 )

26. Unafikiri Biblia ina maana gani inaposema tunapaswa “kuomba kwa bidii”? Tazama Warumi 12:12 . ( 97 )

27. Ni aina gani ya sala ambayo ni "uhai wa roho"? ( 98 ) Kwa nini?

28. Henoko alitembeaje na Mungu? ( 98 , 99 ) Tunaweza kufanya nini ili kutembea na Mungu?

29. Tunawezaje kuishi kama katika angahewa ya mbinguni? ( 99 )

30. Tukiendelea kuwa karibu na Mungu, ni nini kitatokea majaribu yasiyotarajiwa yanapokuja? ( 99 , 100 )

31. Pitia mambo mengi ambayo Mungu anatukaribisha kuyaeleza Kwake katika maombi. ( 100 )

32. Je, uhusiano kati ya Mungu na kila nafsi uko karibu kiasi gani? ( 100 )

33. Ni nini kinachoweza kuondoa mada na motisha ya maombi? ( 101 )

34. Tunapopuuza ushirika na wengine katika ushirika wa Kikristo, Je, hii inaathirije uzoefu wetu wa Kikristo? ( 101 )

35. Tunaposhirikiana katika ushirika wa Kikristo, uzoefu wetu wa Kikristo huathiriwaje? ( 101 , 102 )

36. Nini kingetokea katika uzoefu wetu wa Kikristo ikiwa tungefikiria na kuzungumza zaidi kuhusu Kristo? ( 102 )

37. Mbali na kuomba na kupokea, ni nini kingine ambacho maombi yetu yanapaswa kujumuisha? ( 103 )

38. Tunapaswa kufanya kazi kwa roho gani kwa ajili ya utukufu wa Mungu? ( 103 )

39. Ni nini kinapaswa kuwa mada ya hisia zetu zenye furaha zaidi? ( 103 , 104 )

## Somo la Tano - Kurasa 105-126

1. Ni tatizo gani hasa linalowasumbua wale walio vijana katika maisha ya Kikristo? ( 105 )

2. Ni mambo gani matatu kuhusu Mungu yanayothibitishwa na ushuhuda wenye mantiki? ( 105 )

3. Unafikiri kwa nini Mungu hajaondoa uwezekano wa sisi kuwa na shaka? ( 105 )

4. Maliza sentensi: "Imani yetu lazima itegemee ________________________________________________." ( 105 )

Unaamini hii ina maana gani?

5. Tunaweza kuelewa makusudi ya Mungu kwa kiasi gani? ( 106 )

6. Badala ya kutilia shaka, siri kuu za Biblia zinapaswa kutufanya tufanye nini? ( 106 , 107 )

7. Eleza jinsi Ukweli wa Biblia unavyorekebishwa kwa makundi yote ya watu ( 107 )

8. Mwamini anapaswa kuitikiaje Ukweli kwamba kuna mafumbo katika Biblia ambayo hayawezi kueleweka? ( 108 )

9. Watu wenye shaka na makafiri huitikiaje kutoweza kuelewa kila kitu katika Biblia? ( 108 )

10. Kwa nini kuna nadharia na mafundisho maarufu ambayo yanatakiwa kutokea  kwenye Biblia, lakini hayatoki hapo? ( 108 , 109 )

10. Why are there popular theories and doctrines that are supposed to come from the Bible, but do not? (108, 109)

11. Kwa nini viumbe vilivyoumbwa havitakuwa na uelewa kamili wa Mungu na kazi Zake? ( 109 )

12. Ni kwa namna gani pekee tunaweza kuelewa Neno la Mungu? ( 109 )

13. Malizia sentensi: “Mungu anataka mwanadamu atumie

______________________________________________

yake.” ( 109 )

14. Watu husomaje Biblia kwa njia ambayo inaweza kusababisha madhara? ( 110 )

15. Ni nini chanzo halisi cha shaka na wasiwasi katika visa vingi? ( 111 )

16. Ni kwa njia gani pekee tunaweza kufikia Ukweli katika kujifunza Biblia? ( 111 )

17. Tunawezaje kupokea nuru na uelewa zaidi? ( 111 )

18. Uzoefu una nafasi gani katika kujenga imani yetu katika Neno la Mungu? ( 111 )

19. Ni lini  ndipo tunaweza kuwa na uhakika kwamba tutapata majibu ya yote ambayo yametusumbua? ( 113 )

## “Kufurahi katika Bwana”

20. Inamaanisha nini? “Kupitia kila mmoja wa watoto Wake, Yesu hutuma barua kwa ulimwengu.” ( 115 )

21. Je, tunawezaje kumfurahisha Shetani? ( 116 )

22. Ni wazo gani potofu kuhusu maisha ya kidini ambalo Shetani anajaribu kuwasilisha? ( 116 )

23. Pitia masomo ya ndoto ya Ellen White ya bustani yenye miiba na maua ya waridi. ( 116 , 117 )

24. Linganisha matokeo ya kupitia upya matukio ya zamani ambayo yamekuwa ya furaha na yale ambayo yamekuwa ya kukatisha tamaa. ( 117 )

25. Fikiria ulinganifu uliopo kati ya mtoto anayelalamika na malalamiko yetu kuhusu Baba yetu wa mbinguni. ( 118 )

26. Ni madhara gani mawili yanayotokea kwa kuzungumza kuhusu mashaka? ( 119 )

27. Tunawezaje kuwaathri wengine bila kujua kwa wema au ubaya? ( 120 )

28. Eleza maisha na tabia ya Kristo. ( 120 )

29. Je, Kristo alibeba nini, popote alipoenda, ( 120 )

30. Fupisha jinsi tunavyopaswa kumwiga Kristo. ( 120 , 121 )

31. Ni nini kitakachotufanya tusiweze kuwapenda wengine? ( 121 ) Tunawezaje kujifunza kuwapenda wengine?

32. Unafikiri inamaanisha nini "kujikobesha shida"? ( 121 , 122 )

33. Maliza sentensi hii. “Hatupaswi kuruhusu misukosuko ______________________________________________________.” ( 122 )

34. Ni mapendekezo gani mawili yanatolewa kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya biashara? ( 122 )

35. Katika Mahubiri ya Yesu Mlimani, ni masomo gani ya kumtumaini Mungu yanayojifunzwa kutoka kwa ndege? ( 123 )



36. Katika mahubiri hayo-hayo, ni masomo gani Kristo aliyatoa kutoka kuhusu yungiyungi? (water lilies)( ( 124 )



37. Ni sifa gani za furaha zinazotafutwa kutokana na nia za ubinafsi? ( 124 )

38. Utumishi wa Mungu unalinganishwaje? ( 124 )

39. Ni "nguzo kuu" gani tunazohimizwa kuzikumbuka? ( 125 )

40. Tuna uhakika gani kuhusu majaribu? ( 125 )

41. Pitia thawabu za furaha za mbinguni. ( 125 , 126 )

Asili na ufunuo wa Mungu kwa wanadamu, vyote kwa pamoja hushuhudia upendo wa Mungu. Ni uvunjaji (uasi) wa Sheria ya Mungu, Sheria ya upendo, ndio imeleta misiba na kifo. Lakini hata katikati ya mateso yanayotokana na dhambi, upendo wa Mungu unafunuliwa. “Mungu ni upendo” imeandikwa juu ya kila chipukizi, juu ya kila unyasi unaochipuka.

Masihi alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu ili kudhihirisha upendo wa Mungu usio na kikomo. Upendo, rehema, na huruma zilikuwa zimefunuliwa katika kila tendo la maisha Yake; Moyo Wake ulikwenda kwa huruma nyororo, mapenzi mwanana, na kujali, kwa watoto wa wanadamu. Alichukua asili ya mwanadamu, ili Aweze kufikia matakwa ya mwanadamu. Maskini na wanyenyekevu zaidi hawakuogopa kumkaribia Yeye. Hiyo ndiyo tabia ya Kristo kama inavyofunuliwa katika maisha Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu.

Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa ndiyo maana Yesu aliishi, aliteseka, na kufa. Alifanyika “Mtu wa Huzuni,” ili sisi tupate kufanywa washirika wa furaha ya milele. Lakini dhabihu hii kuu haikutolewa ili kuunda katika Moyo wa Baba upendo kwa mwanadamu, sio kumfanya awe tayari kutuokoa. Hapana, hapana! “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee.” Yohana 3:16. Baba anatupenda, sio kwa sababu ya upatanisho mkuu, bali Yeye Alitoa upatanisho kwa sababu anatupenda. Hakuna mwingine ila Mwana wa Mungu Ndiye Ambaye angeweza kutimiza ukombozi wetu.

Hii inaweka thamani iliyoje kwa mwanadamu! Kupitia uasi, wana wa wanadamu wanakuwa raia wa Shetani. Kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho ya Kristo, wana wa Adamu wanaweza kuwa wana wa Mungu. Upendo usio na kifani wa Mungu kwa ulimwengu ambao haukumpenda! Mawazo yana nguvu ya kutiisha juu ya nafsi na huleta akili katika utumwa wa mapenzi ya Mungu.

Mwanadamu hapo awali alijaliwa uwezo bora na akili iliyo na utimamu mzuri. Alikuwa mkamilifu katika nafsi yake, na mapatano na Mungu. Mawazo yake yalikuwa safi, malengo yake yalikuwa matakatifu. Lakini kwa kutokutii, nguvu zake zilipotoshwa, na ubinafsi ukachukua nafasi ya upendo. Asili yake ilidhoofika sana kupitia dhambi ambayo haikuwezekana kwake, kwa nguvu zake mwenyewe, kupinga nguvu za uovu.

Haiwezekani sisi, naam, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni miovu, na hatuwezi kujibadilisha. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya sisi wanadamu kubadilishwa kutoka katika dhambi hadi utakatifu. Nguvu hiyo ni Kristo. Neema Yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha uwezo usio na uhai wa nafsi, na kutuvuta kwa Mungu, kwa utakatifu. Kwa wote, kuna jibu moja tu, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Hebu na tuikubali njia hii iliyotolewa kwa ajili yetu ili tuweze kugeuzwa na kufanana Naye, na kurejeshwa katika ushirika na malaika wanaohudumia, kwa maelewano na ushirika na Baba na Mwana.

Mtu atakuwaje mwenye haki mbele za Mungu? Mwenye dhambi atafanywaje kuwa mwadilifu? Ni kwa njia ya Kristo pekee tunaweza kuletwa katika mapatano na Mungu, kwa utakatifu; lakini tunawezaje kumwendea Kristo?

Toba ni pamoja na huzuni kwa ajili ya dhambi na kuiacha. Hatutaacha dhambi mpaka tuone ubaya wake; mpaka tuiache kwa moyo, hakutakuwa na mabadiliko ya kweli katika maisha. Lakini moyo unapokubali kuongozwa na Roho wa Mungu, dhamiri itahuishwa, na mwenye dhambi atatambua jambo fulani la kina, na utakatifu wa Sheria takatifu ya Mungu, na msingi Wa serikali Yake mbinguni na duniani. Kisha usadikisho hushika akili na moyo.

Ombi la Daudi, baada ya anguko lake, linaonyesha asili ya huzuni ya kweli kwa ajili ya dhambi. Toba yake ilikuwa ya dhati na ya kina. Hakukuwa na jitihada za kutuliza hatia yake; hakuwa na hamu ya kutoroka hukumu inayomtishia ila aliongozwa katika maombi yake. Daudi aliona ukubwa wa kosa lake; aliona unajisi wa nafsi yake; yeye aliichukia dhambi yake. Haikuwa

kwa ajili ya msamaha tu kwamba aliomba, lakini kwa ajili ya usafi wa moyo. Alitamani furaha ya utakatifu, kurejeshwa katika maelewano na ushirika na Mungu.Toba kama hii haiwezi kufikiwa na uwezo wetu wenyewe na kuikamilisha; bali hupatikana tu kutoka Kristo.

Kristo Yuko tayari kutuweka sisi huru kutokana na dhambi, lakini halazimishi nia hiyo. Tukikataa, Je, Yeye anaweza kufanya nini zaidi? Jifunze Neno la Mungu kwa maombi. Unapoona ukubwa wa dhambi maishani mwako, kama unavyojiona jinsi ulivyo, usikate tamaa kwa kupoteza matumaini. Ni wenye dhambi ndio ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Shetani anapokuja kukuambia kuwa wewe ni mwenye dhambi mkuu, wewe mtazame Mkombozi wako na uongee juu ya wema Wake. Ikiri dhambi yako, lakini mwambie adui kwamba "Kristo alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi" ili mimi nipate kuokolewa (1 Timotheo 1:15).

"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema." Mithali 28:13. Masharti ya kupata rehema ya Mungu ni rahisi na ya haki na busara. Ungameni dhambi zenu kwa Mungu, Ambaye peke Yake Ndiye anayeweza kuwasamehe, na msameheane makosa yenu ninyi kwa ninyi. Wale ambao hawajanyenyekesha nafsi zao mbele za Mungu, kwa kukiri hatia yao, bado hawajatimiza hatua ya kwanza ya kukubalika, kwani sharti tuwe tayari kuinyenyekesha mioyo yetu na kufuata masharti ya Sheria ya Neno la Kweli. Kukiri ambako kunamiminiwa kwa roho ya ndani hupata njia yake kwa Mungu wa huruma Asiye na kikomo. Kuungama kwa kweli siku zote huwa na tabia maalum, na hukubali dhambi fulani. Maungamo yote yanapaswa kuwa ya uhakika na ya kulenga jambo mahususi. Imeandikwa, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1John 1:9.

Ahadi ya Mungu ni, "Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote." Yeremia 29:13. Moyo wote sharti utolewe, au mabadiliko hayawezi kamwe kufanywa ndani yetu ambayo kwayo tunapaswa kurejeshwa kwa mfano Wake Bwana.

Vita dhidi ya nafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa. Kujitolea kwa

nafsi, kusalimisha Mapenzi yetu yote kwa Mungu, kunahitaji mapambano; lakini nafsi inapaswa kunyenyekea kwa Mungu kabla ya kufanywa upya katika utakatifu. Katika kujitoa kwa Mungu, ni lazima kuacha yote ambayo yangetutenganisha Naye. Kuna wale wanaodai kumtumikia Mungu huku wakitegemea juhudi zao wenyewe kutii Sheria Yake, ili kuunda tabia sahihi na kupata wokovu. Mioyo yao haiguswi na hisia yoyote ya kina ya upendo wa Kristo, lakini wanatafuta kutekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo kama vile ambavyo Mungu anataka kutoka kwao ili kuipata mbingu. Dini kama hiyo haina thamani.

Kristo akikaa ndani ya moyo, roho itajawa na upendo Wake, na furaha ya kuungana Naye, kwamba roho itashikamana Naye; na katika kumfikiria Yeye, nafsi itasahauliwa. Upendo kwa Mwenyezi Mungu utakuwa chemchemi ya kila wazo na tendo. Mambo hayo hayalengi viwango vya chini kabisa, bali hulenga kupatana kikamilifu na Mapenzi ya Mkombozi wao.

Je, unahisi kwamba ni dhabihu kubwa sana kwako kutoa yote kwa Kristo? Jiulize swali, "Ni nini Kristo ametoa kwa ajili yangu?" Mwana wa Mungu alitoa maisha yake yote, kwa upendo na akapitia mateso kwa ajili ya ukombozi wetu. Je, sisi, tusiostahili, ambao ni walengwa wa upendo mkuu hivyo, tutazuia mioyo yetu Kwake? Je, Tunatoa nini zaidi wakati tunatoa yote? Ni Moyo uliochafuliwa na dhambi tu, ndiyo tunatoa na hakuna lingine la thamani tunalolitoa kwa Mungu, tunautoa moyo huu, ili Yesu ausafishe, ausafishe kwa damu Yake Mwenyewe, na kutuokoa kwa upendo Wake usio na kifani. Na ajabu ni kwamba, bado watu wanafikiri ni vigumu kuacha yote! (na kumbe kile tunachokiacha ni moyo mchafu tu). Mungu hataki tutoe chochote ambacho ni cha manufaa kwetu ili tubaki salama. Katika yote anayofanya, Yeye ana maslahi ya watoto Wake katika mtazamo Wake.

Wengi wanauliza, "Nifanyeje ili kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu?" Unatamani kujitoa Kwake, lakini u dhaifu katika uwezo wa kimaadili, kisha una utumwa wa mashaka, na unatawaliwa na tabia za maisha ya dhambi. Ahadi na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Ujuzi ulio nao kuhusu ahadi zako zilizovunjwa na ahadi ulizopoteza hudhoofisha kujiamini kwako katika unyofu

wako mwenyewe, na kukufanya uhisi kwamba Mungu hawezi kukukubali; lakini huna haja kukata tamaa.

Unachohitaji kuelewa ni nguvu ya kweli ya uthubutu (uchaguzi). Hii ndiyo nguvu inayotawala katika asili ya mtu, nguvu ya uamuzi, au ya kuchagua. Kila kitu kinategemea hatua sahihi ya uthubutu. Nguvu ya uhuru wa kuchagua ambao Mungu amewapa wanadamu; ni juu ya hii unapaswa kuifanyia mazoezi. Huwezi kubadilisha moyo wako, na huwezi kujibadili wewe mwenyewe, kwahiyo mpe Mungu mapenzi (matamanio) ya moyo wako; lakini unaweza kuchagua kumtumikia. Unaweza kumpa mapenzi yako; Naye Atafanya kazi ndani yako, kunia na kutenda sawasawa na mapenzi Yakememа. Kwa hivyo asili yako yote itaweza kuletwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo; mapenzi yako yataelekezwa Kwake, mawazo yako yatakuwa sawa na Yeye.

Matamanio ya kuwa na wema na utakatifu ni sawa kadiri yanavyokwenda; lakini ukiishia hapa, hautafaidika kwa chochote. Wengi watapotea huku wakitumaini na kutamani kuwa Wakristo. Hawafikii hatua ya kuweka mapenzi yao kwa Mungu. Hawachagui sasa kuwa Wakristo.

Kupitia mazoezi sahihi ya uthubutu, mabadiliko yote yanaweza kufanywa katika maisha yako. Utakuwa na nguvu kutoka juu ili kukuweka imara, na hivyo kupitia kuendelea kujitoa daima kwa Mungu utawezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya imani.

Kwa vile dhamiri yako imehuishwa na Roho Mtakatifu, umeona kitu juu ya uovu/ubaya wa dhambi, na nguvu zake, hatia yake, na majanga yake; na sasa unaitazama dhambi kwa chuki. Ni amani ndiyo unayohitaji. Umeungama dhambi zako, na kuziweka mbali na moyo wako. Umeamua kujitoa kwa Mungu. Sasa nenda Kwake, na umwombe kwamba akuoshe dhambi zako na kukupa moyo mpya.

Basi amini kwamba Yeye Anafanya hivi kwa sababu ameahidi hivyo. Zawadi ambayo Mungu anatuahidi, ni sharti tuamini kwamba tunaipokea, na kwamba ni zetu. Wewe ni mwenye dhambi. Huwezi kulipia dhambi zako zilizopita;

huwezi kuubadili moyo wako na kujifanya kuwa mtakatifu. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia Kristo. Wewe amini tu ahadi hiyo. Tubu dhambi zako na kujitoa kwa Mungu. Utapenda kumtumikia. Vile vile unapofanya hivi, hakika Mungu atatimiza Neno Lake kwako. Ikiwa unaamini katika ahadi hiyo, Mungu anaitoa kwako kweli (kiuhalisia). Usisubiri mpaka uhisi kuwa umefanywa mzima, lakini sema, "Naamini; ni hivyo, si kwa sababu ninaihisi, bali kwa sababu Mungu "Aliahidi."

## *Sehemu ya Pili*

### Je, ninawezaje Kubaki Mkweli kwa Kristo?

Yesu anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Kuna sharti kwa ahadi hii - kwamba tuombe sawasawa na Mapenzi ya Mungu. Lakini ni Mapenzi ya Mungu kutusafisha na dhambi zetu, kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Hivyo tunaweza kuomba baraka hizi, na kuamini kwamba tunazipokea, na kumshukuru Mungu kwamba tumepokea ahadi hizo.

Tangu sasa ninyi si mali yenu wenyewe; mmenunuliwa kwa bei kubwa. Kupitia tendo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezaa maisha mapya ndani ya moyo wako. Wewe ni mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, na Yeye anakupenda kama vile anavyompenda Mwanawe.

Sasa kwa kuwa umejitoa kwa Yesu, usirudi nyuma tena, usijiondoe Kwake, lakini siku baada ya siku sema, "Mimi ni wa Kristo, nimejitoa Kwake," na umwombe Akupe Roho Wake ili Akutunze kwa neema Yake. Kama ilivyo, unapojitoa kwa Mungu, na kumwamini, basi, unakuwa mtoto Wake, ndivyo na wewe wanapaswa kuishi ndani Yake.

Hapa ndipo maelfu wanaposhindwa; hawaamini kwamba Yesu anasamehe kila nafsi, yaani mtu mmoja mmoja. Hawamtilii maanani Mungu katika Neno Lake. Ni fursa ya wote wanaotii masharti kujua wenyewe kwamba msamaha unatolewa kwa kila dhambi. Ondoa shaka kwamba ahadi za Mungu

hazikukusudiwa kwa ajili yako. Ahadi za Mungu zipo kwa ajili ya kila nafsi inayotubu. Inueni macho juu, ninyi wenye mashaka na kutetemeka; kwa maana Yesu Yu hai ili atuombee. Mshukuruni Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mwanawe mpendwa.

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama, mambo yote yamekuwa mpya." 2 Wakorintho 5:17. Huenda mtu asiweze kutaja wakati au mahali hasa, au kufuatilia mlolongo wote kwamba mambo yalikuwaje katika huu mchakato wa uongofu; lakini hii haithibitishi kuwa wewe haujaongoka.

Mabadiliko yataonekana katika mwenendo, tabia, na utendaji wako. Tofauti itakuwa wazi na kuamuliwa kati ya vile ambavyo ulivyo sasa na ulivyokuwa. Nani ana moyo wako? Mawazo yetu yanamilikiwa na nani? Je, tunapenda kuzungumza juu ya nini au nani? Ni nani aliye na upendo wetu makini na nguvu zetu bora zaidi? Ikiwa sisi ni wa Kristo, mawazo yetu yapo pamoja Naye. Hakuna uthibitisho wa toba ya kweli isipokuwa inafanya kazi ya matengenezo.

Uzuri wa tabia ya Kristo utaonekana kwa wafuasi Wake. Ilikuwa furaha Yake Masihi kufanya Mapenzi ya Mungu. Kuna makosa mawili ambayo watoto wa Mungu hasa wanatakiwa kujilinda nayo: La kwanza ni lile la kujivunua kazi zao wenyewe, kujiamini kuwa wao wanaweza kufanya kitu fulani, ili kuweza kujileta wenyewe katika mapatano na Mungu. Yote ambayo mwanadamu anaweza kufanya bila Kristo yamechafuliwa na ubinafsi na dhambi. Ni neema ya Kristo pekee, kwa njia ya imani, ndiyo ambayo inaweza kutufanya watakatifu.

Kosa la pili lililo kinyume na la hatari ni kwamba watu huamini kwamba imani katika Kristo huwaachilia wanadamu kutoka katika kuishika Sheria ya Mungu; kwamba kwa kuwa na imani pekee tunakuwa washiriki wa neema ya Kristo, matendo yetu hayana la kufanya katika suala la ukombozi wetu.

Utii ni tunda la imani. Haki inafafanuliwa kwa kiwango cha Sheria takatifu ya Mungu, kama inavyoonyeshwa katika zile Amri kumi (Kutoka 20:3-20). Kile kinachoitwa imani katika Kristo ambacho kinadai kuachilia watu kutoka katika wajibu wa utii kwa Mungu, sio imani, lakini ni kiburi na uelewa ulio na makosa.

Sharti la uzima wa milele, kama lilivyo sasa ndivyo lilivyokuwa siku zote - kama ilivyokuwa katika edeni (au paradiso) kabla ya anguko la wazazi wetu wa kwanza, sharti hilo ni Utii mkamilifu kwa Sheria ya Mungu, ambayo ndiyo uadilifu mkamilifu.

Ikiwa uzima wa milele ungetolewa kwa sharti lolote pungufu ya hili, basi ni furaha ya sayari zote na mbingu imo hatarini. Njia ingelifunguliwa wazi kwa ajili ya dhambi, pamoja na msururu wake wote wa misiba na taabu, hata kama watu hawafi.

Kristo anabadilisha moyo. Anakaa moyoni mwetu kwa imani. Tunapaswa kudumisha uhusiano huu na Kristo kwa imani na kujitoa daima kwa mapenzi yetu Kwake; na mradi unafanya hivi, Yeye atafanya kazi ndani yake kutaka na kutenda kulingana na mapenzi Yake mema.

Kadiri unavyomkaribia Masihi, ndivyo utakavyoona ulivyo na makosa zaidi machoni pako; maana maono yako yatakuwa wazi zaidi. Huu ni ushahidi kwamba udanganyifu wa Shetani unapoteza nguvu zake. Hakuna upendo wa kina kwa Yesu unaoweza kukaa katika moyo ambao hautambui dhambi yake wenyewe. Nafsi inayogeuzwa kwa neema ya Kristo itapendezwa na tabia Yake Mungu. Mtazamo wa dhambi zetu unasukuma na Yeye anayeweza kusamehe; na wakati nafsi, inatambua unyonge wake, na kumfikia Kristo, Yeye atajidhihirisha kwa uwezo Wake. Kadri hisia za kumhitaji zinavyotusukuma Kwake na kwa Neno la Mungu, ndivyo tutakavyokuwa na mitazamo iliyotukuka zaidi juu ya tabia Yake, na kwa ukamilifu zaidi tutaiakisi sura Yake.

Badiliko la mioyo ambalo kwalo tunafanyika kuwa wana wa Mungu linapatikana katika Biblia kama kuzaliwa. Tena linalinganishwa na kuota kwa mbegu nzuri iliyopandwa na mkulima. Ni Mungu Ndiye anayeleta chipukizi la majani kutokea na kisha ua, na mwishowe matunda. Ni kwa uwezo Wake mbegu hukua. Kama vile Ua linavyoligeukia jua, ili miale yake angavu isaidie katika ukamilifu mzuri na ulinganifu wake; ndivyo sisi tutakiwavyo kuligeukia Jua la Haki, ili nuru ya mbinguni iangaze juu yetu, ili tabia zetu ziweze kukuzwa katika kufanana na Kristo.

Je, unauliza, “Ninawezaje kukaa ndani ya Kristo?” Kama jinsi ulivyompokea Kristo hapo kwanza. "Basi kama mlimpokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye.” Wakolosai 2:6. Kwa imani wewe ukawa Wake Kristo; na kwa imani unapaswa kukua ndani Yake kwa kutoa na kupokea. Unapaswa kutoa yote, moyo wako, mapenzi yako, huduma yako, hebu jitoe Kwake ili kutii matakwa Yake yote; nawe sharti uvibebe vyote, yaani umchukue Kristo (Ambaye Ndiye vyote), Ambaye ni utimilifu wa baraka zote, Naye Akae moyoni mwako, Awe nguvu yako, Awe haki yako, na Msaidizi wako wa milele wa kukupa uwezo wa kutii.

Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, Nitwae, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote na itimizwe ndani yako.” Niepushe kuyafanya yale ambayo sipaswi kuyafanya, na kuyafanya yale ambayo napaswa kufanya. Hili ni jambo la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Peleka mipango yako yote Kwake, ili itekelezwe au iache kutokana na majaliwa Yake yatakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku unaweza kuendelea ku yatoa maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.

Maisha ndani ya Kristo ni maisha ya utulivu. Kunaweza kuwa hakuna furaha yenye mihemko ya hisia, lakini kunapaswa kuwa na uvumilivu wa kuendelea kudumu katika Imani yenye matumaini. Wakati akili inapokaa juu ya ubinafsi, inageuzwa mbali na Kristo, Aliye chanzo cha nguvu na uhai. Kwa hivyo, ni juhudi ya mara kwa mara ya Shetani kutoa usikivu kutoka kwa Mwokozi na hivyo kuzuia muungano na ushirika wa roho na Kristo.

Kristo alipotwaa asili ya mwanadamu juu Yake, Aliufungamanisha ubinadamu Kwake kwa kifungo cha upendo ambacho hakiwezi kamwe kuvunjwa na mamlaka yoyote, isipokuwa chaguo la mwanadamu mwenyewe. Shetani ataendelea kuweka vivutio vya kutushawishi kuvunja uhusiano huu yaani kuchagua kujitenga na Kristo. Lakini wacha tuendelee kuinua macho

yetu kumtazama Kristo, Naye atatuhifadhi. Tukimtazama Masihi, tuko salama. Hakuna kinachoweza kutung'oa kutoka mkononi Mwake. Yote ambayo Kristo alikuwa kwa wanafunzi, anatamani yawe kwa watoto Wake leo.

Yesu alituombea, na aliomba kwamba tuwe na umoja Naye, kama vile Yeye alivyo mmoja na Baba. Huu ni muungano wa thamani kiasi gani! Hivyo, tukimpenda na kukaa ndani Yake, “Tutakua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye Aliye kichwa, Kristo.” Waefeso 4:15.

Mungu Ndiye chanzo cha uhai na nuru na furaha kwa ulimwengu. Popote uzima wa Mungu unapokuwepo ndani ya mioyo ya watu, uzima huo utatiririka kwa wengine kwa upendo na baraka.

Furaha ya Mwokozi wetu ilikuwa katika kuinuliwa na ukombozi wa wanadamu walioanguka. Kwa hili hakuyahesabu maisha Yake kuwa ya thamani Kwake Yeye Mwenyewe, bali aliustahimili msalaba na kuidharau aibu. Wakati upendo wa Kristo umo ndani ya moyo, ni kama manukato au harufu nzuri isiyoweza kufichwa. Upendo kwa Yesu utadhihirika katika hamu ya kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kwa ajili ya baraka na kuinuliwa kwa ubinadamu. Upendo kwa Kristo huleta mwitikio wa upendo, rehema, na huruma yenye mguso kwa viumbe vyote ambavyo Baba yetu wa mbinguni Anavitunza. Wale walio washiriki wa neema ya Kristo watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote, ili wengine aliowafia wapate kushiriki zawadi ya mbinguni. Watafanya yote wawezayo kufanya duniani, ili dunia iwe mahali bora zaidi katika kukaa kwao humo. Roho hii ndiyo chanzo cha uhakika cha nafsi iliyoongoka kweli kweli. Mara tu mtu anapokuja kwa Kristo ndipo unazaliwa ndani ya moyo wake, hamu ya kufanya Kristo ajulikane kwa wengine na kwamba ni urafiki wa thamani gani ameupata kwa Yesu (In Jesus I found a friend). Ikiwa tumeonja na kuona kwamba Bwana ni mwema, tutakuwa na kitu cha kusema. Tutajaribu kuwasilisha kwa wengine vivutio vya Kristo na mambo yasiyoonekana ya ulimwengu ujao. Kutakuwa na nguvu yenye matamanio makubwa katika kufuata njia ambayo Yesu aliipita.

Na jitihada za kuwabariki wengine zitaleta mwitikio wa baraka juu yetu wenyewe. Wale ambao wanakuwa washiriki katika kazi ya upendo, huletwa

karibu zaidi na Muumba wao. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine hutoa kina, uthabiti, na kuwa na tabia ya kupendeza kama Kristo kwa mhusika, na kisha huleta amani na furaha kwa mhusika (mtoaji). Nguvu huja kwa kujizoeza. Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani, au hata kuacha mazingira ya nyumba zetu, ikiwa hapo ni pale ambapo wajibu wetu uko, ili kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Kwa roho ya upendo tunaweza kufanya kazi kwa unyenyekevu katika maisha "kwa Bwana." Wakolosai 3:23. Ikiwa upendo wa Mungu umo moyoni, utadhihirika katika maisha yetu. Haupaswi kungojea hafla nzuri au kutarajia uwezo wa ajabu kabla ya kwenda kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Wanafunzi wanyenyekevu na maskini zaidi wa Yesu wanaweza kuwa baraka kwa wengine wakati wote.

Kuna njia nyingi ambazo Mungu anatafuta kujitambulisha kwetu na kutuleta katika ushirika pamoja Naye. Ikiwa tutasikiliza tu, Asili huzungumza na hisia zetu bila kukoma. Kazi zilizoumbwa na Mungu zitatufundisha masomo ya thamani ya utii na uaminifu.

Hakuna machozi yanayotolewa ambayo Mungu hayatambui. Hakuna mwenendo asioutia alama. Kama tungeweza kumwamini kikamilifu, mahangaiko yote yasiyofaa yangetupiliwa mbali. Maisha yetu yasingejazwa na kukata tamaa kama ilivyo sasa; kwa maana kila kitu, kiwe kikubwa ama kidogo, kingeachwa mikononi mwa Mungu.

Mungu huzungumza nasi kupitia kazi Zake na majaliwa na kupitia ushawishi wa Roho Wake juu ya moyo yetu. Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake. Hapa tunayo mistari iliyo wazi zaidi ya ufunuo wa tabia Yake, kushughulika Kwake na wanadamu, na kazi kuu ya ukombozi. Jaza moyo wote kwa Neno la Mungu. Neno ni maji yaliyo hai, yakizima kiu yako iwakayo. Neno ni mkate wa uzima kutoka mbinguni.

Siri ya ukombozi ni jambo ambalo malaika wanatamani kuliangalia na kulijua ila ni fumbo na siri; ukombozi wa mwanadamu itakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika enzi zote zisizo na kikomo za milele. Kama ni hivyo, Je, haifai basi tufikirie sasa kwa makini na kujifunza leo hii? Tunapotafakari juu ya Mwokozi, kutakuwa na njaa na kiu ya nafsi ya kuwa

kama Yeye Ambaye tunamwabudu.

Biblia iliandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Kweli kuu zinazohitajika kwa wokovu zinafanywa wazi kama mchana. Hakuna kitu kinachohesabiwa kuimarisha akili kuliko kujifunza Maandiko Matakatifu. Lakini kuna faida kidogo inayopatikana kwa kusoma Biblia haraka-haraka. Fungu moja likisomwa kwa makini hadi tukagundua umuhimu kwa akili zetu na uhusiano wake, na mpango wa wokovu ukawa dhahiri, huu ndio usomaji wa thamani zaidi kuliko usomaji wa sura nyingi bila malengo dhahiri na hakuna maagizo chanya yaliyopatikana.

Weka Biblia yako pamoja nawe. Upatapo nafasi, isome; yaweke maandishi kwenye kumbukumbu yako. Hatuwezi kupata hekima bila uangalifu wa dhati na kujifunza kwa sala.

Kamwe Biblia haipaswi kusomwa bila maombi. Kabla ya kufungua kurasa Zake, tunapaswa kuomba nuru ya Roho Mtakatifu, nayo itatolewa. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru watakuwa pamoja na wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo wanatafuta mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anawathaminiwanadamu? Yeye alimtoa Mwanawe ili afe kwa ajili yao na anamtuma Roho Wake Mtakatifu kuwa mwalimu wa mwanadamu, Naye ni kiongozi wa kudumu!

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa Yake, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu anazungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake. Ili kuwasiliana na Mungu, sharti tuwe na kitu cha kumwambia kuhusu maisha yetu halisi, maisha ya kila siku. Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni sharti tumjulishe Mungu mambo yalivyo kwetu, bali ni ili Atuwezeshe kumpokea Yeye mioyoni mwetu. Maombi hayamshushi Mungu kwetu, lakini maombi hutupeleka juu Kwake.

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupa utimilifu wa baraka Zake. Inashangaza kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! Mungu Yuko tayari kutubariki na Anawiwa kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio

wanyenyekevu zaidi. Malaika wa mbinguni wanashangaa wanapofikiria juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, nao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana, wakati Moyo wa Mungu wenye upendo usio na kikomo una matamanio nao, Naye Yupo tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria.

Giza la mwovu linawafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya kunong'ona ya adui huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii fursa ya maombi. Walakini maombi ndio ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala ya mbinguni, ambapo rasilimali zisizo na kikomo za Mweza wa yote zinatunzwa.

Kuna masharti fulani ambayo kwayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yetu: Moja ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Tukiwaza maovu mioyoni mwetu, tukishikamana na dhambi yoyote tuijuayo; Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu na aliyeungama hukubaliwa daima. Wakati wote makosa yanayojulikana yanaposahihishwa, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu.

Kipengele kingine cha maombi yenye nguvu ni imani. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia kwa bidii ahadi Zake; kwani wakati wa kujibiwa utakuja hakika, na tutapokea baraka tunazozihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa namna tutakavyo na kila kitu tunachokitamani ni dhana za kufikirika.

Tunapokuja kwa Mungu katika maombi, tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha ndani ya mioyo yetu wenyewe. Kuendelea kudumu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea majibu yetu. Sharti tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu.

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwa maana haya ndiyo maisha ya kiroho. Sala ya familia au ya hadhara pekee yake haitoshi. Maombi ya siri yanasikika kwa Mungu Ajibuye maombi.

Hakuna wakati au mahali pasipofaa kutoa ombi kwa Mungu. Katika umati wa watu mtaani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kumsihi Mungu Atupe mwongozo wa Kiungu.

Hebu roho na ivutwe na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya anga la mbinguni. Sisi tunaweza kuwa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kwa ile kawaida ya ua linavyoligeukia jua. Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu.

Wewe huwezi kumlemea; huwezi kumchosha. Yeye hachoshwi na matakwa ya watoto Wake.

Tunapata hasara tunapopuuza fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo sisi kwa sisi katika utumishi kwa Mungu. Ikiwa Wakristo watashirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Kweli za thamani za ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa na wangeburudishana wao kwa wao.

Ni sharti tukusanyike pamoja kwa ajili ya msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa vinapaswa kuwa mada ya kutafakari, mada ya mazungumzo, na hisia zetu za furaha zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu kila baraka tunayoipokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini kila kitu kilicho katika mikono ile iliyotundikwa msalabani kwa ajili yetu.

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mbawa za sifa kwa Mungu. Tunapoonyesha shukrani zetu, ndivyo tukaribiavyo kuabudu na majeshi ya mbinguni. Wengi nyakati fulani wanatatizwa na mapendekezo ya kutilia shaka kuhusu Mungu. Mungu kamwe hatuambii tuamini bila kutoa uthibitisho wa kutosha wa kujenga imani yetu. Tunaweza kuficha uhalisia au ukweli Kwa namna tuwezavyo, ila sababu halisi ya shaka na kutokuamini, katika hali nyingi, ni kupenda dhambi. Ni sharti tuwe na nia ya dhati ya kujua Ukweli na utayari wa moyo kuitii.

Kabla ya kuingia kwa dhambi, Adamu alifurahia ushirika wa wazi na Muumba wake; lakini tangu mwanadamu alipojitenga yeye mwenyewe kutoka kwa Mungu kwa kutenda dhambi, jamii ya kibinadamu imekatiliwa mbali na upendeleo huu mkuu. Kwa mpango wa ukombozi, hata hivyo, njia imefunguliwa ambayo kwayo wakaaji wa dunia wanaweza bado kuwa na uhusiano na Mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kwa Roho Wake, na nuru ya Bwana imekuwa ikipandikizwa ulimwenguni kwa mafunuo, kupitia watumishi Wake wateule. “Watu watakatifu wa Mungu walinena kama walivyokuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” 2 Petro 1:21.

Wakati wa karne ishirini na tano za kwanza za historia ya mwanadamu, hapakuwa na ufunuo ulioandikwa (Musa aliishi miaka 2500 hivi baada ya Adamu kuumbwa, na ndiye mwandishi wa kwanza). Wale ambao walikuwa wamefundishwa na Mungu, waliwasilisha ujuzi wao kwa wengine, na maarifa haya yalipitishwa kutoka kwa baba kwenda kwa mwana, kupitia vizazi vilivyofuatana. Maandalizi ya Neno lililoandikwa yalianza wakati wa Musa.

Mafunuo yaliyovuviwa yalijumuishwa katika kitabu kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa muda mrefu kipindi cha miaka elfu na mia sita (1600), kutoka kwa Musa, mwanahistoria wa uumbaji na Sheria, hadi Yohana, mwandishi wa Kweli kuu za injili (takribani Kutoka 1500 KK hadi 100 BK).

Biblia inaelekeza kwa Mungu kama mwandishi Wake; lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na kwa mtindo wake tofauti vitabu vyake mbalimbali vinawasilisha sifa za waandishi kadhaa. Kweli zilizofunuliwa zote “hutolewa kwa pumzi ya Mungu” (2 Timotheo 3:16); lakini zinaonyeshwa kwa maneno ya wanadamu, kwani si imla, ila walipewa njozi na ndoto na wakaandika kwa maneno yao. Roho Mtakatifu ametoa nuru katika akili na mioyo ya watumishi Wake. Amewapa ndoto na maono, alama na takwimu; na wale waliofunuliwa Kweli hizi, wameonyesha wenyewe mawazo hayo katika lugha ya kibinadamu.

Amri kumi zilinenwa na Mungu Mwenyewe, na ziliandikwa kwa mkono Wake Mwenyewe. Amri Kumi ni za Mungu Mwenyewe. Tunatakiwa tuwe waangalifu sana, kwani amri za mataifa yetu tunazitilia maanani, na tunapozivunja tunapata shida, sembuse Amri za Mwenyezi Mungu? Hakuna

awezaye kushika sheria na kutembea na Mwenyezi Mungu isipokuwa amepata msaada kutoka Kwake, na Kila mwanadamu aombaye msaada huo, Mungu Yupo tayari kumpa.

## Ngazi ya Kufika Mbinguni - Mwongozo wa Kujifunzia

*Kitabu cha Ngazi ya Kufika mbinguni, ambacho kimetafsiriwa kutoka kwenye Kingereza 'Steps to the Messiah'* ni mojawapo ya vitabu vyenye mionjo ya kiroho zaidi, vinavyozingatia Masihi na kazi Yake ya ukombozi na jinsi anavyotufikisha mbinguni. Nakala ya kwanza ilichapwa mwaka wa 1891. Kitabu hiki kimetafsiriwa kwenye lugha zaidi ya 160 (hadi Mei 1985).

Asili yake ni tofauti kidogo na *The Great Controversy* . Haikutegemea maono fulani maalum. Kuanzia mwaka 1890, Ellen White aliandaa kitabu hiki kipya, akielezea kwa urahisi na kwa uwazi hatua za kuchukuliwa na wenye dhambi katika kumjia Mungu. Kitabu hicho pia kilikidhi wito wa vitabu vidogo ambavyo vingeweza kutumiwa na wainjilisti katika kuwafikia watu.

Tuna uhakika kwamba kusudi la awali la mwandishi litatimizwa tena kadri kitabu cha Ngazi ya Kufika mbinguni, kitakavyosomwa na sehemu kubwa ya kanisa kwa msaada wa Mwongozo wa Kujifunza. Hii itakuwa fursa nzuri sana ya kuwafikia washiriki wapya kwa kitabu hiki cha ibada kinachopendwa sana.

### Somo la Kwanza - Kurasa 9-36

1. Ni vyanzo gani viwili muhimu vinavyoshuhudia upendo wa Mungu? Kila kimoja kinatuambia nini? (9, 10)

2. Ingawa uvunjaji wa sheria ya Mungu umeleta huzuni na kifo, tunaweza kujifunza nini kutokana na laana hiyo? (9 , 10)

3. Shetani amejaribuje kumwakilisha Mungu vibaya kwa wenye dhambi? (10 , 11 )

4. Yesu alipokuja kuishi miongoni mwa wanadamu, Je, alimwakilishaje Mungu? (11)

5. Kazi ya Yesu ilikuwa “kuwahubiri maskini ________________, kuwaponya ________________, kuwahubiria wafungwa ________________, kuwaponya vipofu ________________, kuwaweka ________________ walioumizwa.” ( 11 )

6. Kwa nini Yesu alichukua asili ya mwanadamu? ( 12 )

7. Unafikiri kwa nini watoto wadogo walivutiwa na Yesu? ( 12 )

8. Eleza jinsi Yesu alivyorekebisha au kukemea dhambi. ( 12 )

9. Kwa sababu gani Yesu alikuwa “Mtu wa Huzuni”? ( 13 )

10. Ni nini hasa kilichovunja moyo wa Mwana wa Mungu? ( 13 )

11. Upendo wa Mungu kwa mwanadamu na dhabihu iliyotolewa vinahusianaje hasa? (13)

12. Kwa nini Yesu alikuwa dhabihu pekee inayowezekana kutolewa kwa ajili ya dhambi? ( 14 )

13. Zaidi ya dhabihu Yake kwa ajili ya wenye dhambi, Yesu amejiunganishaje na wanadamu? ( 14 )

14. Kristo ametufanyia nini zaidi ya msamaha wa dhambi? ( 15 )

## "Haja ya Mwenye Dhambi kwa Kristo"

15. Dhambi imeathirije akili ya mwanadamu? ( 17 )

16. Eleza hali ya moyo usiofanywa upya. ( 17 )

17. Mbingu ingekuwaje kwa mwenye dhambi asiyetubu? ( 17, 18 )

18. Kwa nini elimu, utamaduni, utekelezaji wa nia, na juhudi za kibinadamu, havitoshi kumleta mtu kwenye utakatifu? ( 18 )

19. Kweli au Si kweli. Kukuza wema uliopo ndani ya mwanadamu kwa asili ndiko pekee kunakohitajika ili kuokolewa. ( 18 , 19 )

20. Kwa nini haitoshi kujua kuhusu Mungu? Toa Maandiko yanayounga mkono jibu lako. ( 19 )

21. Ngazi katika ndoto ya Yakobo inawakilisha nini? ( 20 )

Kumbuka matumizi ya hii ngazi kwa Agano Jipya.

22. Andika orodha ya mawakala yaliyoorodheshwa kwa niaba ya mwanadamu ili kumwokoa. ( 21 )

23. Mungu hutumia njia gani kutuonya dhidi ya kumtumikia Shetani? ( 21, 22 )

## "Toba"

24. Fafanua toba. ( 23 )

25. Ni nini kilikuwa kibaya na toba ya Esau na Yuda? ( 23 , 24 )

26. Moyo unapofunguliwa kwa Roho wa Mungu, mwenye dhambi huathiriwaje? ( 24 )

27. Daudi alipotubu, aliomba mambo yapi? ( 25 )

28. Ni kipi kinachotangulia - toba au kuja kwa Yesu? ( 26 )

29. Maliza sentensi—"Hatuwezi kutubu tena ." ( 26 )

30. Je, inawezekana kuionea aibu dhambi bila kumjua Kristo? Kuwa tayari kujadili jibu lako. ( 27 )

31. Nini kitatokea kwa mwenye dhambi ambaye hapingi upendo wa Kristo? ( 27 )

32. Swali la tafakari: Je, nimepata jibu la shauku yangu ya kitu ambacho sina ndani ya Kristo? Kama sivyo, kwa nini sivyo? ( 28 )

33. Ni nini hutokea wakati nuru kutoka kwa Kristo inapoangaza ndani ya roho zetu? Jadili uzoefu wa Danieli na Paulo. ( 28 , 29 )

34. "Mungu haoni dhambi zote kuwa sawa kwa ukubwa; kuna viwango vya hatia katika makadirio yake, na vile vile katika makadirio ya mwanadamu." Hii ina maana gani? Jiandae kujadili. ( 30 , 31 ).

35. Kwa nini tusingoje na kujitahidi wenyewe kuwa bora zaidi kabla ya kuja kwa Kristo? ( 31 )

36. Ungemjibuje mtu anayependekeza kwamba Mungu ni mwema sana kuwaangamiza wenye dhambi? ( 31 , 32 )

37. Ungempa jibu gani mtu anayesema, “Mimi ni sawa tu au bora kuliko wale wanaojiita Wakristo?” ( 32 )

38. Je, kuna hatari gani ya kuahirisha mambo katika kuacha dhambi? ( 37 , 38 )

39. Kupuuza au kukataa neema ya Kristo kutamwathirije mwenye dhambi? ( 33 , 34 )

40. Ni faraja gani inayotolewa kwa wale wanaojaribiwa kukata tamaa kuhusu dhambi zao? ( 35 , 36 )

## Somo la Pili - Kurasa za 37-56

1. Kulingana na Mithali 28:13, hatupaswi tu kukiri dhambi zetu, bali tunapaswa kuzi __________________. ( 37 )

2. Kwa nini safari za hija na toba hazina manufaa kwa wenye dhambi? ( 37 )

3. Inapendekezwa kwamba tuungame dhambi kwa Mungu na makosa yetu kwa kila mmoja wetu. Hii ina maana gani? ( 37 )

4. Sharti la kwanza la kukubalika na Mungu ni lipi? ( 37 , 38 )

5. Malizia sentensi ifuatayo: “Sababu pekee ya kutokuwa na ondoleo la dhambi zilizopita ni ______________________________________________.” ( 38 )

6. Ungamo: Linapaswa kufanywaje? Linapaswa kutofanywaje? ( 38 )

7. Kwa nini ungamo liwe maalum, kwa kuikiri dhambi fulani? ( 38 )

8. Jadili mfano wa dhambi ya Israeli na kwa nini toba/ungamo maalum lilipaswa kufanywa. ( 38 , 39 )

9. Baada ya kukiri dhambi, ni hatua gani mbili za ziada zinazopaswa kuchukuliwa? Jadili mifano ya Maandiko. ( 39 )

10. Kwa nini ni muhimu kwa mwenye dhambi kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu ili kurekebisha kasoro za tabia? ( 40 )

11. Dhambi ya Adamu na Hawa iliathirije hisia yao ya kuwajibika kwa matendo yao? ( 40 )

12. Kwa upande mwingine, toba ya kweli itamwongoza mtenda dhambi kufanya nini? ( 40 , 41 ) Jadili mifano kadhaa ya Biblia.

## "Utakaso"

13. Pitia maelezo ya Maandiko kuhusu hali yetu ya asili kama wenye dhambi. ( 43 )

14. Ni vita gani kubwa zaidi iliyowahi kupiganwa? ( 43 )

15. Fupisha majibu:
A. Uwakilishi wa Shetani kuhusu serikali ya Mungu: ( 43 )

B. Serikali ya Mungu kama ilivyo kweli:

16. Kwa nini Mungu halazimishi utii wetu? ( 43 , 44 )

17. Orodhesha baadhi ya sanamu zinazoweza kutuzuia kumkaribia Mungu. ( 44 )

18. Ni aina gani ya dini inayopendekezwa hapa kwamba "haina thamani"? ( 44 )

19. Badala ya kuuliza ni kiasi gani tunapaswa kumpa Mungu, lengo letu linapaswa kuwa nini? ( 45 )

20. Ni jibu gani linaloweza kutolewa kwa wale wanaofikiri kwamba dhabihu kubwa sana kutoa yote kwa Kristo? ( 45 )

21. Tunabakiwa na nini tunapotoa "yote"? ( 46 )

22. Jadili kauli hii: “Mungu hatuhitaji tuache chochote ambacho ni kwa faida yetu kukihifadhi.” ( 46 )

23. Je, Mungu anawaomba watoto Wake wawe na furaha kwa ajili ya wakati ujao? Unafikiri Mkristo anawezaje kuwa na amani hata katika shida? ( 46 , 47 )

24. Unaelewaje matumizi ya nguvu ya kuchagua, au utashi? ( 47 )

25. Kuna tofauti gani kati ya kutamani kuwa mwema na kuchagua kuwa Mkristo? ( 47 , 48 )

## "Imani na Kukubali"

26. Hali ya asili ya mwenye dhambi na mwenye hatia inaelezewaje? ( 49 )

27. Ni baadhi ya njia hatuwezi kuwa na amani ya roho? ( 49 )

28. Ni baachi ya njia gani za amani zinazoweza kupatikana? ( 49 )

29. Ni hatua gani zinazopaswa kuchukuliwa baada ya kukiri dhambi? ( 49 , 50 )

30. Kwa nini tunapaswa kuamini kwamba dhambi zetu zimesamehewa? ( 50 ) Toa mfano kutoka kwa huduma ya Yesu.

31. Kwa nini mtu aliyepooza aliweza kutembea? ( 50 , 51 ) Tumia uzoefu huu katika hali yako kama mwenye dhambi.

32. Inawezekanaje kwetu kusimama mbele ya sheria ya Mungu bila aibu au majuto? ( 51 )

33. Kwa nini haiwezekani kwetu kuja kwa Mungu kwa majaribio, ili kujithibitisha? ( 52 )

34. Kwa nini maelfu hushindwa katika uzoefu wao wa Kikristo? ( 52 )

35. Tunapaswa kuwa huru kutokana na tuhuma gani? Kwa nini? ( 52 , 53 )

36. Mtenda dhambi aliyetubu anapaswa kuitikiaje juhudi za Shetani za kuiba uhakikisho wake wa kukubaliwa na Mungu? ( 53 )

37. Yeremia anaongezaje somo la upendo wa Baba yetu wa mbinguni kama linavyoonyeshwa katika mfano wa mwana mpotevu? ( 54 )

38. Isaya anatoa ulinganisho gani kati ya upendo wa Mungu na upendo wa kianadamu kwa mtoto? ( 54 )

39. Tunapomkaribia Mungu kwa ________________ na ________________, Yeye atatukaribia kwa ________________ na ________________. ( 55 )

## Somo la Tatu - Kurasa 57-84

1. KWELI AU SI KWELI. Ili kujua kama ameongoka kweli au la, mtu anapaswa kuwa na uwezo wa kufuatilia hali na wakati wa kuongoka kwake. ( 57 )

2. Yawezekanaje kujulikana kwamba Roho wa Mungu anafanya kazi katika maisha ya mtu? ( 57 )

3. Ni kwa nini tabia hiyo haifunuliwi? Na Je, inafunuliwa na nini? ( 57 , 58 )

4. Ni mambo gani yanaweza kutoa usahihi wa nje tu wa mwenendo? ( 58 )

5. Ni ushahidi gani wa ndani unaoonyesha kwamba sisi ni wa Kristo? ( 58 )

6. Tunapokuwa viumbe wapya katika Kristo, nini hutokea kwa vipaumbele vyetu, ladha zetu, na tabia zetu? ( 58 )

7. Hakuna toba ya kweli isipokuwa kuwe na ______________________________. ( 59 )

8. Mkristo wa kweli ana mtazamo gani kuhusu wajibu au dhabihu? ( 59 )

9. Tengeneza orodha ya matokeo saba katika maisha ambapo upendo ndio kanuni ya vitendo. ( 59 )

10. Wakristo wapya wanahitaji kujilinda dhidi ya makosa gani mawili? ( 59 , 60 )

11. Unafikiri tunawezaje kuepuka makosa yoyote kati ya hayo? ( 59 , 60 )

12. Ishara ya kweli ya uanafunzi ni ipi? ( 60 )

13. Unaelewaje kauli hizi: “Hatupati wokovu wetu kwa ajili ya utii wetu.” “Utii ni tunda la imani.” ( 61 )

14. Dhana au imani ya uongo hufafanuliwaje? ( 61 )

15. Hali ya uzima wa milele ikoje? ( 62 )

16. Kwa maneno yako mwenyewe, fupisha jinsi “Kristo alivyotufanyia njia ya kutorokea.” ( 62 )

17. Linganisha "imani ambayo ni tofauti kabisa na imani" na imani ambayo imeunganishwa na imani. ( 63 )

18. Kadiri tunavyomkaribia Yesu, ndivyo tutakavyoonekana kuwa na makosa zaidi. Badala ya kusababisha kukata tamaa, hii ni ushahidi wa nini? ( 64 , 65 )

19. Hisia ya dhambi zetu inapaswa kutusukuma kufanya nini? ( 65 )

20. Toa mifano miwili kutoka kwa uumbaji/maumbile iliyotumika katika Biblia kuelezea kuzaliwa kama watoto wa Mungu. ( 67 )

21. Ukuaji wa Kikristo unaonyeshwaje kutoka kwa maumbile? ( 67 )

22. Ni njia gani asili, inaonyesha kwamba hakupaswi kuwa na wasiwasi au tashwishwi katika ukuaji wa Kikristo? ( 68 )

23. Ukuaji endelevu wa Kikristo unahakikishwaje? ( 69 )

24. Kazi ya kwanza kabisa ya siku inapaswa kuwa ipi? ( 70 )

25. Tutapangaje kila siku? ( 70 )

26. Unaelewaje kauli ifuatayo: “Maisha katika Kristo ni maisha ya utulivu”? ( 70 )

27. “Ni kwa _________________ Yeye, _________________ Yeye, _________________ kikamilifu juu Yake, kwamba mtabadilishwa kuwa _________________ Yake.” ( 71 )

28. Wale wanaomtegemea Kristo kikamilifu watapata uzoefu gani? ( 71 )

29. Shetani atajaribu kugeuza mawazo yetu kwa watu gani? ( 71 )

30. Ni kwa jinsi gani tu uhusiano wa upendo kati ya Kristo na ubinadamu unaweza kuvunjika? ( 72 )

31. Yohana, mwanafunzi, hakuwa na upendo wa kawaida. Alipataje kuwa hivyo? ( 73 )

32. Ni masomo gani tunayoweza kujifunza kutokana na uzoefu wa wanafunzi baada ya Yesu kurudi mbinguni? ( 74 , 75 )

## "Kazi na Maisha"

33. Ni masomo gani ya kujifunza kutoka kwenye huduma ya malaika? ( 77 )

34. Upendo kwa Yesu utaonyeshwaje katika matendo yetu? ( 77 , 78 )

35. Ni nini kilikuwa "lengo moja kuu" la maisha ya Kristo duniani? ( 78 )

36. Ni nini kitakachoonekana kama matokeo ya neema ya Kristo katika maisha yetu? ( 78 , 79 )

37. Juhudi za kuwabariki wengine zitatutendeaje? ( 79 )

38. Kwa nini Mungu hakuruhusu kuhubiriwa kwa injili na malaika? ( 79 )

39. Orodhesha baadhi ya faida tunazopata kutokana na kufanya kazi kwa ajili ya wengine. ( 80 )

40. Ni kwa namna gani tu, tutaweza kukua katika neema? ( 80 , 81 )

41. Tunaweza kujifunza nini kutokana na miaka ya mapema ya Yesu kama seremala? ( 81 , 82 )

42. Ni somo gani muhimu linalopendekezwa kuhusu matumizi ya talanta katika mfano? ( 82 , 83 )

## Somo la Nne - Kurasa 85-104

1. Mungu huzungumza nasi kwa njia gani nne leo? ( 85 na 87 )

2. Kwa nini asili ni mojawapo ya njia bora zaidi za Mwokozi za kutufundisha? ( 85 )

3. Tengeneza orodha ya baadhi ya masomo muhimu zaidi tunayoweza kujifunza kutokana na maumbile. ( 85-87 )

4. Kwa nini Mkristo ana faida zaidi ya mtunga mashairi au mtaalamu wa asili anaposoma maumbile/uumbaji/asili? ( 87 )

5. Ni masomo gani maalum ya kujifunza kutokana na utafiti wa wahusika wa Biblia? (87, 88 )

6. Tunawezaje "kula mwili na kunywa damu" ya Kristo? ( 88 )

7. Sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika vizazi vyote itakuwaje? ( 88 )

8. Je, faida chanya ya kujifunza somo hili itakuwa nini hata sasa? ( 89 )

9. "Kadiri ________________ yetu inavyozidi kumhusu Kristo, ndivyo tutakavyozidi ________________ kwake kwa wengine na ________________ kwake kwa ulimwengu?" ( 89 )

10. Matokeo chanya ya kujifunza na kutafakari kwetu Maandiko Matakatifu yatakuwa nini? ( 89 , 90 )

11. Ni mapendekezo gani yanayotolewa kuhusu mbinu za kujifunza Maandiko? ( 90 , 91 )

12. Ni nini kinachopaswa kutangulia kujifunza Biblia? Kwa nini? ( 91 )

13. Ni msaada gani wa kianadamu unaoahidiwa katika funzo letu la Biblia? ( 91 )

14. Ni nani ambaye ni mwalimu es pekee Mwenye ufanisi wa Ukweli wa Kiungu? ( 91 )

## "Haki ya Maombi"

15. Angalia marudio ya njia nne ambazo Mungu huzungumza nasi. ( 93 )

16. Ushirika na Mungu ni wa pande mbili. Je, sehemu yetu ni ipi? ( 93 )

17. Maliza sentensi: “Sala ni ____________________________________________________.” ( 93 )

18. Ni madhumuni gani yanayopendekezwa kwa ajili ya maombi? ( 93 )

19. Taja sababu kadhaa za Yesu kuomba mara nyingi alipokuwa duniani. ( 93 , 94 )

20. Ni nini kinachowapata wale wanaopuuza maombi? ( 94 )

21. Maombi huitwa ________________ katika mkono wa imani. Andika sentensi kamili. ( 94 , 95 )

22. Masharti manne ya kujibiwa kwa maombi yametolewa. Yaorodheshe. ( 95-97 )

23. Mungu wakati mwingine hujibuje maombi yetu tunapoomba kitu ambacho hakitakuwa baraka? ( 96 )

24. Dhana inafafanuliwaje kuhusiana na sala? ( 96 )

25. Ni katika hali gani pekee tunaweza kutarajia rehema na baraka kutoka kwa Mungu tunapoomba? ( 97 )

26. Unafikiri Biblia ina maana gani inaposema tunapaswa “kuomba kwa bidii”? Tazama Warumi 12:12 . ( 97 )

27. Ni aina gani ya sala ambayo ni "uhai wa roho"? ( 98 ) Kwa nini?

28. Henoko alitembeaje na Mungu? ( 98 , 99 ) Tunaweza kufanya nini ili kutembea na Mungu?

29. Tunawezaje kuishi kama katika angahewa ya mbinguni? (99 )

30. Tukiendelea kuwa karibu na Mungu, ni nini kitatokea majaribu yasiyotarajiwa yanapokuja? ( 99 , 100 )

31. Pitia mambo mengi ambayo Mungu anatukaribisha kuyaeleza Kwake katika maombi. ( 100 )

32. Je, uhusiano kati ya Mungu na kila nafsi uko karibu kiasi gani? ( 100 )

33. Ni nini kinachoweza kuondoa mada na motisha ya maombi? ( 101 )

34. Tunapopuuza ushirika na wengine katika ushirika wa Kikristo, Je, hii inaathirije uzoefu wetu wa Kikristo? ( 101 )

35. Tunaposhirikiana katika ushirika wa Kikristo, uzoefu wetu wa Kikristo huathiriwaje? ( 101 , 102 )

36. Nini kingetokea katika uzoefu wetu wa Kikristo ikiwa tungefikiria na kuzungumza zaidi kuhusu Kristo? ( 102 )

37. Mbali na kuomba na kupokea, ni nini kingine ambacho maombi yetu yanapaswa kujumuisha? ( 103 )

38. Tunapaswa kufanya kazi kwa roho gani kwa ajili ya utukufu wa Mungu? ( 103 )

39. Ni nini kinapaswa kuwa mada ya hisia zetu zenye furaha zaidi? ( 103 , 104 )

## Somo la Tano - Kurasa 105-126

1. Ni tatizo gani hasa linalowasumbua wale walio vijana katika maisha ya Kikristo? ( 105 )

2. Ni mambo gani matatu kuhusu Mungu yanayothibitishwa na ushuhuda wenye mantiki? ( 105 )

3. Unafikiri kwa nini Mungu hajaondoa uwezekano wa sisi kuwa na shaka? ( 105 )

4. Maliza sentensi: “Imani yetu lazima itegemee ______________________________________________.” ( 105 )

Unaamini hii ina maana gani?

5. Je, unaweza kuelewa makusudi ya Mungu kwa kiasi gani? ( 106 )

6. Badala ya kutilia shaka, siri kuu za Biblia zinapaswa kutufanya tufanye nini? ( 106 , 107 )

7. Eleza jinsi Ukweli wa Biblia unavyoratibiwa kwa makundi yote ya watu ( 107 )

8. Mwamini anapaswa kuitikiaje Ukweli kwamba kuna mafumbo katika Biblia ambayo hayawezi kueleweka? ( 108 )

9. Watu wenye shaka na makafiri husemaje kuhusu kutoweza kuelewa kila kitu katika Biblia? ( 108 )

10. Kwa nini kuna nadharia na mafundisho maarufu ambayo yanatakiwa kutokea kwenye Biblia, lakini hayatoki hapo? ( 108 , 109 )

11. Kwa nini viumbe vilivyoumbwa na Bwana, havina uelewa kamili wa Mungu na kazi Zake? ( 109 )

12. Ni kwa namna gani pekee tunaweza kuelewa Neno la Mungu? ( 109 )

13. Malizia sentensi: "Mungu anataka mwanadamu atumie

________________________________________________

yake." ( 109 )

14. Watu husomaje Biblia kwa njia ambayo inaweza kusababisha madhara? ( 110 )

15. Ni nini chanzo halisi cha shaka na wasiwasi katika visa vingi? ( 111 )

16. Ni kwa njia gani pekee tunaweza kufikia Ukweli katika kujifunza Biblia? ( 111 )

17. Tunawezaje kupokea nuru na uelewa zaidi? ( 111 )

18. Uzoefu una nafasi gani katika kujenga imani yetu katika Neno la Mungu? ( 111 )

19. Ni lini ndipo tunaweza kuwa na uhakika kwamba tutapata majibu ya yote ambayo yametusumbua? ( 113 )

20. Sentesi hii inamaanisha nini? “Kupitia kila mmoja wa watoto Wake, Yesu hutuma barua kwa ulimwengu.” ( 115 )

21. Je, tunawezaje kumfurahisha Shetani? ( 116 )

22. Ni wazo gani potofu kuhusu maisha ya kidini ambalo Shetani anajaribu kuwasilisha? ( 116 )

23. Pitia masomo ya ndoto ya Ellen White ya bustani yenye miiba na maua ya waridi. ( 116 , 117 )

24. Linganisha matokeo ya kupitia upya matukio ya zamani ambayo yamekuwa ya furaha na yale ambayo yamekuwa ya kukatisha tamaa. ( 117 )

25. Fikiria ulinganifu uliopo kati ya mtoto anayelalamika na malalamiko yetu kuhusu Baba yetu wa mbinguni. ( 118 )

26. Ni madhara gani mawili yanayotokea kwa kuzungumza kuhusu mashaka? ( 119 )

27. Tunawezaje kuwaathri wengine bila kujua kwa wema au ubaya? ( 120 )

28. Eleza maisha na tabia ya Kristo. ( 120 )

29. Je, Kristo alibeba nini, popote alipoenda, ( 120 )

30. Fupisha jinsi tunavyopaswa kumwiga Kristo. ( 120 , 121 )

31. Ni nini kitakachotufanya tusiweze kuwapenda wengine? (121 ) Tunawezaje kujifunza kuwapenda wengine?

32. Unafikiri inamaanisha nini "kujikobesha shida"? ( 121 , 122 )

33. Maliza sentensi hii. “Hatupaswi kuruhusu misukosuko ______________________________________________________________.” ( 122 )

34. Ni mapendekezo gani mawili yanatolewa kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya biashara? ( 122 )

35. Katika Mahubiri ya Yesu Mlimani, ni masomo gani ya kumtumaini Mungu tunayojifunza kutoka kwa ndege? ( 123 )



36. Katika mahubiri hayo-hayo, ni masomo gani Kristo aliyatoa kutoka kuhusu yungiyungi? (water lilies)( ( 124 )



37. Ni sifa gani zinazoleta furaha, zinazotafutwa kutokana na nia za ubinafsi? ( 124 )

38. Utumishi wa Mungu unalinganishwaje? ( 124 )

39. Ni "nguzo kuu" gani tunazohamasishwa kuzikumbuka? ( 125 )

40. Tuna uhakika gani kuhusu majaribu? ( 125 )

41. Pitia thawabu za furaha za mbinguni. ( 125 , 126 )

**Tembelea -MAARIFAmtandaoni.Com au RohoYaUnabii.Org**
Unafikiri ni vitabu gani viandikwe ili kusaidia au kutafsiriwa, tupe mapendekezo yako
***Vitabu vya Kalamu ya Uvuvio vilivyotafsiriwa or self help books***

THE FOLLOWING ARE BOOKS TRANSLATED or Written in SWAHILI

1.Testimonies for the church 9 Volumes
10.Fundamentals of Christian Education
11.Pastoral Ministry
12.*The Great Controversy*
13.Counsel for the Church
14.Heaven
15.About the Angels
16.Testimonies on Sexual Behaviour, Adultery and Divorce
17.Welfare Ministry
18. Prayer
19. Short Version of Prayer
20. Gospel Workers
21. Campmeetings
22. Dress Reform
23. Mission to the Cities
24. Steps to Christ
25. Food Ministry
26. Story of Redemption
27. *Early Writings*
28. Ministry of Healing
29. Story of Redemption
30. Counsels to Teachers, Parents and Students
31. Testimonies to Ministers and 'Gospel Workers
32.Counsel in Diet and Foods-not edited
33.Early Writings
34.God's Remnant Church
35. Counsel on Health
36. Retirement Years
37. Peter's Counsel-not edited
38. Evangelism
39. *Child Guidance*
40. Adventist Home
41. Medical ministry-not edited
42. an Appeal to mothers-not edited
43. Manuscript Release Volume 1
44. The Southern Work
45 Selected Messages volume 1
46. Selected Messages Volume 2
47. Bible Commentary Volume 7a
48. Broke Blue Print
49. Medical Missionary Manual
50. Greek Strong-New Testament-Old is being done now
51. Desire of Ages

52. Tell it to the world-uambie ulimwengu
53. Path to the throne on pipeline
54. People of Providence

**Books Written**

2.Children Bible in form of 365 Devotion Swahili and English
Biblia ya watoto-Visa 407 vya Biblia katika mfumo wa Kesha
4.Layman-Mlei Swahili and Englishi
5.21st Century godly woman Mwanamke wa Karne ya 21
5.Summary of the Bible-Muhtasari wa Biblia still on editing, has not come yet
6. DO HARD THINGS-FANYA VITU VIGUMU appeal for youth-by harris translation
7. Your Health-What should you do? Jinsi ya kusaidia afya yako-English and Swahili
9. Parenting-Kuzaa na Kulea, Swahili and English
10 . 42 percent of people have not been reached
11. Teaching Children, youth and adults about issues pertaining to sexuality
12. Three angels messages
13. Mambo ya kuombea watoto wako
14. Biblia ya Ahadi na Maandishi mekundu pale Mungu/KRISTO WANAZUNGUMZA
15. BIBLIA YA KRONOLOJIA
16. NGUVU YA UKARIMU HOSPITALITY
17. NGUVU YA KUOMBEA NA KUBARIKI WATOTO WAKO
18. NATURAL HEALTH BY JAMES LUKE AND NATASHA OF TRINIDAD-TRANSLATION
19. DO HARD THINGS-FANYA VITU VIGUMU appeal for youth-by harris translation
20. Courtship 100 questions to ask and also distillation of courtship documentary on pipeline

21. Teaching a child to read Swahili

Ufafanuzi wa vitabu 66 vya Biblia kwa Kiswahili-Na majadiliano
COMMENTS ON 66 BOOKS OF THE BIBLE-ABOUT 16,000 PAGES-EACH BOOK WILL BE SEPARATED, SWAHILI AND ENGLISH

# 222 Maombi ya Biblia

Kuna maombi zaidi ya 222 kwenye Biblia, 176 katika Agano la Kale na 46 katika Agano Jipya.Maombi halisi, wala sio marejeo ya sala. Kauli zote “alipoomba, akamwomba Bwana, akaliitia Jina la Bwana,”.

Unabii 351 wa Agano la Kale Uliotimizwa Katika Yesu Kristo

Unabii--------------

Maelezo-----------

Utimilifu-----------

**<u>Mifano ya Yesu</u>**

Mifano ya viriba vipya na ngozi mpya za Divai

Mfano wa Kinara cha Taa

Mfano wa mjenzi mwenye Hekima na mpumbavu

Mfano wa Mpanzi

Mfano wa Magugu

Mfano wa Mbegu ya Haradali

Mfano wa Chachu

Mifano ya Hazina Iliyofichwa na Lulu

Mfano wa Nyavu

Mfano wa Mwenye Nyumba

Mfano wa Kondoo Anayetangatanga

Mfano wa Mtumishi Asiye na Rehema

Mfano wa Wafanyakazi katika Shamba la Mizabibu

Mfano wa Wana Wawili

Mfano wa Wapangaji

Mfano wa Karamu ya Harusi

Mfano wa Mtini

Mfano wa Wanawali Kumi

Mfano wa Talanta

Mfano wa Kondoo na Mbuzi

Mifano ya Marko

Mfano wa Mbegu Inayoota

Mfano wa Mmiliki Anayerudi

Mifano ya Luka

Mfano wa Mkopeshaji Pesa

Mfano wa Tajiri Mpumbavu

Mfano wa Watumishi Walio Macho

Mfano wa Watumishi Wenye Hekima na Wapumbavu

Mfano wa Mtini Usiozaa

Mfano wa Bwana na Mtumishi

Mfano wa Msamaria Mwema

Mfano wa Rafiki anayetafuta Mkate

Mfano wa Mahali pa Heshima

Mfano wa Karamu Kubwa

Mifano kuhusu Kuhesabu Gharama

Mfano wa Kondoo Aliyepotea

Mfano wa Sarafu Iliyopotea

Mfano wa Mwana Mpotevu

Mfano wa Meneja Mwerevu

Mfano wa Tajiri na Lazaro

Mfano wa Mjane Mvumilivu

## Miujiza ya Yesu

1. Kubadilisha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11)

2. Kufanya ishara Yerusalemu (Yohana 2:13-25)

3. Kuponywa kwa mwana wa afisa wa kifalme (Yohana 4:46-54)

4. Kuvua samaki wengi (Luka 5:3-10)

5. Kuponywa kwa mtu aliyekuwa na pepo huko Kapernaumu (Marko 1:21-28, Luka 4:33-37)

6. Kuponywa kwa mama mkwe wa Simoni Petro (Mathayo 8:14-15, Marko 1:29-31, Luka 4:38-39)

7. Kuponya wagonjwa wakati wa jioni (Mathayo 8:16, Marko 1:32, Luka 4:40)

8. Kumponya mwenye ukoma (Mathayo 8:1-4; Marko 1:40-45; Luka 5:12-15)

9. Kumponya mtu aliyepooza (Mathayo 9:1-8, Marko 2:1-12, Luka 5:18-26)

10. Kumponya mtu aliyekuwa kiwete kwa miaka 38, kwenye Bwawa la Bethzatha (Yohana 5:1-18)

11. Kuponya mkono uliopooza (Mathayo 12:9-14, Marko 3:1-6, Luka 6:6-10)

12. Kuponya watu kwenye umati uliomfuata Galilaya (Mathayo 12:14-21, Marko 3:6-12)

13. Kuponya watu wengi kabla ya kutoa mahubiri Galilaya (Luka 6:17-19)

14. Kumponya mtumishi wa akida (Mathayo 8:5-13, Luka 7:1-10)

15. Kumfufua mwana wa mjane huko Naini (Luka 7:11-17)

16. Kuponya watu wakati wa ziara ya wanafunzi wa Yohana Mbatizaji (Luka 7:18-35)

17. Kumponya mtu kipofu na bubu mwenye pepo (Mathayo 12:22-37)

18. Kutuliza bahari yenye dhoruba (Mathayo 8:23-27, Marko 4:35-41, Luka 8:22-25)

19. Kumponya mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wa Gerasa (Mathayo 8:28-32, Marko 5:1-13, Luka 8:26-33)

20. Kumponya mwanamke aliyetokwa na damu ndani (Mathayo 9:20-22, Marko 5:25-34, Luka 8:43-48)

21. Kumfufua binti wa Yairo (Mathayo 9:18-19, 23-25; Marko 5:22-24, 35-43; Luka 8:41-42, 49-56)

22. Kumponya vipofu wawili (Mathayo 9:27-31)

23. Kumponya mtu bubu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu (Mathayo 9:32-33)

24. Yesu anawaponya watu wachache baada ya kukataliwa Nazareti (Mathayo 13:53-58, Marko 6:1-6)

25. Yesu anawapa mitume Wake uwezo wa kufanya miujiza (Mathayo 10:1-8, Marko 6:7-13, Luka 9:1-6)

26. Uponyaji wa wengi huko Bethsaida (Mathayo 14:13-14 na Luka 9:10-11)

27. Kuwalisha wanaume 5000 na familia zao (Mathayo 14:16-21, Marko 6:35-44, Luka 9:12-17, Yohana 6:5-14)

28. Yesu anatembea juu ya maji (Mathayo 14:22-33, Marko 6:45-52, Yohana 6:16-21)

29. Uponyaji wa wengi huko Genesareti (Mathayo 14:34-36; Marko 6:53-56)

30. Kumponya binti wa mwanamke Mkanaani aliyekuwa amepagawa na pepo (Mathayo 15:21-28, Marko 7:24-30)

31. Kumponya kiziwi asiyeweza kusema (Marko 7:31-37)

32. Kuponya watu wengi katika na karibu na Dekapoli (Mathayo 15:29-31)

33. Kuwalisha wanaume 4000 na familia zao (Mathayo 15:29-39, Marko 8:1-10)

34. Kumponya kipofu huko Bethsaida (Marko 8:22-26)

35. Kumponya mvulana mwenye pepo (Mathayo 17:14-20, Marko 9:17-29, Luka 9:37-43)

36. Kuvua samaki akiwa na sarafu kinywani mwake (Mathayo 17:24-27)

37. Kumponya mtu aliyezaliwa kipofu huko Yerusalemu (Yohana 9:1-41)

38. Yesu anawapa mitume Wake nguvu za miujiza (Luka 10:1-17)

39. Kumponya bubu Mwanamume aliyekuwa amepagawa na pepo (Luka 11:14-28)

40. Kumponya mwanamke mwenye ulemavu wa miaka 18 (Luka 13:10-13)

41. Kumponya mtu mwenye ugonjwa wa kupooza (Luka 14:1-6)

42. Kumfufua Lazaro (Yohana 11:1-44)

43. Kuponya wanaume 10 waliokuwa na ukoma (Luka 17:11-19)

44. Kumponya Bartimayo mwenye upofu (Mathayo 20:29-34, Marko 10:46-52, Luka 18:35-43.

45. Kuponya vipofu na viwete Hekaluni (Mathayo 21:12-17)

46. Mtini unaonyauka ambao haukuzaa matunda (Mathayo 21:18-22; Marko 11:12-14, 20-25)

47. Kurejesha sikio lililokatwa (Luka 22:45-54)

48. Yesu anawatokea mitume Wake baada ya kufufuka (Yohana 20:19-21)

49. Yesu anamtokea Tomaso baada ya kufufuka (Yohana 20:24-28)

50. Kuvua samaki 153 (Yohana 21:4-11)

-----------------------------------------------------------------------------------

# 222 Maombi ya Biblia

Kuna maombi zaidi ya 222 kwenye Biblia, 176 katika Agano la Kale na 46 katika Agano Jipya.Maombi halisi, wala sio marejeo ya sala. Hizi ni Kauli zote katika Biblia kama hizi “alipoomba, akamwomba Bwana, akaliitia Jina la Bwana,”

-----------------------------------------------------------------------------------

Unabii 351 wa Agano la Kale Uliotimizwa Katika Yesu Krist

Unabii--------------

Maelezo-----------

Utimilifu-----------

1. Mwa 3:15 -Uzao wa mwanamke (kuzaliwa na bikira)- Wagalatia 4:4-5; Mathayo 1:18

2. Mwa 3:15 -Atamponda kichwa Shetani- Waebrania 2:14; 1 Yohana 3:8

3. Mwa 5:24- Kupaa mbinguni kimwili kulionyeshwa- Marko 16:19

4. Mwa 9:26-27- Mungu wa Shemu atakuwa Mwana wa Shemu- Luka 3:36

5. Mwa 12:3 -Uzao wa Ibrahimu utabariki mataifa yote-Wagalatia 3:8; Matendo 3:25-26

6. Mwa 12:7- Ahadi Iliyotolewa kwa Uzao wa Ibrahimu- Wagalatia 3:16

7. Mwa 14:18- Kuhani kwa mfano wa Melkizedeki -Waebrania 6:20

8. Mwa 14:18- Mfalme wa Amani na Haki- Waebrania 7:2

9. Mwa 14:18- Karamu ya Mwisho ilitabiri- Mathayo 26:26-29

10. Mwa 17:19 -Uzao wa Isaka (Mwa 21:12)- Warumi 9:7

11. Mwa 22:8 -Mwana-Kondoo wa Mungu aliyeahidiwa- Yohana 1:29

12. Mwa 22:18 -Kama uzao wa Isaka, atabariki mataifa yote- Wagalatia 3:16

13. Mwa 26:2-5- Uzao wa Isaka ulioahidiwa kama Mkombozi -Waebrania 11:18

14. Mwa 28:12- Daraja la kwenda mbinguni -Yohana 1:51

15. Mwa 28:14- Uzao wa Yakobo -Luka 3:34

16. Mwa 49:10 -Wakati wa kuja Kwake- Luka 2:1-7; Gal 4:4

17. Mwa 49:10- Uzao wa Yuda- Luka 3:33

18. Mwa 49:10- Aliyeitwa Shilo au Aliyetumwa- Yohana 17:3

19. Mwa 49:10 -Masihiaja kutoka kabila ya Yuda kupoteza utambulisho- Yohana 11:47-52

20. Mwa 49:10- Utii wa watu utakuwa Kwake- Yohana 10:16

21. Kutoka 3:13-15- "MIMI NIKO" Mkuu-Yohana 4:26; 8:58

22. Kutoka 12:5 -Mwana-Kondoo asiye na dosari -Ebr 9:14; 1 Pet 1:19

23. Kutoka 12:13- Damu ya Mwana-Kondoo huokoa kutoka kwa ghadhabu -Rum 5:8

24. Kutoka 12:21-27- Kristo Ndiye Pasaka yetu- 1 Kor 5:7

25. Kutoka 12:46- Hakuna mfupa wa Mwana-Kondoo utakaovunjwa -Yohana 19:31-36

26. Kutoka 15:2 -Kuinuliwa Kwake kulitabiriwa kama Yeshua -Matendo 7:55-56

27. Kutoka 15:11- Tabia Yake-Utakatifu- Luka 1:35; Matendo 4:27

28. Kutoka 17:6 -Mwamba wa Kiroho wa Israeli- 1 Kor 10:4

29. Kutoka 33:19- Tabia Yake-Mtu Mwenye Huruma -Luka 1:72

30. Mambo ya Walawi 1:2-9- Sadaka Yake yenye harufu nzuri kwa Mungu- Efe 5:2

31. Mambo ya Walawi 14:11- Mwenye ukoma kusafishwa-Ishara ya ukuhani- Luka 5:12-14; Matendo 6:7

32. Law 16:15-17- Atakufa kifo cha mara moja cha Kristo, siyo kama dhabihu kila siku- Ebr 9:7-14

33. Law 16:27- Atateseka nje ya Kamb-i Mathayo 27:33; Ebr. 13:11-12

34. Law 17:11 -Damu - uhai wa mwili- Mathayo 26:28; Marko 10:45

35. Law 17:11- Ni damu inayofanya upatanisho- Rum. 3:23-24; 1 Yohana 1:7

36. Law 23:36-37- Sadaka ya Kinywaji: “Mtu akiona kiu”- Yohana 7:37

37. Hesabu 9:12 -Hakuna mfupa Wake uliovunjwa- Yohana 19:31-36

38. Hesabu 21:9 -Kama Nyoka juu ya mti - Kristo aliinua- Yohana 3:14-18; 12:32

39. Hesabu 24:17- Wakati huo: “Nitamwona, lakini si sasa.”- Yohana 1:14; Gal 4:4

40. Kumb 18:15 -“Kweli Huyu ni Nabii Yule”- Yohana 6:14

41. Kumb 18:15-16- “Kama mngalimwamini Musa, mngaliniamini Mimi.-” Yohana 5:45-47

42. Kumb 18:18- Aliyetumwa na Baba kusema Neno Lake- Yohana 8:28-29

43. Kumb 18:19 -Yeyote asiyesikiliza lazima abebe dhambi Yake- Matendo 3:22-23

44. Kumb 21:23 -Amelaaniwa aangikwaye juu ya mti-- Gal 3:10-13

45. Yoshua 5:14-15- Kapteni wa wokovu wetu -Ebr 2:10

46. Ruthu 4:4-10 -Kristo, Ndugu yetu, ametukomboa- Efe 1:3-7

47. 1 Sam 2:35 -Kuhani Mwaminifu -Ebr 2:17; 3:1-3, 6; 7:24-25

48. 1 Sam 2:10 -Atakuwa Mfalme aliyepakwa mafuta kwa Bwana- Mathayo 28:18; Yohana 12:15

49. 2 Sam 7:12 -Uzao wa Daudi- Mathayo 1:1

50. 2 Sam 7:13 -Ufalme Wake ni wa milele -2 Pet 1:11

51. 2 Sam 7:14a- Mwana wa Mungu- Luka 1:32; Rum 1:3-4

52. 2 Sam 7:16 -Nyumba ya Daudi ilianzishwa milele- Luka 3:31; Ufu 22:16

53. 2 Wafalme 2:11- Kupaa mbinguni kimwili kuliashiria- Luka 24:51

54. 1 Nyakati 17:11- Uzao wa Daudi- Mathayo 1:1; 9:27

55. 1 Nyakati 17:12-13-Atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi milele- Luka 1:32-33

56. 1 Nyakati 17:13- “Nitakuwa Baba Yake, Yeye…Mwanangu.”- Ebr 1:5

57. Ayubu 9:32-33 -Mpatanishi kati ya mwanadamu na Mungu -1 Tim 2:5

58. Ayubu 19:23-27- Ufufuo ulitabiriwa- Yohana 5:24-29

59. Zaburi 2:1-3 -Uadui wa wafalme uliopangwa tangu mwanzo- Matendo 4:25-28

60. Zaburi 2:2 -Kumiliki cheo, Mpakwa Mafuta (Kristo)- Yohana 1:41; Matendo 2:36

61. Zaburi 2:6 -Tabia Yake-Utakatifu- Yohana 8:46; Ufu 3:7

62. Zaburi 2:6 -Kumiliki cheo Mfalme -Mathayo 2:2

63. Zaburi 2:7 -Alimtangaza Mwana Mpendwa- Mathayo 3:17; Warumi 1:4

64. Zaburi 2:7-8- Kusulubiwa na Kufufuka kulielezea- Matendo 13:29-33

65. Zaburi 2:8-9- Atatawala mataifa kwa fimbo ya chuma- Ufunuo 2:27; 12:5; 19:15

66. Zaburi 2:12 -Uzima huja kwa imani katika Yeye- Yohana 20:31

67. Zaburi 8:2- Vinywa vya watoto wachanga hukamilisha sifa Zake- Mathayo 21:16

68. Zaburi 8:5-6 -Kudhalilishwa na kuinuliwa Kwake- Ebr 2:5-9

69. Zaburi 9:7-10- Atahukumu ulimwengu kwa haki- Matendo 17:31

70. Zaburi 16:10- Hakutaka kuona uharibifu- Matendo 2:31; 13:35

71. Zaburi 16:9-11- Angefufuka kutoka kwa wafu- Yohana 20:9

72. Zaburi 17:15 Ufufuo ulitabiriwa- Luka 24:6

73. Zaburi 18:2-3 Pembe ya wokovu- Luka 1:69-71

74. Zaburi 22:1- Kuachwa kwa sababu ya dhambi za wengine- 2 Kor 5:21

75. Zaburi 22:1- “Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?”- Mathayo 27:46

76. Zaburi 22:2 -Giza juu ya Kalvari kwa saa tatu- Mathayo 27:45

77. Zaburi 22:7- Wanapiga kelele na kutikisa kichwa- Mathayo 27:39-44

78. Zaburi 22:8- “Alimtumaini Mungu, na amwokoe”- Mathayo 27:43

79. Zaburi 22:9-10- Alizaliwa Mwokozi- Luka 2:7

80. Zaburi 22:12-13- Wanatafuta kumwuua- Yohana 19:6

81. Zaburi 22:14- Damu Yake ilimwagika walipomchoma ubavuni- Yohana 19:34

82. Zaburi 22:14-15- Aliteseka sana pale Kalvari-Mark 15:34-37

83. Zaburi 22:15 -Aliona kiu -Yohana- 19:28

84. Zaburi 22:16 -Wamtoboa mikono na miguu- Yohana 19:34-37; 20:27

85. Zaburi 22:17-18- Walimvua nguo Zake mbele ya macho ya watu- Luka 23:34-35

86. Zaburi 22:18- Waligawanya mavazi Yake- Yohana 19:23-24

87. Zaburi 22:20-21- Alijikabidhi kwa Mungu- Luka 23:46

88. Zaburi 22:20-21- Nguvu za Shetani zikimchubua Mkombozi kisigino- Ebr 2:14

89. Zaburi 22:22 -Ufufuo Wake ulitangazwa- Yohana 20:17

90. Zaburi 22:27-28- Atakuwa mtawala wa mataifa- Kol 1:16

91. Zaburi 22:31- “Imekwisha”- Yohana 19:30; Ebr 10:10-12, 14, 18

92. Zaburi 23:1- “Mimi Ndimi Mchungaji Mwema”- Yohana 10:11; 1 Pet 2:25

93. Zaburi 24:3- Kuinuliwa Kwake kulitabiri- Matendo 1:11; Wafilipi 2:9

94. Zaburi 30:3 Ufufuo Wake ulitabiri- Matendo 2:32

95. Zaburi 31:5- “Mikononi Mwako naiweka roho Yangu”- Luka 23:46

96. Zaburi 31:11- Marafiki Zake walimkimbia- Marko 14:50

97. Zaburi 31:13- Wakafanya shauri la kumwua- Mathayo 27:1; Yohana 11:53

98. Zaburi 31:14-15- “Alimtumaini Mungu, sasa na amwokoe”- Mathayo 27:43

99. Zaburi 34:20- Hakuna hata mfupa Wake uliovunjika- Yohana 19:31-36

100. Zaburi 35:11- Mashahidi wa uongo walisimama dhidi Yake- Mathayo 26:59

101. Zaburi 35:19- Alichukiwa bila sababu- Yohana 15:25

102. Zaburi 38:11- Marafiki Zake walisimama mbali- Luka 23:49

103. Zaburi 38:12- Maadui walijaribu kumnasa kwa hila- Marko 14:1; Mathayo 22:15

104. Zaburi 38:12-13- alikaa kimya mbele ya washtaki Wake- Mathayo 27:12-14

105. Zaburi 38:20 -Alizunguka-zunguka akitenda mema -Matendo 10:38

106. Zaburi 40:2-5- Furaha ya ufufuo Wake ilitabiriwa- Yohana 20:20

107. Zaburi 40:6-8- Furaha Yake—mapenzi ya Baba- Yohana 4:34; Ebr 10:5-10

108. Zaburi 40:9- Alipaswa kuhubiri Haki katika Israeli- Mathayo 4:17

109. Zaburi 40:14- Kukabiliwa na maadui katika Bustani- Yohana 18:4-6

110. Zaburi 41:9- Kusalitiwa na rafiki anayemfahamu- Yohana 13:18

111. Zaburi 45:2 -Maneno ya Neema yanatoka midomoni Mwake- Yohana 1:17; Luka 4:22

112. Zaburi 45:6 -Kumiliki cheo, Mungu au Elohim- Ebr 1:8

113. Zaburi 45:7- Upako maalum wa Roho Mtakatifu- Math 3:16; Ebr 1:9

114. Zaburi 45:7-8- Yeye Anayeitwa Kristo (Masihi au Mpakwa Mafuta)- Luka 2:11

115. Zaburi 45:17- Jina Lake likumbukwe milele- Efe 1:20-21; Ebr 1:8

116. Zaburi 55:12-14- Alisalitiwa na rafiki, si adui- Yohana 13:18

117. Zaburi 55:15- Kifo kisichotubu cha Msaliti- Math 27:3-5; Matendo 1:16-19

118. Zaburi 68:18- Kuwapa wanadamu zawadi- Waefeso 4:7-16

119. Zaburi 68:18 -Alipaa Mbinguni- Luka 24:51

120. Zaburi 69:4- Alichukiwa bila sababu- Yohana 15:25

121. Zaburi 69:8 -Mgeni kwa ndugu Zake- Yohana 1:11; 7:5

122. Zaburi 69:9- Mwenye Bidii kwa Nyumba ya Bwana- Yohana 2:17

123. Zaburi 69:14-20- Uchungu wa Masihi wa roho kabla ya kusulubiwa- Mathayo 26:36-45

124. Zaburi 69:20- “Nafsi Yangu ina huzuni nyingi”- Mathayo 26:38

125. Zaburi 69:21 -Aliyepewa siki alipokuwa na kiu- Mathayo 27:34

126. Zaburi 69:26- Mwokozi Alitolewea kafara na kupigwa na Mungu -Yohana 17:4; 18:11

127. Zaburi 72:10-11- Watu wakuu wangemtembelea- Mathayo 2:1-11

128. Zaburi 72:16 -Chembe ya ngano kuanguka ardhini- Yohana 12:24-25

129. Zaburi 72:17- Imani katika Jina Lake itazaa watoto- Yohana 1:12-13

130. Zaburi 72:17- Mataifa yote yatabarikiwa Naye- Gal 3:8

131. Zaburi 72:17- Mataifa yote yatamwita mbarikiwa- Yohana 12:13; Ufunuo 5:8-12

132. Zaburi 78:12- Angefundisha kwa mifano- Mathayo 13:34-35

133. Zaburi 78:2b- Kutangaza Hekima ya Mungu kwa mamlaka- Mathayo 7:29

134. Zaburi 80:17- Mkono wa kuume wa Mtu wa Mungu- Marko 14:61-62

135. Zaburi 88 -Mateso na Laana ya Kalvari- Mathayo 27:26-50

136. Zaburi 88:8 -Walisimama mbali na kumtazama- Luka 23:49

137. Zaburi 89:27- Mzaliwa wa kwanza- Kol 1:15-18

138. Zaburi 89:27 -Imanueli ni mkuu kuliko wafalme wa kidunia- Luka 1:32-33

139. Zaburi 89:35-37- Uzao wa Daudi, kiti cha enzi, ufalme wadumu milele- Luka 1:32-33

140. Zaburi 89:36-37 -Tabia Yake-Uaminifu- Ufu 1:5; 19:11

141. Zaburi 90:2- Yeye ni wa milele- (Mika 5:2) Yohana 1:1

142. Zaburi 91:11-12 -Alitambuliwa kama Masihi, Kristo atajaribiwa- Luka 4:10-11

143. Zaburi 97:9 -Kuinuliwa Kwake kulitabiri- Matendo 1:11; Efe 1:20

144. Zaburi 100:5 -Tabia Yake-Wema Mathayo- 19:16-17

145. Zaburi 102:1-11- Mateso na Lawama za Kalvari- Yohana 19:16-30

146. Zaburi 102:25-27- Masihi Ndiye Mwana Aliyekuwepo Zamani- Waebrania 1:10-12

147. Zaburi 109:25 -Alidhihakiwa- Mathayo 27:39

148. Zaburi 110:1- Mwana wa Daudi- Mathayo 22:42-43

149. Zaburi 110:1 -Apaa hadi mkono wa kuume wa Baba- Marko 16:19

150. Zaburi 110:1 -Mwana wa Daudi aitwaye Bwana- Mathayo 22:44-45

151. Zaburi 110:4- Kuhani kwa utaratibu wa Melkizedeki- Waebrania 6:20

152. Zaburi 112:4 -Tabia Yake-Mwenye Huruma, Neema, et al- Mathayo 9:36

153. Zaburi 118:17-18- Ufufuo wa Masihi wahakikishwa -Luka 24:5-7; 1 Kor 15:20

154. Zaburi 118:22-23- Jiwe lililokataliwa ni Msingi wa pembeni mwa jengo -Mathayo 21:42-43

155. Zaburi 118:26a- Aliyebarikiwa awasilishwa kwa Israeli- Mathayo 21:9

156. Zaburi 118:26b -Atakuja Hekaluni, likiwa limesimama- Mathayo 21:12-15

157. Zaburi 132:11- Uzao wa Daudi (tunda la Mwili Wake)- Luka 1:32; Matendo 2:30

158. Zaburi 129:3- Alipigwa mijeledi -Mathayo 27:26

159. Zaburi 138:1-6 -Ukuu wa Uzao wa Daudi wawashangaza wafalme- Mathayo 2:2-6

160. Zaburi 147:3-6- Huduma ya Kristo duniani ilielezewa- Luka 4:18

161. Mithali 1:23 -Atatuma Roho wa Mungu -Yohana 16:7

162. Mithali 8:23- Aliyechaguliwa tangu milele -Ufunuo 13:8; 1 Pet 1:19-20

163. Wimbo 5:16- Yule bora kabisa- Yohana 1:17

164. Isaya 2:3 -Atawafundisha mataifa yote- Yohana 4:25

165. Isa 2:4 -Atahukumu miongoni mwa mataifa -Yohana 5:22

166. Isa 6:1- Isaya alipoona utukufu Wake -Yohana 12:40-41

167. Isa 6:8 -Aliyetumwa na Mungu -Yohana 12:38-45

168. Isa 6:9-10 -Mifano Yake huanguka kwenye masikio ya viziwi- Mathayo 13:13-15

169. Isa 6:9-12- Watakuwa Vipofu na viziwi kwa Maneno Yake Kristo-Matendo 28:23-29

170. Isa 7:14- Kuzaliwa na bikira -Luka 1:35

171. Isa 7:14- Atakuwa Imanueli-Mungu pamoja nasi- Mathayo 1:18-23; 1 Tim 3:16

172. Isa 8:8 -Anaitwa Emmanueli -Mathayo 28:20

173. Isa 8:14- Jiwe la kujikwaa, Mwamba wa kukwaza -1 Pet 2:8

174. Isa 9:1-2 -Huduma Yake itaanza Galilaya- Mathayo 4:12-17

175. Isa 9:6 -Mtoto aliyezaliwa- Mwenye Uungu na Ubinadamu- Luka 1:31

176. Isa 9:6 -Mwana aliyepewa-Uungu Luka 1:32; Yohana 1:14; 1 Tim 3:16

177. Isa 9:6- Alitangazwa kuwa Mwana wa Mungu Mwenye nguvu- Rum 1:3-4

178. Isa 9:6- Mtu wa Ajabu, Peleh- Luka 4:22

179. Isa 9:6- Mshauri, Yaatz -Mathayo 13:54

180. Isa 9:6- Mungu Mwenye Nguvu, El Gibor- 1 Kor 1:24; Tito 2:3

181. Isa 9:6- Baba wa Milele, Avi Adth -Yohana 8:58; 10:30

182. Isa 9:6- Mfalme wa Amani, Sar Shalom- Yohana 16:33

183. Isa 9:7- Ataanzisha ufalme wa milele -Luka 1:32-33

184. Isa 9:7- Tabia Yake-Mwaminifu -Yohana 5:30

185. Isa 9:7- Hakuna mwisho wa Serikali Yake, Kiti cha Enzi, na Amani- Luka 1:32-33

186. Isa 11:1- Kuitwa Mnazareti-Tawi, Nezer -Mathayo 2:23

187. Isa 11:1- Fimbo kutoka kwa Yese-Mwana wa Yese -Luka 3:23-32

188. Isa 11:2- Aliyepakwa Mafuta kwa Roho- Mathayo 3:16-17; Matendo 10:38

189. Isa 11:2- Tabia Yake-Hekima, Maarifa, na mengine- Kol 2:3

190. Isa 11:3- Angejua mawazo yao- Luka 6:8; Yohana 2:25

191. Isa 11:4- atahukumu kwa haki- Matendo 17:31

192. Isa 11:4 -Atahukumu kwa upanga wa kinywa Chake- Ufu 2:16; 19:11, 15

193. Isa 11:5- Tabia: Mwenye Haki na Mwaminifu- Ufunuo 19:11

194. Isa 11:10- Mataifa Wanamtafuta -Yohana 12:18-21

195. Isa 12:2 -Ataitwa Yesu-Yeshua -Mathayo 1:21

196. Isa 22:22- Yule aliyepewa mamlaka yote ya kutawala -Ufunuo 3:7

197. Isa 25:8- Ufufuo Ulitabiriwa- 1 Kor 15:54

198. Isa 26:19- Nguvu  Yake ya Ufufuo ilitabiriwa -Mathayo 27:50-54

199. Isa 28:16- Masihi Ndiye jiwe la pembeni la thamani -Matendo 4:11-12

200. Isa 28:16- Msingi Ulio imara 1 Kor 3:11;- Mathayo 16:18

201. Isaya 29:13- Alionyesha utii wa kinafiki kwa Neno Lake- Mathayo 15:7-9

202. Isaya 29:14- Wenye hekima huaibishwa na Neno- 1 Kor 1:18-31

203. Isaya 32:2- Kimbilio-Atakuwa mahali pa kujificha- Mathayo 23:37

204. Isaya 35:4- Atakuja na kuwaokoa- Mathayo 1:21

205. Isaya 35:5-6- Atakuwa na huduma ya miujiza- Mathayo 11:2-6

206. Isa 40:3-4- Iliyotanguliwa na mtangulizi- Yohana 1:23

207. Isa 40:9- “Tazameni Mungu wenu” -Yohana 1:36; 19:14

208. Isa 40:10- Atakuja kutuza- Ufunuo 22:12

209. Isa 40:11- Mchungaji-mtoaji wa maisha Mwenye huruma-Yohana 10:10-18

210. Isa 42:1-4- Mtumishi-kama mkombozi mwaminifu na mvumilivu- Mathayo 12:18-21

211. Isa 42:2 -Mpole na mnyenyekevu- Mathayo 11:28-30

212. Isa 42:3- Anawaletea tumaini wasio na tumaini- Yohana 4

213. Isa 42:4- Mataifa yatasubiri mafundisho Yake- Yohana 12:20-26

214. Isa 42:6 -Nuru (wokovu) wa Mataifa- Luka 2:32

215. Isa 42:1-6- Huruma Yake ya duniani kote- Mathayo 28:19-20

216. Isa 42:7- Macho ya vipofu yalifunguliwa -Yohana 9:25-38

217. Isa 43:11 -Yeye Ndiye Mwokozi pekee- Matendo 4:12

218. Isa 44:3- Atatuma Roho wa Mungu- Yohana 16:7-13

219. Isa 45:21-25- Yeye ni Bwana na Mwokozi -Wafilipi 3:20; Tito 2:13

220. Isa 45:23- Yeye atakuwa Mwamuzi- Yohana 5:22; Warumi 14:11

221. Isa 46:9-10- Anatangaza mambo ambayo hayajafanyika -Yohana 13:19

222. Isa 48:12- Wa Kwanza na Wa Mwisho- Yohana 1:30; Ufunuo 1:8, 17

223. Isa 48:16-17- Alikuja kama Mwalimu -Yohana 3:2

224. Isa 49:1- Aliitwa kutoka tumboni-Ubinadamu Wake -Mathayo 1:18

225. Isa 49:5- Mtumishi kutoka tumboni- Luka 1:31; Wafilipi 2:7

226. Isa 49:6- Atairejesha Israeli- Matendo 3:19-21; 15:16-17

227. Isa 49:6 -Yeye ni Wokovu kwa Israeli- Luka 2:29-32

228. Isa 49:6- Yeye ni Nuru ya Mataifa -Yohana 8:12; Matendo 13:47

229. Isa 49:6- Yeye ni Wokovu hadi miisho ya dunia- Matendo 15:7-18

230. Isa 49:7 -Atadharauliwa na Taifa -Yohana 1:11; 8:48-49; 19:14-15

231. Isa 50:3- Mbingu zimefunikwa na giza kwaajili ya aibu Yake- Luka 23:44-45

232. Isa 50:4 -Yeye ni mshauri Mwenye hekima na maarifa kwa waliochoka -Mathayo 7:29; 11:28-29

233. Isa 50:5 -Mtumishi aliyefungwa kwa hiari na kwa utii -Mathayo 26:39

234. Isa 50:6a -“Niliwapa mgongo Wangu wale walionipiga” -Mathayo 27:26

235. Isa 50:6b -Alipigwa mashavuni- Mathayo 26:67

236. Isa 50:6c -Alitemewa mate- Mathayo 27:30

237. Isa 52:7- Alitangaza habari njema juu ya milima- Mathayo 5:12; 15:29; 28:16

238. Isa 52:13- Mtumishi aliyetukuzwa -Matendo 1:8-11; Waefeso 1:19-22; Wafilipi 2:5-9

239. Isa 52:14- Mtumishi aliyetukana kwa njia ya kushangaza -Luka 18:31-34; Mathayo 26:67-68

240. Isa 52:15- Mataifa yalishtushwa na ujumbe wa Mtumishi- Luka 18:31-34; Mathayo 26:67 -68

241. Isa 52:15- Damu Yake iliyomwagika yanyunyizia mataifa- Ebr 9:13-14; Ufunuo 1:5

242. Isa 53:1 -Watu Wake hawakumwamini -Yohana 12:37-38

243. Isa 53:2- Ataonekana kama mtu wa kawaida -Wafilipi 2:6-8

244. Isa 53:3a- Alidharauliwa- Luka 4:28-29

245. Isa 53:3b- Alikataliwa -Mathayo 27:21-23

246. Isa 53:3c -Huzuni kubwa na sikitiko- Mathayo 26:37-38; Luka 19:41; Ebr 4:15

247. Isa 53:3d- Watu hujificha wasihusiane Naye- Marko 14:50-52

248. Isa 53:4a -Angepata uponyaji- Mathayo 8:16-17

249. Isa 53:4b -Alidhaniwa amelaaniwa na Mungu- Mathayo 26:66; 27:41-43

250. Isa 53:5a -Amebeba adhabu kwa maovu ya wanadamu- 2 Kor 5:21; Ebr 2:9

251. Isa 53:5b -Sadaka Yake hutoa amani kati ya mwanadamu na Mungu- Kol 1:20

252. Isa 53:5c -Sadaka Yake ingemponya mwanadamu dhambi- 1 Pet 2:24

253. Isa 53:6a -Angekuwa mchukua dhambi kwa wanadamu wote- 1 Yohana 2:2; 4:10

254. Isa 53:6b -Ni Mapenzi ya Mungu kwamba achukue dhambi kwa ajili ya wanadamu wote- Gal 1:4

255. Isa 53:7a- Mtumishi aliyeonewa na kuteswa- Mathayo 27:27-31

256. Isa 53:7b- Alikaa kimya mbele ya washtaki Wake- Mathayo 27:12-14

257. Isa 53:7c- Mwana-Kondoo wa dhabihu -Yohana 1:29; 1 Pet 1:18-19

258. Isa 53:8a -Alifungwa na kuteswa- Mathayo 26:47-27:31

259. Isa 53:8b -Angehukumiwa- Yohana 18:13-22

260. Isa 53:8c -Aliuawa- Mathayo 27:35

261. Isa 53:8d -Alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu- 1 Yohana 2:2

262. Isa 53:9a -Alizikwa katika kaburi la tajiri- Mathayo 27:57

263. Isa 53:9b Asiyekuwa na hatia na hakufanya vurugu- Luka 23:41; Yohana 18:38

264. Isa 53:9c- Hakuna udanganyifu au hila kinywani Mwake- 1 Pet 2:22

265. Isa 53:10a- Ni Mapenzi ya Mungu kwamba afe kwa ajili ya wanadamu- Yohana 18:11

266. Isa 53:10b- Ni Sadaka kwa ajili ya dhambi- Mathayo 20:28; Gal 3:13

267. Isa 53:10c -Atafufuliwa na kuishi milele- Rum 6:9

268. Isa 53:10d -Angefanikiwa -Yohana 17:1-5

269. Isa 53:11a- Mungu aliridhika kikamilifu na mateso Yake -Yohana 12:27

270. Isa 53:11b -Mtumishi wa Mungu angemhesabia haki mwanadamu -Rum 5:8-9, 18-19

271. Isa 53:11c- Mbeba dhambi kwa ajili ya wanadamu wote- Ebr 9:28

272. Isa 53:12a- Alimeinuliwa na Mungu kwa sababu ya dhabihu Yake- Mathayo 28:18

273. Isa 53:12b- Angetoa maisha Yake ili kuwaokoa wanadamu- Luka 23:46

274. Isa 53:12c- Alihesabiwa pamoja na wakosaji -Marko 15:27-28

275. Isa 53:12d- Mbeba dhambi za wanadamu wote -1 Pet 2:24

276. Isa 53:12e -Mwombezi kwa Mungu kwa niaba ya wanadamu- Luka 23:34; Warumi 8:34

277. Isa 55:3 -Angefufuliwa na Mungu- Matendo 13:34

278. Isa 55:4a- Shahidi -Yohana 18:37

279. Isa 55:4b -Yeye ni kiongozi na Amiri Jeshi- Ebr 2:10

280. Isa 55:5 -Mungu angemtukuza- Matendo 3:13

281. Isa 59:16a- Mwombezi kwaajili ya wanadamu kwa Mungu- Mathayo 10:32

282. Isa 59:16b- Angekuja kutoa wokovu -Yohana 6:40

283. Isa 59:20- Angekuja Sayuni kama Mkombozi wao- Luka 2:38

284. Isa 60:1-3- Angeonyesha nuru kwa Mataifa -Matendo 26:23

285. Isa 61:1a- Roho wa Mungu juu Yake- Mathayo 3:16-17

286. Isa 61:1b- Masihi angehubiri habari njema -Luka 4:16-21

287. Isa 61:1c -Angetoa uhuru kutoka kwa utumwa wa dhambi-Yohana 8:31-36

288. Isa 61:1-2a- Angetangaza kipindi cha neema- Gal 4:4-5

289. Yer 23:5-6 -Uzao wa Daudi -Luka 3:23-31

290. Yer 23:5-6 -Masihi angekuwa Mungu na Mwanadamu -Yohana 13:13; 1 Tim 3:16

291. Yer 31:22 -Alizaliwa na bikira -Math 1:18-20

292. Yer 31:31 -Masihi angeweka Agano Jipya- Math 26:28

293. Yer 33:14-15- Uzao wa Daudi- Luka 3:23-31

294. Ezek 34:23-24- Uzao wa Daudi -Math 1:1

295. Ezek 37:24-25- Uzao wa Daudi -Luka 1:31-33

296. Dan 2:44-45- Jiwe litakalovunja falme -Math 21:44

297. Dan 7:13-14a -Angepaa mbinguni -Matendo 1:9-11

298. Dan 7:13-14b- Yeye Aliyeinuliwa sana- Efe 1:20-22

299. Dan 7:13-14c -Utawala wake ungekuwa wa milele- Luka 1:31-33

300. Dan 9:24a -Atakomesha dhambi- Gal 1:3-5

301. Dan 9:24a- Atafanya upatanisho kwa ajili ya uovu- Rum 5:10; 2 Kor 5:18-21

302. Dan 9:24b- Ni mtakatifu- Luka 1:35

303. Dan 9:25- Tangazo Lake- Yohana 12:12-13

304. Dan 9:26a- Kukatiliwa mbali- Mathayo 16:21; 21:38-39

305. Dan 9:26b- Kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu- Ebr 2:9

306. Dan 9:26c- Aliuawa kabla ya kuharibiwa kwa hekalu- Math 27:50-51

307. Dan 10:5-6- Masihi katika hali ya utukufu- Ufu 1:13-16

308. Hos 11:1 -Angeitwa kutoka Misri -Math 2:15

309. Hos 13:14 -Angeshinda kifo -1 Kor 15:55-57

310. Yoeli 2:32- Atatoa wokovu kwa wanadamu wote- Rum 10:9-13

311. Yona 1:17- Kifo na ufufuo wa Kristo- Math 12:40; 16:4

312. Mika 5:2a -Alizaliwa Bethlehemu- Mathayo 2:1-6

313. Mika 5:2b -Mtawala wa Israeli- Luka 1:33

314. Mika 5:2c- Yeye ni wa milele mbele na nyuma- Yohana 8:58

315. Hag 2:6-9- Angetembelea Hekalu la pili- Luka 2:27-32

316. Hag 2:23- Uzao wa Zerubabeli -Luka 2:27-32

317. Zek 3:8 -Mtumishi wa Mungu- Yohana 17:4

318. Zek 6:12-13- Kuhani na Mfalme- Ebr 8:1

319. Zek 9:9a -Alikaribishwa kwa furaha Yerusalemu -Mathayo 21:8-10

320. Zek 9:9b -Alionwa kama Mfalme -Yohana 12:12-13

321. Zek 9:9c -Ni Masihi- Yohana wa haki 5:30

322. Zek 9:9d -Masihi angeleta wokovu- Luka 19:10

323. Zek 9:9e -Masihi angekuwa mnyenyekevu- Mathayo 11:29

324. Zek 9:9f -Aliwasilishwa Yerusalemu akiwa amepanda punda -Mathayo 21:6-9

325. Zek 10:4 -Jiwe la pembeni- Efe 2:20

326. Zek 11:4-6a -Wakati wa kuja Kwake, Israeli itakuwa na viongozi wasiofaa- Mathayo 23:1-4

327. Zek 11:4-6b- Kukataliwa kunamfanya Mungu aondoe ulinzi Wake- Luka 19:41-44

328. Zek 11:4-6c -Alikataliwa, na mfalme mwingine akawekwa mbadala Wake -Yohana 19:13-15

329. Zek 11:7- Huduma kwa "maskini," masalio waaminio- Mathayo 9:35-36

330. Zek 11:8a- Kutoamini kunamlazimisha Masihi kuwakataa- Mathayo 23:33

331. Zek 11:8b- Anadharauliwa -Mathayo 27:20

332. Zek 11:9 -Anaacha kuwahudumia wale waliomkataa- Mathayo 13:10-11

333. Zek 11:10-11a- Kukataliwa kunamfanya Mungu aondoe ulinzi- Luka 19:41-44

334. Zek 11:10-11b- Masihi angekuwa Mungu- Yohana 14:7

335. Zek 11:12-13a -Alisalitiwa kwa vipande 30 vya fedha -Mathayo 26:14-15

336. Zek 11:12-13b- Alikataliwa- Mathayo 26:14-15

337. Zek 11:12-13c- Vipande 30 vya fedha vilivyotupwa katika nyumba ya Bwana- Mathayo 27:3-5

338. Zek 11:12-13d- Masihi Ni Mungu- Yohana 12:45

339. Zek 12:10a- Mwili wa Masihi ungechomwa mkuki -Yohana 19:34-37

340. Zek 12:10b -Masihi angekuwa Mungu na mwanadamu- Yohana 10:30

341. Zek 12:10c- Masihi angekataliwa -Yohana 1:11

342. Zek 13:7a -Mpenzi wa Mungu Angekufa kwa ajili ya wanadamu -Yohana 18:11

343. Zek 13:7b -Kifo cha kikatili Alama  -Yohana 14:27

344. Zek 13:7c- Mungu na mwanadamu- Yohana 14:9

345. Zek 13:7d- Israeli walitawanyika kutokana na kumkataa- Mathayo 26:31-56

346. Zek 14:4 -Angerudi kwenye Mlima wa Mizeituni -Matendo 1:11-12

347. Mal 3:1a -Mjumbe wa kuandaa njia kwa ajili ya Masihi -Marko 1:1-8

348. Mal 3:1b -Kuonekana ghafla hekaluni- Marko 11:15-16

349. Mal 3:1c- Mjumbe wa Agano Jipya- Luka 4:43

350. Mal 4:5- Mtangulizi katika roho ya Eliya -Mathayo 3:1-3; 11:10-14; 17:11-13

351. Mal 4:6 -Mtangulizi angewageuza wengi kwenye haki- Luka 1:16-17

(Joint Base Elmendorf / Richardson)